# USAWIRI WA WATOTO KATIKA RIWAYA ZA KISASA ZA KISWAHILI ZILIZOANDIKWA NA MOHAMED SULEIMAN MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

**FLORENCE MOIGE ONDIEKI**

**Tasnifu hii ya utafiti Imewasilishwa katika Halmashauri ya Masomo ya Mafuzuili kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili (M. A) katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Egerton.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON.**

**MACHI 2015**

## UNGAMONA IDHINI

**UNGAMO**

Kazi hii ni yangu na haijawahi kuwasilishwa kwa shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

**Sahihi:----------------------------** **Tarehe:-----------------------------**

Florence Moige Ondieki.

AM12/2519/09

**IDHINI**

Tasnifu hii ya shahada ya Uzamili imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Egerton.

**Sahihi: -------------------------------** **Tarehe--------------------------------**

Prof. Mutiti James.

**Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton.**

**Sahihi: --------------------------------** **Tarehe: --------------------------------**

Dkt. Wendo Nabea.

**Idara ya Mawasiliano na Mtalaa wa Fasihi, Chuo Kikuu cha Laikipia.**

## HAKILINZI

© 2014Florence Moige Ondieki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri, kuiga au kutoa kazi hii kwa njia yoyote ile pasi na ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Chuo Kikuu cha Egerton au/ na mwandishi.

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mume wangu mpendwa Kennedy Ondieki na Wanangu ninaowaenzi, Wycliffe Ombongi na Peter Onduso. Ninawapenda kama mboni ya jicho langu kwani mlijinyima mengi kwa ajili yangu.

## SHUKURANI

Ningependa kutoa shukurani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia utulivu na afya njema wakati wote nilipokuwa nikitaalamia shahada hii ya Uzamili. Nashukuru Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa fursa ya kusomea humo. Aidha, nawashukuru kwa njia ya kipekee wasimamizi wangu: Prof. James Mutiti na Dkt. Wendo Nabea kwa kuniongoza nilipokuwa nikishughulikia tasnifu yangu. Mungu awabariki na awape maisha marefu.

Namshukuru Dkt. Ontieri Omari wa Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa kunipa ushauri kuhusu kazi yangu wakati wote nilipohitaji msaada wake. Nilipotaka kutamauka alinihimiza na kunipa msukumo wa kujizatiti ili kuhitimisha mradi niliouanza.

Nawashukuru walimu wangu Prof. Cathrine Kitetu, Prof. Francis Aswani, Dkt. Furaha Tchai, Dkt. KipkoechKipsabit kwa kunijaza hekima ambayo imekuwa nuru iliyoniongoza katika kukamilisha kozi yangu bila matatizo yoyote. Sitawasahau kwa kujitolea kwenu katika kunifundisha kozi mbalimbali na kunielekeza nilipohitaji usaidizi wenu, hususan nilipokuwa nikifanya utafiti wangu.

Ni muhimu pia kuwashukuru wahadhiri wafuatao kwa kukubali kuisoma kazi yangu katika viwango mbalimbali na kunipa ushauri: Dkt. Nancy Ayodi (Chuo Kikuu cha Maasai Mara)na Dkt. Gwachi Mayaka (Chuo Kikuu cha Laikipia). Ushauri wenu ulinisaida sana katika kuziba mianya ambayo ingeonekana katika kazi yangu. Nawashukuru wazamili wenzangu Benard Waswa, Irene Areba, na Mathew Kwambai kwa kukubali kujadiliana nami kuhusu kazi yangu. Aidha, ni muhimu kumshukuru Bw. Mule aliyekuwa akinipigia chapa kazi yangu nyakati zote nilipohitaji huduma yake. Mungu ambariki na aendelee kumpa roho safi.

Kwa wazazi Wangu ingawaje wamekuwa wendazao nawashukuru kwa kunipeleka shule na kunionyesha umuhimu wa elimu katika maisha. Namshukuru mume wangu mpendwa Kennedy na wanetu Wycliffe na Peter kwa kunipa mazingira tulivu katika kipindi chote nilipokuwa masomoni. Tumaini langu ni kwamba Wycliffe na Peter mtapita kima hiki cha masomo. Mungu awabariki na awaongezee siku za kuishi hapa duniani. Sitawasahau ndugu zangu na marafiki walionitakia mema siku zote nilipokuwa chuoni.

Mwisho, nawashukuru enyi nyote mlionisaidia kwa njia moja au nyingine nilipokuwa nikiishughulikia kazi yangu. Kusema ukweli, haiwezekani kuwataja wote waliotoa usaidizi wao. Mungu awazidishie matendo mema maishani mwenu.

## IKISIRI

Fasihi ni muhimu kwa vile inahusisha utumiaji wa lugha kisanaa kwa madhumuni ya kutubainishia utaratibu wa maisha katika jamii na kutuonyesha jinsi jamii ilivyo. Fasihi hutumbuiza, huelimisha na kuhimiza maadili kupitia mwenendo bora. Vilevile huonya na kukosoa. Utafiti huu umeshughulikia usawiri wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili, ambazo ni *Kiu, Nyota ya Rehema, Kichwa Maji* na *Rosa Mistika.* Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza usawiri wa watoto katika riwaya husika na mielekeo ya watu wazima kuwahusu wahusika watoto. Utafiti huu ulijikita katika madhumuni matatu. Kwanza ni kuchunguza uwakilishi wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili, kubainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili na kutambua mielekeo ya watu wazima kwa wahusika watoto. Watoto ambao walichunguzwa katika utafiti huu ni wa umri mdogo pamoja na vijana ambao ni wazawa waliotajwa katika riwaya husika. Hii ni kwa sababu wahusika watoto wamekuwa wakitumiwa katika kazi za fasihi kwa muda mrefu lakini hawajawahi kuangaziwa na wahakiki. Utafiti huu utawafungua wasomi wengi macho kuhusiana na usawiri wa watoto. Riwaya zilizochunguzwa ni nne: *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zilizoandikwa na Mohamed Suleiman Mohamed; *Rosa Mistika* na *Kichwa Maji* zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Uhalisia/Uyakinifu. Nadharia hii iliasisiwa na kumbo la tabaka la maendeleo. Baadhi ya waasisi wa nadharia ya uhalisia ni kama vile; Balzac, Stendhal na Flaubert. Nadharia ya uhalisia hutumiwa na watunzi kumulika matatizo katika jamii. Njia za utafiti zilizotumika katika utafiti huu ni upekuzi wa kimaktaba na mtandao. Deta iliyokusanywa ilipangwa kulingana na maswali ya utafiti na kuchanganuliwa kwa kuzingatia mkabala wa kithamano ambapo mtafiti alitoa maelezo kuhusu usawiri wa watoto. Aidha, utafiti huu ulichunguza jinsi lugha iliyotumiwa na watu wazima imewadhalilisha watoto katika fasihi. Majedwali pia yametumiwa kuonyesha muhtasari wa deta iliyokusanywa. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa watoto wanasibwana matatizo kama vile; kutolishwa vizuri, kutoelimishwa vizuri na wazazi wao, kudhulumiwa kimapenzi na kupokonywa urithi wao. Watoto walitekeleza majukumu mbalimbali kama vile; ukahaba, wizi, kulima, kupika na kuuza pombe. Aidha, utafiti huu uligundua kuwa watu wazima walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto kulingana na lugha waliyoitumia. Matusi kama vile; malaya, mwehu, nunda na mkorofi yalitumika kuwarejelea baadhi yawahusika watoto katika riwaya zilizochanganuliwa. Mwisho, mtafiti ametoa hitimishona kupendekeza mada ambazo zinaweza kutafitiwa zaidi. Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi hasa waandishi wa vitabu vya fasihi na kuwawezesha kuwakilisha watoto kwa njia chanya.

## ABSTRACT

Literature is very important because it uses language in an artistic manner for the purpose of enlightening us about people's lives in a society. It also focuses on the ways of life in a society. Literature entertains, educates, encourages and emphasizes good morals. It also warns and helps in rectifying bad behaviour. Previous research show that children characters are portrayed negatively as they are denied their rights in Kiswahili plays. This study carried out an analysis of the portrayal of children characters in four selected modern Kiswahili novels. These are *Kiu* and *Nyota ya Rehema*by Mohamed Suleiman Mohamed; *Kichwa Maji* and *Rosa Mistika* by Euphrase Kezilahabi. The main objective of this research was to investigate how children are portrayedin the selected novels. This study was based on three objectives. First it was to investigate children representation in the modern Kiswahili novels, to identify roles played by children characters in the selected novels and to discover adults' attitude towards children characters in the selectd novels.The research investigated young children and youths. This is because children characters have always been used in literary works for a long time but are never focused on by critics. This research forms an eye opener on the portrayal of them. The study was premised on the theory of Realism which was founded by the Progressive Class in France. Among the founders were people like, Balzac, Stendhal and Flaubert. Realism theory is used by writers to highlight things that take place in the society. To generate data, a library based design and internet were used. The generated data was analysed on the basis of of research questions. The qualitative research design was used whereby the researcher gave explanations on the portrayal of children characters and the language used by adults towards children and its effects on them. Tables were used to show the summary of the collected data. The findings of this study disclosed that children characters face challenges like not being fed well, not educated, they are abused sexually and are denied inheritance of their parents' property. They played roles like; prostitution, theft, digging, preparing and selling traditional beer.The findings also showed that adults had negative attitudes towards children characters in the analysed novels. The deamining language they used proved this clearly. Abusive words like; prostitute, mad, wild cat and nuisance were used to refer to some of the children characters in the analysed novels. Finally, the researcher gave the summary of the study and recommendations on the areas for further research. It is hoped that the findings of this study will help scholars more especially the authors of literature books to portray children characters positively.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** ........ **ii**
**IDHINI** ........ **ii**
**HAKILINZI** ........ **iii**
**TABARUKU** ........ **iv**
**SHUKURANI** ........ **v**
**IKISIRI** ........ **vi**
**ABSTRACT** ........ **vii**
**YALIYOMO** ........ **viii**
**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ **xi**
**SURA YA KWANZA** ........ **1**
**UTANGULIZI** ........ **1**
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.2 Suala la Utafiti ........ 3
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 3
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 4
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 4
1.6 Upeo wa Utafiti ........ 5
1.7 Maelezo ya Istilahi ........ 6
**SURA YA PILI** ........ **7**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** ........ **7**
2.1 Utangulizi ........ 7
2.1.1 Uwakilishi wa Watoto katika Fasihi ........ 7
2.1.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Majukumu na Jinsia ya watoto katika fasihi ........ 9
2.1.3 Mielekeo ya Watu Wazima na Matajiri kwa Watoto ........ 10
2.2 Misingi ya Nadharia ........ 13
**SURA YA TATU** ........ **16**
**MBINU ZA UTAFITI** ........ **16**
3.1 Utangulizi ........ 16
3.2 Njia za Utafiti ........ 16
3.3 Vifaa vya Utafiti ........ 16
3.4 Uteuzi wa Sampuli ........ 16
3.5 Ukusanyaji wa Deta ........ 17

3.6 Uchanganuzi wa Deta....................................................................................................18
**SURA YA NNE ........................................................................................................... 20**
**UWASILISHI NA UCHANGANUZI WA DETA ..................................................... 20**
4.1 Utangulizi .................................................................................................................20
4.2 MatatizoYanayowasibu Wahusika Watoto ...............................................................20
4.2.1 Kufukuzwa Nyumbani.......................................................................................... 20
4.2.2 Kunyimwa Uhuru wa Kujieleza ............................................................................ 23
4.2.3 Kutosomeshwa na Wazazi wao ............................................................................. 24
4.2.4 Kupokonywa Urithi ............................................................................................... 27
4.2.6 Kudhulumiwa Kimapenzi....................................................................................... 33
4.2.7 Kunyimwa Uhuru wa Kutangamana na Marafiki Zao .......................................... 43
4.2.8 Kubaguliwa kwa Jumla .......................................................................................... 45
4.2.9 Kutukanwa............................................................................................................. 46
4.2.10 Jedwali 1: Muhtasari wa Matatizo Yanayowasibu Wahusika WatotoKatika Riwaya za Kisasa za Kiswahili. .................................................................................................... 48
4.3Majukumu Yanayotekelezwa na Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili ................50
4.3.1 Kuchuma Rasilimali ................................................................................................ 50
4.3.2 Kuwalea Wadogo Zao ............................................................................................. 64
4.3.3 Kusoma.................................................................................................................... 64
4.3.4 Kuteka Maji ............................................................................................................. 66
4.3.5 Jedwali 2: Muhtasari wa Majukumu Yanayotekelezwa na Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili ....................................................................................................... 66
4.4Mielekeo ya Watu Wazima na Matajiri kwa Watoto.....................................................68
4.4.1 Mielekeo ya Watu Wazima Katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi........................... 68
4.4.2 Mielekeo ya Watu Wazima Katika Riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed .......... 71
**SURA YA TANO ........................................................................................................ 76**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................ 76**
5.1 Utangulizi ..................................................................................................................76
5.2 Muhtasari....................................................................................................................76
5.3 Hitimisho....................................................................................................................77
5.3.1 Kuchunguza Uwakilishi wa Watoto katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili................ 77
5.3.2. Kubainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili..................................................................................................................... 77

5.3.3. Kutambua mielekeo ya wahusika matajiri/watu wazima kwa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili. ........................................................................................................ 78
5.4 Mapendekezo ........................................................................................................................80
**MAREJELEO ......................................................................................................................... 82**

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 1:** Muhtasari wa Matatizo Yanayowasibu Wahusika Watoto Katika Riwaya za kisasa za kiswahili………………………………………………………………………………………….…...50

**Jedwali 2**: Muhtasari wa Majukumu Yanayotekelezwa na Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili ……………………………………………………………………………….70

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Kuna tanzu kadhaa katika fasihi andishi kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi, shajara, wasifu na tawasifu. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa riwaya. Riwaya ina umuhimu maishani kwa sababu humulika, hukosoa, huelimisha na kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Riwaya ya kisasa ya Kiswahili ilianza kujitokeza mwishoni mwa karne ya 19 na ilikua kutokana na hadithi za fasihi simulizi. Kuja kwa Wazungu (karne 19 na 20) kulikuwa ni hatua ya maendeleo ya fasihi nathari ya Kiswahili. Mwingereza Edward (1879), Mjerumani Velten (1907) na Buttner (1894) walikuwa wa kwanza kunukuu ngano za fasihi simulizi kwa maandishi ya hati za Kilatini. Baadaye zilichapishwa na kutumiwa katika shule za msingi.

Baadaye, riwaya za Wazungu na Waarabu ziliweza kutafsiriwa. Kati ya riwaya za kwanza zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ni *Mashimo ya Mfalme Suleimani* (King Solomon`s Mines) na *Safari ya Goliva* (Gulliver's Travels). Baada ya miongo ya thelathini ndipo tungo za fasihi nathari zilipodhihirika ambazo si za mapokeo na zilikuwa zimebuniwa kwa hati za Kilatini. Kutokana na usomaji, ile hamu ya uandikaji ilizuka miongoni mwa wenyeji.

Kuanzishwa kwa halmashauri ya usanifishaji kuliwatia watu moyo wa kubuni na kuandika hadithi za Kiswahili. Kuanzia mwongo wa 40, riwaya zilijikita zaidi katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Mtindo wa nyingi ulikuwa ule wa fasihi simulizi. Kati ya hizo ni*Kurwa* na*Doto* (Farsy), na *Lila na Fila* (Kiimbila).

Riwaya za Kiswahili zimekuwa zikijikita katika maudhui mbalimbali kutegemea wakati zilipoandikwa. Kwa mfano, zile zilizoandikwa kati ya miaka ya 1950 na 1960 zilitawaliwa na fantasia ambapo maudhui yalikuwa ya dini, utamaduni, maadili na aila. Mfano mzuri ni riwaya za Shabaan Robert kama vile *Kusadikika* na *Kufikirika* zilizoangazia mambo ya kidhahania. Kwa hivyo, hazingeweza kuwahamasisha watu kuhusu haki zao. Mwishoni mwa miaka ya 1960 na 1970 na vilevile mwanzo wa miaka ya 1980 kazi za kihalisia zilichukua nafasi kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Wasomi wengi walidai kuwa licha ya nchi za Afrika Mashariki kujinyakulia uhuru, uhuru wao ulikuwa ni wa bendera tu na kuwa viongozi walikuwa wasaliti wa nchi zao. Waandishi wa miaka ya 1970 walitumia kazi zao kuwahamasisha wanajamii kuhusu haki zao. Mohamed (1981) anasema kuwa waandishi

wanastahili kuongozwa na itikadi za kihalisia wanapoandika kazi za fasihi. Mawazo sawa na haya yalitolewa na Wamitila (2002) na Ngugi (1981) wanaposema kuwa kazi za fasihi zinastahili kushughulikia yanayotendeka katika jamii.

Baadhiya riwaya zilizoanza kushughulika na mgongano wa kitamaduni uliotokana na hali ya kiuchumi-jamii ni kama vile M. S. Mohamed katika (*Kiu* na *Nyota ya Rehema*), Kezilahabi E. katika (*Kichwa Maji* na *Rosa Mistika*). Watunzi hawa walijikita katika uhalisia kwa sababu walitaka kuhamasisha jamii kuhusu haki zao ikizingatiwa kwamba wakati huu ndio jamii za Afrika Mashariki zilikuwa zimepata uhuru na jamii hizi zilikuwa zinaanzakukuza taaluma zao. Hatimaye kuna zile zilizoanza kushughulikia maswala ya kisiasa hasa katika Afrika ya Mashariki.

Katika usomi wa fasihi ya watoto, kumeonekana kuwa na ubaguzi wa kijinsia wakati wa kuwapa wahusika majukumu. Hili linadhihirika wazi kutokana na wanayosema wataalamu mbalimbali wakiwemo Ernst (1995), Jett na Masland (1993) wanaodai kuwa wavulana hupewa majukumu ya kupigania na kukomboa ilhali wasichana hupewa jukumu la kulinda maslahi tu. Madai sawa na haya yalitolewa na Fox (1993) aliposema kuwa wahusika wasichana hudhihirishwa kama wapendwa, washamba, wanaokubali kila kitu na wanaotegemea. Wavulana nao kwa upande mwingine wanaonyeshwa kuwa wenye uwezo wa kuvumbua na kujitegemea. Ingawajeuwakilishi wa wahusika watoto katika tamthilia umefanywa, unaonyesha kuwa wamewakilishwa kwa njia isiyofaa lakini uwakilishi huu si bayana.Mtafiti alishawishiwa na tafiti za awali na akawa na shauku ya kuendeleza usawiri wa watoto katika fasihi.

Pengo lililopo ni kwamba jinsi ambavyo watoto wamewakilishwa katika kazi za sanaa za miongo ya sabini, katika janibu za Tanzania haijawahi kushughulikiwa katika usomi wa fasihi. Mtafiti alichanganua usawiri wa watoto katika riwaya nne za kisasa ambazo zimeandikwa na watunzi wawili tofauti kwa wakati maalum. Hii ni kwa sababu Ndung'o(1997) anasema;

> ... fasihi haibuki kutoka ombwe tupu, fasihi huibuka kutokana na jamii maalum ya wakati maalum. Fasihi ni zao la jamii. Inatumiwa kama kioo na kama kioo humulika vipengee vya maisha vya jamiiinayohusika.

Baadhi ya vipengele vya kimaudhui vilivyochunguzwa ni kama vile; dhuluma ya kimapenzi, kupokonywa urithi, kubaguliwa kielimu, watoto kufukuzwa nyumbani, na kunyimwa uhuru

wa kutangamana na wenzao. Vilevile, ukahaba, pombe, malezi,wizi na usomi ni vipengele vilivyochunguzwa. Lugha inayotumika ili kutambua mielekeo ya watu wazima kwa watoto pia ilichunguzwa. Hapa mtafiti alichunguza vifungu vya maneno, msamiati na sentensi zilivyojitokeza katika riwaya husika.

Kiini cha utafiti huu kilikuwa ni kuchanganua watoto katika riwaya za *Nyota ya Rehema, Kiu, Rosa Mistika* na *Kichwa maji*. Mohamed Suleiman Mohamed na KezilahabiEuphrase waliandika riwaya hizi miaka ya 1970. Hii ilikuwa ni enzi ya usasa ambapo haki mbalimbali za kibinadamu zilithaminiwa. Lakini riwaya sasa imeingia katika enzi tofauti ambayo ni baada -ya –usasa. Utafiti huu ulimulika watoto katika riwayahusika kwa kuangalia uwakilishi wao kwa jumla na umuhimu wa kubadili uwakilishi huu. Watoto wanastahili kusaidiwa kukuza vipawa vyao badala ya kudhulumiwa.

## 1.2 Suala la Utafiti

Katika karne hii ya ishirini na moja, suala la haki za kibinadamu, wakiwemo watoto linazidi kutiliwa mkazo. Kumekuwa na rai kuwa watoto hunyimwa haki zao na wanajamii na hivyo limekuwa ni suala nyeti. Fasihi huakisi yaliyomo katika jamii. Mohamed na Kezilahabi wanaweka wazi yanayofanyika katika jamii zao kupitia riwaya hizi. Watoto ni muhimu katika fasihi. Aghalabu huwa wanasawiriwa kwa njia hasi lakini usawiri wao si bayana. Jinsi ambavyo watoto wamesawiriwa katika kazi za sanaa za miongo ya sabini katika janibu za Tanzania haijawahi kushughulikiwa katika usomi wa fasihi. Bado riwaya hizi ndizo mwafaka zaidi maadamu riwaya ya Kiswahili imeingia katika baada-ya-usasa ambapo inajikita katika mazingaombwe.Halihii imepelekea kuweko kwa pengo la kielimu na kumshawishi mtafiti kuwa na hamu ya kuhakiki riwaya za Kiswahili ili aweze kutambua jinsi wahusika watoto wanashughulikiwa na kusawiriwa. Swali kuu lililoko ni ikiwa watoto wamepewa haki katika majukumu na hadhi na wanajamii katika fasihi. Utafiti huuulichunguza usawiri wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kudhihirisha usawiri wa watoto katika riwaya nne teule za kisasa za Kiswahili. Mtafiti alitimiza lengo hili kwa:

i. Kuchunguza uwakilishi wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.
ii. Kubainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili.

iii. Kutambua mielekeo ya wahusika matajiri na watu wazima kwa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je, watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili wamewakilishwa vipi?
ii. Katika riwaya za kisasa za Kiswahili, watoto wana majukumugani muhimu wanayoyatekeleza?
iii. Wahusika matajiri na watu wazima kwa jumla wana mielekeo gani kwa wahusika watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Inatarajiwa kuwa matokeo ya utafiti huu yatasaidia kufahamishawasomi wengi kuhusiananamasuala ya kihalisia ambayo yametumika katika riwaya za Mohamed na Kezilahabi. Inatazamiwa kuwa uchunguzi huu utatoa mchango katika usomi wa Kiswahili hasa katika uandishi wa vitabu vya fasihi. Vilevile, waandishi wataweza kuviangalia upya ili kubadilisha uwakilishi wa watoto katika fasihi andishi. Hii ni kwa sababu watoto na vijana wanaposoma riwaya za Kiswahili na kugundua kuwa mara nyingi wahusika watoto wamehusishwa na mambo mabaya, wanaweza kuwa na mielekeo hasi kwa fasihi andishi. Matokeo ya utafiti huu huenda yakachangia katika ukuaji na kupendwa kwa fasihi nchini Kenya na kote barani Afrika.

Inatumainiwakuwa uchunguzi huu utaweka wazi uwakilishi wa watoto katika fasihi. Hili litawezekana kupitia Taasisi ya Kuendeleza Mtaala wa Elimu nchini Kenya (KICD) ambayo inajishughulisha na ukaguzi na uchaguzi wa vitabu bora vinavyostahili kutumika katika shule na vyuo. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yatasaidia taasisi hii katika uchaguzi wa vitabu bora vya fasihi vitakavyotumika katika shule za upili na vyuo vikuu. Aidha, uchanganuzi huu utasaidia serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa vile yatagundua ni haki zipi watoto hunyimwa katika jamii. Wamitila (2000) akimnukuu Lenin anasema kuwa fasihi ni kioo cha jamii na hivyo basi, matokeo ya utafiti huu wa kifasihi yatafanya mashirika haya kushughulikia tatizo hili wakati wa kudurusu sheria zinazohusiana na haki za watoto.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia utanzu wa riwaya. Kuna riwaya nyingi ambazo zimeandikwa na waandishi mbalimbali. Utafiti huu ulijihusisha na riwaya nne za kisasa za Kiswahili ambazo zimeandikwa na watunzi wawili tofauti. Riwaya hizi ni *Nyota ya Rehema* na *Kiu* iliyoandikwa na Mohamed, *Kichwa Maji* na *Rosa Mistika* za Kezilahabi. Sababu ya kuteuliwa kwa riwaya hizi nne ni kwamba zinaafikiana na lengo, madhumuni na nadharia ya utafiti huu. Waandishi hawa wamezingatia muktadha wa mahali kwa sababu kazi hizi zilikuwa zikishika Tanzania yote. Kezilahabi aliwakilisha bara yaani Ukerewe, naye Mohamed visiwani yaani Unguja. Vilevile, riwaya za Kiswahili katika miaka ya sabini zinazionyesha jamii za Afrika Mashariki zikiwa katika hali ya migongano baina ya vijana na watu wazima, na hivyo basi matukio katika riwaya husika yanaashiria hali halisi katika jamii. Katika miaka ya sabini fasihi ya Kiswahili ilikuwa imeanza kupevuka. Aidha, ni wakati huu jamii hizi za Afrika Mashariki zilikuwa zimepata uhuru na zilikuwa zimeanza kukuza taaluma yao. Ingawa kuna masuala anuwai ambayo huzingatiwa katika uhakiki wa riwaya, utafiti huu hasa ulihusu watoto. Ulichunguza usawiri wa watoto kwa jumla. Uwakilishi wao, majukumu wanayotekeleza na mielekeo ya wahusika  watu wazima na matajiri kwa watoto.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

**Haki:** Mambo, vitu au mahitaji ya kimsingi wanayostahili kupewa wanadamu wote na wanajamii kama vile; kuruhusiwa kutangamana na marafiki zao, kurithi mali ya wazazi wao, kuelimishwa, kutodhulumiwa kimapenzi na kutofukuzwa nyumbani katika riwaya husika.

**Jukumu:** i).Tendo la makosa.

ii).Wajibu.

**Kioo:**Mwongozo unaoonyesha mwelekeo wa jamii.

**Kudurusu:** Kupitia tena maandishi yaliyoandikwa zamani kwa madhumuni ya kusahihisha, kuongeza au kuboresha ili kutoa chapisho jipya.

**Kutia chumvi:** Kusifu kitu kupita kiasi.

**Mielekeo:** Mawazo; misimamo.

**Mtoto:**Mhusika yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na miwili katika riwaya zilizochunguzwa.

**Nafasi:** Cheo

**Riwaya ya kisasa:**Riwaya iliyoandikwa kati ya 1970 na 1980 na ilijihusisha na maudhui ya uongozina usaliti wa kisiasa. Riwaya hii ni tofauti na riwaya mpya kwa sababu riwaya mpya iliandikwa kuanzia miaka ya 1990 na inajikita katika maudhui ya udhahania na mazingaombwe.

**Uhalisia:** Matendo, haliau vitu vinavyoweza kubadilika na kutendeka katika maisha ya binadamu ya kila siku.

**Vijana:** Mhusika wa makamo (umri wa miaka 12 hadi 18) katika riwaya zilizochunguzwa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alipitia maandishi yanayohusu dhana ya wahusika kwa jumla na wahusika watoto katika fasihi andishi na fasihi ya watoto. Vilevile, sura hii imeangazia maandishi yaliyochapishwa kuhusu majukumu yanayotekelezwa na watoto katika fasihi. Aidha, mielekeo ya watu wazima na matajiri kuwahusu wahusika watoto katika tamthilia na riwayaimeangaziwa. Hatimaye, mtafiti ameelezea nadharia na mikabala iliyomwongoza.

### 2.1.1 Uwakilishi wa Watoto katika Fasihi

Murning ( 2007) anaangazia wahusika watoto katika riwaya zake za Kiingereza. Hata kama wahusika walikuwa watoto, alikusudia zisomwe na watu wazima. Vilevile, watoto anaozungumzia si wale wa umri mdogo bali wale wakubwa. Alisema kuwa wahusika watoto si wahusika watu wazima lakini wanastahili kuwakilishwa vizuri kwa uaminifu kama wahusika watu wazima. Naye Austen (1975) anasema kuwa mwanzoni mwa karne ya 19, waandishi wengi wa riwaya waliandika kuhusu wavulana na wasichana waliokuwa wakitafuta wazazi wao. Kwa sababu ya vifo, watoto wengi walibaki wakiwa mayatima. Austen aliandika kuhusu wahusika watoto na aligusia madhara yaliyosababishwa na vifo vya wazazi. Vilevile, alisema kuwa wahusika watoto wengi wangekuwa na ubinafsi kwa vile hawakupata mwongozo kutoka kwa wazazi wao. Habari sawa na hizo kadhalika ziliandikwa na kikundi cha wanawake kilichojulikana kama *The Bronte Sisters* ( 1847).

Waandishi wengi walikuwa na shauku ya kutaka kujua fikra ya watoto mayatima na wakaweza kufungamanisha huzuni na ile hali ya mtoto kuwa yatima. Hili liliweza kujidhihirisha katika drama na katika watoto waliokuwa hawajabaleghe na ambao hawakuwa wameingiliwa na maoni ya wazazi wao. Aidha,Dickens (1978) anasema kwamba wahusika watoto wengi walikuwa mayatima katika uandishi wake. Alielezea jinsi wahusika watoto wawili Oliver Twist na David Copperfied walivyoteswa na walinzi wao hadi kufukuzwa baada ya kutaka kuongezewa chakula. Kazi za Dickens pakubwa ziliangazia watoto mayatima na walioteswa. Utafiti huu ni tofauti na utafiti wao kwa sababu mtafiti alichunguza watoto waliokumbwa na masaibu mbalimbali.

Mutua (2013) alichanganua hadithi fupi za watoto. Alishughulikia kazi za Nyambura Mpesha. Alitambua kuwa, waandishi wanaotumia mbinu ya fantasia huwa na lengo la kutoa mafunzo muhimu kwa watoto kwa njia inayoburudisha na yenye kukumbukika kwa wepesi. Aidha, utafiti wake uligundua kuwa, pana uwezekano kwamba watoto wanaosoma fantasia kwa wingi huwa na ubunifu mkubwa. Sawa na utafiti huu, Mutua alijihusisha na wahusika watoto. Tofauti na utafiti huu ni kwamba, Mutua alitumia mbinu ya fantasia ambayo inasaidia kuficha habari ambazo watunzi hawapendelei kuzitoa kwa njia ya moja kwa moja. Katika utafiti huu, mbinu ya uhalisia ndiyo imetumika ambapo mtunzi anaandika kulingana na yale anayoyaona katika jamii yake. Vilevile, alishughulikia kazi za mtunzi mmoja ilhali utafiti huu ulichunguza kazi zawatunzi wawili tofauti. Mwisho, alishughulikia hadithi fupi lakini utafiti huu ulishughulikia riwaya. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa na umuhimu wake kwani ulionyesha uwakilishi wa watoto katika fasihi. Burnett (1995) alihadithia kuhusu Sarah Crew ambaye licha ya kutokuwa na mama, alimpoteza babake ambapo kifo cha babake kilipelekea Sarah kuteswa na mwalimu wake mkuu shuleni hadi alipokombolewa na marafiki zake.

Fasihi kama kioo cha jamii, hutumulikia yaliyomo katika jamii husika. Kwa mfano, Wamitila (2004:196) anaelezea kuhusu sifa za mhusika mtoto Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Anasema kuwa maisha ya Rehema ni ya kutisha na yanategemea majaliwa. Anaendelea kusema kuwa  anakataliwa na babake mzazi, analazimika kutoroka nyumbani, anaishi maisha ya dhiki mjini, na anabughudhiwa na mwajiri wake.

Rose (1991) alidai kuwa watoto katika familia kubwa walikuwa ni wafanyikazi nyumbani na wazazi walikuwa wakali kwa watoto wao kuliko waajiri wa viwandani. Ingawa utafiti wake ulikuwa wa Kisosholojia, unasaidia kuweka wazi masaibu yanayowakumba watoto katika jamii. Unakaribiana pakubwa na utafiti huu kwa sababu utafiti huu ulichunguza wahusika watoto wanavyochukuliwa na jamii nzima kwa ujumla. Rose aliandika jinsi watoto walivyochukuliwa na wazazi wao na watu wengine matajiri. Alionyesha vile watoto wengi walikuwa wakiteswa na waajiri wao kama vile kupewa chakula kidogo, mahali pabaya pakulala na mshahara duni. Alisema kuwa unywaji wa pombe kwa wazazi, uliwafanya wawe wakatili kwa watoto wao. Utafiti huu katika Shirika la ajira ya Watoto ni tofauti na utafiti huu kwa vile Rose hakuangalia wahusika watoto katika riwaya bali katika mazingira yao ya kila siku kama vile nyumbani na viwandani. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti wetu kwa vile umeonyesha taswira ya mtoto katika jamii kwa ujumla.

### 2.1.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Majukumu na Jinsia ya watoto katika fasihi

Wahakiki wengi wa fasihi ya watoto hudokeza kuwa watoto si wa kiwango kimoja, wanatofautiana kijinsia, kikabila, kidini na kadhalika. Wahakiki wa fasihi ya watoto kama vile Lissa (1987), alishughulikia tofauti ya usomaji baina ya wasichana na wavulana katika fasihi ya watoto. Wanafafanua zaidi kuhusu watoto na kudai kuwa watoto hutawaliwa na watu wazima wakiwemo wahakiki wa fasihi ya watoto kwa sababu watu wazima huzungumza kwa niaba ya watoto badala ya kuwapa nafasi ya kujieleza. Hata hivyo wahakiki hawa hutofautiana kuhusu "uhalisi" kuhusu watoto kujieleza wenyewe na kwa hivyo ni vitabu vipi vitakavyowafaa. Hii imeangazwa na waandishi kama Hunt (1991), Nodelman (1992), John (1992) na McGills( 1996).

Lesnik (1994 na 2004) anauendeleza mjadala huu kwa kudai kuwa utambulisho wa watoto huumbwa na watu wazima. Wao ndio huamua utambulisho wa watoto kwa sababu husema kila kitu kwa niaba ya watoto. Mtaalamu huyu alisema kuwa wasomi wengi huchukulia fasihi ya watoto kama maandishi tu, na kuchunguza matini kama matini bila kuzingatia hadhira. Stephens na McCallum (1998) wanajadili aina tofauti za maandishi ya fasihi ya watoto. Rose (1984) anachunguza sifa bainifu za tanzu hizi ilhali Nodelman (1992) anachunguza jinsi maneno yanavyounganishwa katika matini na kuwakilishwa kupitia michoro katika vitabu vilivyo na michoro. Kwa wale wanaolenga utamaduni, huchunguza fasihi ya watoto kama sehemu ya utamaduni. Kwao fasihi ya watoto ni zao linalotumiwa kama vipengele vingine vya utamaduni wa watoto: michezo ya video, televisheni.

Ernst (1995), Jett na Masland (1993) wanasema kuwa wavulana hupewa majukumu ya kupigania na kukomboa ilhali wasichana hupewa jukumu la kulinda maslahi,kuwa wazazi na malkia wanaohitaji kuchungwa. Temple (1993) ameandika kuwa wahusika watoto wa kike hufaulu kutokana na usaidizi wa watu wengine ilhali wavulana hupata ufanisi kutokana na juhudi zao wenyewe. Aidha, Fox (1993) anadai kuwa wahusika wasichana hudhihirishwa kama wapendwa, washamba, wanaokubali kila kitu na wanaotegemea. Kwa upande mwingine wavulana wamesawiriwa kama wenye uwezo wa kuvumbua na wa kujitegemea. Wazo sawa na hili liliendelezwa na Rudman (1995). Ameandika kuwa wasichana wanaodumisha sifa za ukakamavu wanakiuka kaida. Hii ni kwa sababu wavulana ndio wanastahili kuwa wakakamavu.

### 2.1.3 Mielekeo ya Watu Wazima na Matajiri kwa Watoto

King`ala (1986) alifanya utafiti katika tamthilia ya *Uasi*. Aligundua kwamba utamaduni uliwafanya wazazi kuwapotosha watoto. Alionekana kuegemea upande wa watoto kwa sababu aliandika kuwa wazazi ni lazima wathamini hisia za watoto wao. Aligundua kuwa watoto wengi hufanywa kuwa watumwa na kuwa, wao hupagazwa na masharti mengi ya wazazi wao. Utafiti wa King`ala ulitofautiana na utafiti huu kwa vile hakuzingatia suala la majukumu yanayotekelezwa na watoto na mielekeo ya wahusika matajiri kwa wahusika watoto. Hata hivyo, utafiti wa King`ala ulifaa katika utafiti huu kwa sababu ametaja mateso ambayo ni baadhi ya vipengele muhimu vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu.

Vilevile, King`ala (1986) alihakiki tamthilia ya *Mke mwenza.* Aligundua kuwa wahusika matajiri huharibu watoto hasa vijana kupitia kwa utajiri wao. Mfano mzuri alioweza kututolea ni ule wa Boke mkewe Chahe ambaye alishiriki mapenzi na kijana mdogo aliyejulikana kama Sigawa. Baada ya kushiriki mapenzi naye, alikuwa akimlipa akitumia pesa za mumewe. Utafiti wa King'ala unatofautiana na utafiti huu kwa vile usawiri wa wahusika watoto haukujitokeza vizuri. Majukumu yanayotekelezwa na watoto hayakuangaziwa. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza uwakilishi wa watoto, majukumu yao na mielekeo ya wahusika matajiri kwa watoto.

King`ei (1996) alihakiki riwaya ya *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani.* Aligundua kwamba wazazi wana jukumu kubwa katika malezi ya watoto wao. Vilevile, aligundua kuwa mzozo kati ya wazazi na watoto wao ungeweza kusababisha maafa. Alipendekeza kuwa, ni vizuri kuwe na makubaliano kati ya watoto na wazazi wao kuhusiana na masuala ya maisha. Kwa maoni yake inadhihirika wazi kuwa wazazi ndio chanzo cha watoto kuwa na tabia mbaya. Utafiti wa King`ei unakaribiana na utafiti huu kwa sababu alitafiti riwaya sawa na utafiti huu. Tofauti ni kwamba King`ei alishughulikia riwaya ya Somba ilhali utafiti huu ulishughulikia riwaya nne za watunzi wawili tofauti. Vilevile, suala la majukumu ya wahusika watoto hakuligusia, ilhali katika utafiti huu majukumu ya wahusika watoto katika riwaya husika yaliangaziwa.

Rai sawa na hizi, zilichunguzwa na King'ala (1986). Katika utafiti wake, alitambua kuwa watoto na vijana wamepotoka na kutamauka maishani. Mtafiti huyu alijishughulisha na tamthilia ilhali utafiti huu ulijishughulisha na riwaya. Vilevile, tofauti nyingine iliyoko ni

kwamba hakumulika suala la majukumu ya wahusika watoto katika fasihi kwa undani ilhali katika utafiti huu suala la majukumu ya watoto lilishughulikiwa.

Kamunde (1983) aliangalia wahusika wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Alitafiti riwaya tatu ambazo ni *Utengano, Dunia Mti Mkavu* na *Asali Chungu*. Aligundua kuwa, wanyonge hudhulumiwa kwa misingi ya kitabaka ambayo chanzo chake ni tofauti za kiuchumi. Utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kidogo kwa vile alijumlisha wahusika wote. Utafiti huu ulijishughulisha na wahusika watoto pekee. Hata hivyo, utafiti huu wa Kamunde (1983) ulifaa kwa vile umeonyesha baadhi ya wahusika watoto kama wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

Nganje (1993) aliihakiki tamthilia ya *Masaibu ya Ndugu Jero*. Aligundua ya kwamba watoto hunyanyaswa kimapenzi na watu wazima. Hili analiweka wazi wakati anaposema kuwa msichana anapong`ara humvutia Jero. Yeye anaona kama ni ishara ya wahusika watoto kunyanyaswa kimapenzi. Tofauti na utafiti huu ni kwamba mhakiki huyu hajaelezea majukumu ya wahusika watoto katika tamthilia hiyo. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu amegusia suala la unyanyasaji wa wahusika watoto, jambo ambalo lilishughulikiwa katika utafiti huu.

Ikambili (1997) alishughulikia tamthilia ya *Visiki*, na alitambua kwamba watoto walikuwa na matumaini katika maisha yao ya baadaye. Maisha yao yaliegemea kwenye elimu. Alisema kuwa maisha yao ya baadaye yangekuwa mazuri iwapo wangetilia maanani suala la elimu. Mtafiti huyu hakuonyesha wazi uwakilishi wa watoto maanake hakusema kinachosababisha hali yao katika tamthilia hiyo. Pengine angepiga hatua mbele na kudokeza visababishi vya hali ya hao watoto kama vile wazazi wao, mazingira yao, au uchumi wa nchi. Tofauti na utafiti huu ni kuwa, yeye alihakiki tamthilia lakini utafiti huu ulishughulikia riwaya. Vilevile waandishi ni tofauti. Kazi hizi zinawiana na utafiti huu kwa vile zote zinajihusisha na wahusika watoto.

Tamthilia ya *Visiki* vilevile ilitafitiwa na Syambo (1997) aliyemwangazia mhusika mtoto Amina. Aligundua kuwa Amina ni jasiri. Hata hivyo, hajatuonyesha alichozingatia katika kutoa uamuzi wake. Tofauti iliyoko na utafiti huu ni kuwa alitumia nadharia ya uhakiki mtindo, ilhali katika utafiti huu nadharia ya uhalisia ilitumika. Alihakiki tamthilia ambayo

mwandishi wake ni Ongeti ilhali utafiti huu ulishughulikia riwaya ambazo waandishi ni Mohamed na Kezilahabi.

Mlacha (1985) alichunguza wahusika katika riwaya za Kiswahili Tanzania (1970 -1982). Aligundua ya kwamba wahusika hupewa lugha inayowasaidia kuelezea mambo anayokusudia msanii. Anasema kuwa mhusika anatumia lugha inayoambatanishwa na picha za mawazo zinazojengwa ili kuathiri wasomaji. Tofauti na utafiti huu ni kwamba utafiti wa Mlacha ulishughulikia wahusika kwa jumla. Hakuwatafiti wahusika watoto kando na wengine. Hili ni jambo lililoshughulikiwa na utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile ulihusu wahusika.

Bowen (2003) alichunguza usawiri wa wahusika watoto katika tamthilia zilizopendekezwa katika shule za upili: *Visiki* na *Amezidi*. Aligundua kuwa wahusika watoto wamesawiriwa kwa namna mbalimbali. Hii ni kwa sababu waandishi wote wawili walizaliwa na kukulia katika mazingira tofauti, kwa hivyo walichora watoto wakiwa katika mazingira tofauti. Mohamed amezaliwa Unguja ilhali Ongeti amezaliwa nchini Kenya. Vilevile, aligundua kwamba watoto walikuwa na sifa tofauti na kwamba walikuwa tumaini kwa jamii. Aliibua masuala kuwa watoto wamejitokeza kama wahusika ambao wana upendo, ukarimu, bidii na busara. Aligundua kuwa wanapuuzwa, wanadhulumiwa na wanadunishwa na watu wazima. Aidha, watoto wanakumbana na matatizo ya kunyimwa chakula na kufanyizwa kazi nyingi. Mwisho, aligundua kuwa waandishi wote wawili wametumia wahusika wachache. Utafiti wa Bowen (2003) ni tofauti na utafiti huu kwa sababu utafiti wakeuliongozwa na nadharia ya uhakiki-mtindo wa mtazamo wa Ngara (1982). Kulingana naye, uhakiki-mtindo unaangalia fasihi kwa mtazamo wa kiisimu na una misingi yake katika Umtindo. Aidha uhakiki-mtindo unazingatia karibu vipengele vyote vya fani ingawa unasisitiza sana kipengele cha mtindo.

Bowen (2003) akimnukuu Ngara (1982) anasema kuwa wahusika wanapaswa kuchorwa katika hali ya uhalisia. Anaendelea kusema kwamba ule uhalisia kulingana na Ngara ni uhalisia ambao unaonyesha maendeleo ya kibinadamu na unamkuza binadamu awe ni mtoto, mwanamke au mwanaume. Kwa upande mwingine, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia wa mtazamo wa Georg Lukacs ambao unasisitiza uwasilishi wa maisha katika jamii kwa uaminifu na usahihi. Vilevile, utafiti wa Bowen ulijihusisha na kazi zilizoandikwa baada ya miaka ya 1980 ilhali utafiti huu ulijihusisha na kazi zilizoandikwa miaka ya 1970. Utafiti

wa Bowen (2003) ulikuwa na umuhimu mkubwa sana katika utafiti huu kwa vile uliweka wazi vipengele muhimu vilivyoongoza katika kuchanganua uwakilishi wa watoto.

**2.2 Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia/Uyakinifu. Nadharia hii ilizuka karne ya kumi na tisa hususani kwa lengo la kupinga nadharia ya ulimbwende. Iliasisiwa na kumbo la tabaka la maendeleo wakiwemo waandishi wa Kifaransa kama vile Flaubert, Stendhal na Balzac. George Eliot alieneza nadharia ya uhalisia kule Uingereza naye William Dean Howells akaieneza Marekani. Baadaye kulizuka wataalamu wengine walioiendeleza nadharia hii kama vile; Maxim Gorky, Thomas Mann, Romain Rolland, Hegel na Georg Lukacs. Baadaye kulizuka aina tofautitofauti za uhalisia kama vile, uhalisia wa kibepari, uhalisia wa kijamaa na uhalisia hakiki. Kila moja ya aina hizi za uhalisia ilijishughulisha na majukumu yake. Kwa mfano, Uhalisia wa Kijamaa katika miaka ya 1930 kule Marekani ulijihusisha na michoro iliyosawiri ukosefu wa usawa katika rangi na kijamii. Aidha, kuzorota kwa uchumi kuliwachocheawafanyikazi kushughulika zaidi.Wasanii wengi waliotumia nadharia hii walikuwa wachoraji waliokuwa na maoni ya kisiasa ya kijamaa ambayo ni tofauti na ya Kimaksi. Utafiti huu ulifuata mtazamo wa Georg Lukacs. Kiini cha kuibuka kwa nadharia ya uhalisia ilikuwa ni binadamu kuwa na zinduko ya kwamba matatizo ya binadamu husababishwa na binadamu mwingine. Hivyo basi, msingi wa sababu ya nadharia hii ni kutambua mambo mawili. Kwanza, ni uhusiano wa mtu na jamii yake. Pili, ni nguvu za jamii, kisiasa na utamaduni kwa binadamu na mazingira yake.

Lukacs aliegemea kwenye uhalisia uliowekewa msingi na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel (1998) katika kitabu chake kinachojulikana kama ujumi. Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi namazingira yake. Inakinzana na nadharia ya Aristotle kuhusu jinsi fasihi hufafanuliwa. Kulingana naye, fasihi inaakisi yaliyokuwepo, yaliyomo au yanayoweza kuwepo.

Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanaoandika kwenye msingi huu wanatarajiwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi

anayehusika. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii katika upande wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi.  Mwandishi anapaswa kuyaakisi maisha ya kijamii, kitamaduni na kisiasa. Georg Lukacs ambaye amekuwa na athari kubwa katika mtazamo huu, anauona uhalisia kama lengo kuu la msanii au mwandishi. Mhakiki huyu anaamini kuwa mwandishi anasukumwa au anapaswa kuwa na nia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu wake katika wakati fulani maalum (wakati anaoandika). Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kuidhihirisha mifanyiko ya mabadiliko iliyoko. Lukacs anaiona kazi ya msanii kama kuuelewa ulimwengu kama changamano na wenye ukamilifu fulani unaobadilika na wenye sheria au kanuni maalum. Lukacs anatilia maanani swala la uhusiano uliopo kati ya lugha na sura ya matendo.

Nadharia ya uhalisia imejikita katika nguzo zifuatazo:

1. Fasihi inapaswa ieleze ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii. Mtunzi anapaswa aandike anavyoona maisha wala sio vile anataka yawe.
2. Sanaa lazima iwe aminifu katika kuonyesha hali halisi. Mtunzi asitie chumvi.
3. Sanaa ichukuliwe kama kioo cha kumulikia maisha halisi ya binadamu katika mazingira yake.
4. Mtunzi anapaswa afanye utafiti juu ya yale anayotaka kuandika ili aweze kuandika ukweli unaokubalika kifasihi.
5. Mtunzi anapoandika azingatie mambo madogo madogo ambayo yanasaidia kujenga wazo kubwa.
6. Wahusika lazima wasawiriwe kama walivyo katika jamii. Kwa mfano, wahusika wasisawiriwe wakiwa matajiri sana au wanyonge sana. Hii ni kwa sababu kuna kupanda na kushuka katika maisha.
7. Mtunzi atumie mandhari asili na ayaendeleze katika hali ya ukawaida wake.
8. Uhalisi lazima ushughulikiwe na ubunifu wa mwandishi na kazi yake inayoupa muundo maalum.

Kwa ujumla uhalisia ulilenga hali ya juu ya ukweli wa maisha ya binadamu katika fasihi. Nadharia hii ya uhalisia inatumika kama mwongozo wa kumulikia matatizo katika jamii. Ukusanyaji na uchanganuzi wa deta uliongozwa na nguzo tano za nadharia hii. Hizi ni: mtunzi kuelezea ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii, sanaa kuchukuliwa kama kioo cha kumulikia maisha katika jamii, kutumia mandhari asili, usawiri wa wahusika na ubunifu. Nguzo ya kuelezea ukweli wa maisha ya binadamu katika jamii ilitumika kuangazia mambo

yanayofanyika katika jamii na wala sio vile yeye angetaka yafanyike. Nguzo ya sanaa kuchukuliwa kama kioo cha kumulikia maisha halisi ya binadamu katika mazingira yake ilitumika kudadisi kama wahusika wanaona na kuelewa yanayofanyika katika jamii yao. Nguzo ya mtunzi kutumia mandhari asili na kuyaendeleza katika hali ya ukawaida wake, ilisaidia kutathmini kama mandhari yaliyotumiwa na mtunzi yanalingana na maelezo na majukumu ya wahusika katika riwaya husika. Kuhusu nguzo ya mtunzi kuwasawiri wahusika walivyo katika jamii, mtafiti alichunguza kama wahusika wamepewa sifa za binadamu wa kawaida kutokana na vile mtunzi alikuwa amewachora. Vilevile, uhusiano wa wahusika ulijulikana. Nguzo ya tano ni kwamba uhalisi lazima ushughulikiwe na ubunifu wa mwandishi na kazi yake inayoupa muundo maalum. Nguzo hii ilitumika kuangazia masuala ya kazi za mtunzi, kama kulikuwa njia ya kipekee ya kuifanya kazi yake kuonekana tofauti na kazi za watunzi wengine.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameonyesha njia za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji wa deta, vifaa vya utafiti, uteuzi wa sampuli ya utafiti na jinsi deta ilivyochanganuliwa. Njia zilizotumiwa katika utafiti ni upekuzi wa kimaktaba na utumizi wa mtandao. Vifaa vya utafiti katika uchunguzi huu ni riwaya nne za kisasa za Kiswahili. Katika uteuzi wa sampuli, riwaya nne ziliteuliwa.

### 3.2 Njia za Utafiti

Utafiti huu ulitumia njia ya upekuzi wa kimaktaba ambapo mtafiti alisoma riwaya husika, tasnifu mbalimbali, majarida na vitabu mbalimbali vinavyohusiana na mada ya utafiti huu. Tahakiki mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti huu zilisomwa na mtafiti. Utafiti huu ulifanywa katikamaktaba ya vyuo vikuu vya Egerton, Kenyatta, na Nairobi. Sababu ya kuteuliwa kwa vyuo hivi kama mahali pa utafiti ni kwamba vyuo hivi vilikuwa rahisi kufikika mtafiti alipozingatia gharama. Aidha, deta ya kutosha iliyohitajika ilipatikana katika vyuo hivi. Mbali na tasnifu, vitabu na majarida, mtafiti vilevile alitumia mtandao ili kuangaza vipengele mbalimbali vya uwakilishi wa watoto vilivyojitokeza kama vile kudhulumiwa kimapenzi, kupokonywa urithi, kubaguliwa kielimu, kupewa chakula kidogo, kufukuzwa nyumbani na wazazi wao, utundu na utukutu wao.

### 3.3 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulitumia riwaya za kisasa za Kiswahili ambazo zilikuwa ni chanzo cha deta iliyonuiwa kukusanywa. Riwaya hizi ni; *Kichwa Maji, Rosa Mistika, Nyota ya Rehema* na *Kiu*. Tasnifu mbalimbali zenye madazinazokaribiana na mada ya utafiti huu zilitumiwa. Aidha, majarida mbalimbali yanayohusiana na haki za watoto zilizochanganuliwa katika riwaya hizi yalitumiwa. Mtafiti alitumia uthamano ili kueleza haki mbalimbali wanazonyimwa watoto katika riwaya husika.

### 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulijihusisha na riwaya nne teule za kisasa za Kiswahili ambazo ni *Nyota ya Rehema, Kiu, Kichwa Maji* na *Rosa Mistika.* Riwaya hizi nne ziliteuliwa kimakusudi kutokana na riwaya nyingi zilizoandikwa na waandishi hawa. Hii ni kwa sababu kati ya

mwongo wa 70 na 80, fasihi iliweza kukua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na miongo ya awali. Riwaya hizi za kisasa za Kiswahili zinaonyesha migongano baina ya vijana na watu wazima. Aidha, riwaya hizi ziliandikwa wakati haki za kibinadamu zilikuwa zimeanza kutambuliwa. Mlacha (1984) aligundua kwamba dhamira ya riwaya zilizoandikwa wakati huu ilikuwa ni ujenzi wa jamii mpya na yenye usawa. Wamitila (2002) alikuwa na maoni sawa na haya aliposema kuwa ni vigumu kutenganisha usasa na usasaleo. Kulingana naye, usasaleo una mwelekeo wa kuyahusisha maisha, utamaduni, sanaa na itikadi katika kuangaza hali ya binadamu.

### 3.5 Ukusanyaji wa Deta

Katika ukusanyaji wa deta, utafiti huu ulijikita katika upekuzi wa kimaktaba. Riwaya nne teule zilipekuliwa na mtafiti. Uwakilishi wa wahusika watoto katika riwaya husika ulichunguzwa. Hapa mtafiti aliangazia haki za kimsingi za kifasihi na uhuru ambao watoto wamenyimwa katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Vilevile, matatizo mbalimbali yanayowakumba watoto yalichunguzwa. Akitilia maanani madhumuni ya kwanza ya utafiti huu, mtafiti alizingatia vipengee vifuatavyo :

- Kutolishwa vizuri na wazazi wao.
- Kutopewa uhuru wa kutoka na kutangamana na marafiki zao.
- Kufukuzwa nyumbani na wazazi wao.
- Kunyimwa uhuru wa kujieleza.
- Kutosomeshwa na wazazi wao.
- Kudhulumiwa kimapenzi.
- Kupokonywa urithi.
- Kubaguliwa kielimu.
- Kuchapwa bila sababu.

Kazi zinazohusiana na nadharia za fasihi zilisomwa na mtafiti ili kusaidia kufanya uamuzi katika utafiti huu. Nadharia hii ilikuwa ni nadharia ya Uhalisia. Tahakiki na tafiti za awali zinazohusiana na mada ya utafiti huu pia zilisomwa.

Baadaye mtafiti alichunguza majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya husika. King'ala (1986), anasema:

> Watoto wengi hufanywa kuwa watumwa na kuwa wao hupagazwa na masharti mengi ya wazazi wao.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalimwongoza mtafiti kuzingatia baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya zilizochunguzwa.Wahusika watoto wamehusishwa na:

- Ukahaba.
- Kulima.
- Kuteka maji.
- Kupika na kuuza pombe.
- Kuwalea wadogo wao.
- Wizi.
- Kusoma.

Mwisho, mtafiti alichunguza mielekeo ya wahusika matajiri na watu wazima kuwahusu watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Mielekeo hii ilichunguzwa kwa kuangalia lugha wanayoitumia wahusika hawa. Hili lilitimizwa kwa kuangalia:

- Sentensi zilivyojitokeza katika riwaya husika.
- Maneno au msamiati ulivyotumika katika riwaya zilizochunguzwa.
- Vilevile, vifungu vya maneno vilichunguzwa.

Mtafiti alitumia majedwali kukusanya deta na kuelezea uwakilishi wa watoto katika riwaya husika. Alishughulikia mhusika mmoja mmoja katika riwaya zote. Mtafiti alitambua mielekeo ya wahusika matajiri na watu wazima kwa watoto, kutokana na lugha wanayoitumia kisha akaielezea.

### 3.6 Uchanganuzi wa Deta

Uchanganuzi wa kithamano ulizingatiwa wakati wa kuchanganua deta iliyokusanywa kutokana na upekuzi wa riwaya husika. Mtafiti alipanga matokeo ya utafiti huu katika viwango mbalimbali akizingatia maswali ya utafiti. Uwakilishi wa watoto uliainishwa kwa kuzipanga haki za watoto katika vielelezo vinavyoonyesha aina mbalimbali za haki za watoto. Maelezo pia yalitolewa ili kuweka wazi matokeo kuhusiana na mambo yote yaliyochunguzwa katika utafiti huu. Utafiti huu pia ulitumia majedwali kuonyesha muhtasari wa haki wanazonyimwa watoto na matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo. Mtafiti alizingatia uchanganuzi wa kithamano ambapo mtafiti alitoa maelezo kuhusu yaliyomo

kwenye riwaya lengwa. Utafiti huu hasa ulichanganua lugha inayotumiwa na wahusika, uhusiano wa watoto na watu wazima hasa matajiri, dhuluma wanazokumbana nazo na majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

## SURA YA NNE
## UWASILISHI NA UCHANGANUZI WA DETA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii imechanganua vipengele muhimu vilivyotumika kuwasilisha uwakilishi wa wahusika watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili ambazo ni; *Kichwa Maji*, *Rosa Mistika*, *Nyota ya Rehema* na *Kiu*. Mtafiti ameonyesha aina mbalimbali za matatizo yanayowasibu wahusika watoto katika jamii. Matatizo haya ni pamoja na: kufukuzwa nyumbani, kunyimwa uhuru wa kujieleza, kutosomeshwa na wazazi wao, kupokonywa urithi, kuchapwa bila sababu, kudhulumiwa kimapenzi, kutopewa uhuru wa kutangamana na marafiki zao, kubaguliwa kielimu na kutukanwa. Majukumu yanayotekelezwa na watoto yameonyeshwa, na mwishowe mielekeo ya watu wazima na matajiri kwa watoto imeonyeshwa. Matatizo, majukumu na mielekeo ya watu wazima na matajiri iliyojitokeza katika vipengele vilivyoshughulikiwa imeainishwa na kujadiliwa huku mifano ikitolewa kutokana na matini iliyochanganuliwa kwa nia ya kuthibitisha matokeo ya utafiti na kutathmini maudhui yake yaani:

i. Kuchunguza uwakilishi wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.
ii. Kubainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.
iii. Kutambua mielekeo ya wahusika matajiri na watu wazima kwa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

### 4.2 MatatizoYanayowasibu Wahusika Watoto

Usawirikwa mujibu wa utafiti huu ni jinsi wahusika watoto katika riwaya husika wamechorwa ili kusimamia watoto katika fasihi. Watoto katika riwaya za kisasa wamesawiriwa kwa njia mbalimbali. Mtafiti amewasilishana kuchanganua matatizo wanayokumbana nayo maishani, na mwishowe ametumia majedwali kuonyesha muhtasari wa matokeo ya utafiti huu.

#### 4.2.1 Kufukuzwa Nyumbani

Katika riwaya ya *Kichwa Maji,* mintarafu ya madhumuni ya kwanza, wizi unamfanya Kalia afukuzwe nyumbani na babake. Wazazi hawakujua kuwa kufukuza watoto wao kutoka nyumbani sio suluhisho. Badala ya kumzungumzia, amweleze athari za kuiba, alimfukuza kutoka kwake. Haya yanadhihirika kutokana na matamshi anayoyatoa babake Kalia anapomwambia kuwa hangetaka kumwona Kalia tena katika nyumba yake. Hili analitilia

mkazo zaidi anaposema kuwa hata akifa, Kalia asiende kulia mbele ya kaburi lake. Maneno haya yanaonyesha ghadhabu aliyokuwa nayo babake Kalia.

Watoto wana haki ya kulindwa na wazazi wao. Babake Kalia anapomfukuza nyumbani, hamwambii anakostahili kwenda, hajui atakula nini huko aendako, na hajali mambo mengi mabaya yanayoweza kumdhuru mwanawe. Mzazi huyu anakwepa majukumu yake kama mzazi kwa sababu yeye ndiye alistahili kumfunza mwanawe kuwa wizi ni mbaya. Anapomfukuza kutoka kwake anataka aende akawaibie watu wengine, jambo ambalo linaweza kumtia hatarini. Utafiti huu uligundua kuwa wazazi wengi katika riwaya ya *Kichwa Maji*wanashindwa kurekebisha tabia za watoto wao na wanamalizia kuwafukuza nyumbani. Hatua aliyoichukua babake Kalia inawakilisha wazazi wengi na huenda ndio maana katika nchi za Kiafrika kuna watoto wengi wanaorandaranda mitaani bila sababu. Aidha, mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika*, ukahaba wake ulipozidi, babake alighadhabika sana. Rosa alifikia kiwango cha kumtukana babake mzazi. Rosa aliteta kuwa kila wakati babake aliwachunga. Alimuuliza babake kama angeweza kuwaoa yeye. Babake Rosa hakufurahishwa na swali lile la bintiye kwa sababu alisimama pale kwa muda bila kusema neno. Mwishowe Zakaria anamkana Rosa anapomwambia kuwa tangu siku hiyo Rosa, hangekuwa mtoto wake.

Kwa mintarafuhii, Zakaria alighadhabishwa na matendo ya Rosa na hakuweza kuvumilia zaidi. Rosa hakukosa jibu. Alimwambia kuwa tangu siku hiyo, Zakaria hangekuwa baba yake. Rosa hakupoteza muda wake kwa sababualiingiamaramoja ndani ya motokaa na kwenda zake "Beach". Siku hiyo Rosa hakurudi nyumbani kwa sababu alihofia maisha yake kwani alikuwa amemuudhi babake. Zakaria aliwachunga binti zake kwa sababu ya kukosa imani nao. Hakuamini kuwa watoto wake wangekaa salama bila yeye kuwachunga. Zakaria anamnyima Rosa fursa ya kuwa mwanawe anapomwambia kuwa hangeendelea kuwa mtoto wake. Kutokana na maneno anayoyatamka Zakaria mwenyewe, anamchochea bintiye ambayepia anamjibu bila nidhamu. Watoto wakati mwingi hupenda kuwaiga wazazi wao. Rosa hakuona kama ni jambo la ajabu alipomkana babake baada ya babake kumfanyia hivyo. Mzazi kumkana mtoto wake hadharani kunaweza kuwa na athari kubwa maanake mtoto atakosa kujua kama huyo ni mzazi wake halisi au wa kambo. Utafiti huu uligundua kuwa hasira imewafanya wazazi katika riwaya zilizochunguzwa kufikia kiwango cha kuwakana watoto wao.Mtunzi anataka wazazi waelewe kuwa kuwafukuza watoto nyumbani sio suluhisho wakati watoto wanapofanya kinyume na matakwa yao. Isitoshe, mhusika Rehema

katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* anafukuzwa nyumbani ingawa si kwa njia ya moja kwa moja bali kutokana na yale anayotendewa. Baada ya kifo cha mama yake, Bwana Fuad na bibi Adila, wanamtesa Rehema na kumkabidhi mikononi mwa watumishi ambapo cheo chake kilikuwa ni mtumishi wa watumishi. Anafanya kazi ngumu hadi ufagio unamharibu mikono. Baba yake alimwona mara moja moja. Bibi Adila ambaye ni mamake Rehema wa kambo pia walionana mara moja moja akiamrisha Rehema kutekeleza majukumu kadhaa. Rehema vilevile, alilala pahali pabaya. Udhalimu huuulimfanya aanze kufikiria kutoroka. Rehema aliamua kujitokomeza kwenye msitu wa nyika ambapo alikuwa tayari kwa chochote ambacho kingeweza kutokea yaanimaisha au mauti.

Rehema alikasirishwa na tusi moja akaamua kutoroka kwao. Mpishi mmoja alimwita ‘kizanda’ na kutokana na tusi hili, Rehema hakuweza kuvumilia zaidi. Licha ya kwamba Rehema alikuwa ni mtoto wa tajiri, aliishi akisononeka moyoni. Babake ndiye alikuwa chanzo cha matatizo yake. Baba yake alianza kumchukia pindi tu alipozaliwa. Rangi nyeusi ya ngozi yake ndiyo iliyomletea shida zote alizokumbana nazo. Rehema alinyimwa haki zake kama mtoto na baba yake kwa sababu alikosa mapenzi yake na alilala pahali pabaya. Sawa na Rehema, watoto wengi hukosa mapenzi ya wazazi wao halisi kutokana na sura zao. Utafiti huu uliibua suala kuwa baadhi ya kina baba hukoma kuwajibikia watoto wao pindi tu mzazi mmoja anapokufa hasa mama. Hili mara nyingi hufanyika ikiwa baba ya wale watoto ataoa mke mwingine.

Kutokana na yale anayoyapitia, Rehema anakumbuka mateso ambayo mama yake aliweza kuyapitia alipokuwa hai. Rehema hakuusahau urithi wa mateso alioachiwa na marehemu mama yake. Rehema alishangaa ni kwa nini mama yake alivumilia yote aliyokuwa akiyapitia. Aidha, alishangaa ni kwa nini aliganda kwa Fuad ilhali hakuwa akitakiwa. Alishangaa ni kwa nini mamake hakuondoka aweze kutafuta riziki zake. Rehema hakuona kilichomfanya mamake mzazi ahiari kunyanyaswa, kutengwana kuhamishwa eti kwa sababu alikuwaakipenda. Kwake yeye aliyalinganisha mapenzi yaliyokuwa kati ya wazazi wake na misumari ya nyuki. Uhusiano kati ya wazazi huathiri maisha ya watoto wao baadaye maishani. Rehema hata alipokuwa mkubwa ilikuwa vigumu kwake kuwaamini wanaume wengi. Kutoweka kwa Rehema kutoka kwao kulikuwa dhihirisho kuwa, wazazi hawakuwajali watoto wao. Hii ni kwa sababu mtunzi hajatufunulia kama babake na mamake wa kambo waljishughulisha kumtafuta alipotoweka nyumbani.

### 4.2.2 Kunyimwa Uhuru wa Kujieleza

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, watoto hawana usemi. Tunamwona Kidawa akimwambia Rehema jinsi alivyoozwa akiwa mdogo. Hii inaonyesha kuwa hakupewa uhuru wa kujieleza mwenyewe maanake baadaye ndoa yake haikudumu. Anasema hivi;

> … n'kapewa mume hata chuchu ya ziwa sijaota-dume lenyewe zumbukuku, halina liwezalo isipokuwa kucheza bao na kupiganisha majogoo. Nikaona e-e-e, heri inshalla, kinipacho nini Kidawa? Dunia wasaa. N'kaidai talaka yangu mpaka n'kaipata….huyo- o-o, mjini mpaka leo(uk. 42)

Katika kifungu hiki cha maneno, Kidawa anakiri kwamba hakuwa ameota hata chuchu ya ziwa alipokuwa akiozwa na wazazi wake. Hii ina maana kuwa alikuwa mtoto mdogo sana ambaye hakuwa ametoshea kuitwa mke wa mtu. Wazazi wake walimnyima haki ya kufurahia malezi yao akiwa mdogo. Mtoto wa umri kama wa Kidawa alipokuwa akiozwa, inamaanisha kuwa hakuwa amemaliza shule, kwa hivyo, ni kusema kwamba Kidawa alinyimwa fursa ya kwenda shule. Kipengele hiki kinathibitisha madhumuni ya kwanza ya utafiti huu kwamba wahusika watoto wamewakilishwa wakisibwa na matatizo kadhaa. Wazazi wa Kidawa walikuwa wanajaribu kukwepa majukumu yao, yaani ya kumlea na kumpeleka shuleni hadi akomae na atoshee kuolewa. Utafiti huu uligundua kwamba, wazazi walitamani sana kuwaoza binti zao.

Watoto waliajiriwa na kulipwa pesa kidogo. Kwa sababu ya Rehema kutegemea jasho lake, anakubali kulipwa malipo duni baada ya kazi ngumu. Rehema aliajiriwa kazi kwa shilingi hamsini kila mwezi. Haikuwa kazi rahisi kuyakamilisha masharti ya Rozi, lakini upungufu aliokuwa nao Rehema, ulimfunga. Alikuwa na uhakika kwamba hakuwa na mtu wa kumtegemea isipokuwa nafsi yake mwenyewe. Rehema ananyimwa uhuru wa kujieleza wakati Rozi anapotaka kujua ni kwa nini mtoto hulia usiku. Anamwambia Rehema kwamba;

> Sitaki uzushi, mimi mwenyewe siku zote nampanga, simsikii kulia. Siyo mtoto kalala na wewe ulale, mimi ninapokuwa kazini kwangu silali wala sisinzii. Chukua chai umpelekee bwana, kisha uchanyate viguo vya mtoto; asubuhi nisikute nguo chafu. (Uk 61)

Kutokana na kifungu hiki cha maneno, Rozi anaposema ya kwamba hakuwa akitaka uzushi, anamaanisha kuwa hangependa kubishana na mtu duni kama Rehema. Kwake yeye, Rehema alikuwa ni wa kiwango cha chini mno alipokuwa akijilinganisha naye. Rehema angekuwa na uhuru wa kujieleza pengine Rozi angemsikiliza hata kwa sekunde moja. Si kawaida kwa

binadamu yeyote yule kukosa kulala kwa ajili ya kujipumzisha, lakini Rozi anamwambia Rehema asilale wakati mtoto anapolala. Kando na kumwangalia mtoto, anamwachia Rehema kazi zingine. Rozi hakutaka kusikia eti Rehema alikuwa akipata fursa ya kupumzika. Sawa na Rozi, siku hizi waajiri wengi huwadhulumu wajakazi wao kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, kuna wale wanawalipa malipo duni, wengine huwachapa na hata kuwanyima chakula licha ya kuwa hao ndio huweza kukitayarisha chakula kile. Mtunzi anataka kuwapasha wasomaji habari kuwa waajiri wakati mwingine huwanyima vijakazi wao uhuru wa kujieleza kama alivyofanya Rozi.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rosa akiwa katika darasa la tano anaandikiwa barua na Charles. Kwa bahati mbaya, dadake kwa jina Stella anamwambia baba yao kuhusu hiyo barua. Baba yao anaghadhabishwa na habari hiyo na bila kumpa Rosa fursa ya kujieleza, anaanza kumchapa. Zakaria anakasirika na kumwita Rosa mara moja. Rosa anakuja hali shuka ikiteremka chini. Kabla hajasema lolote anapigwa na kuanguka chini shuka inamtegatega na kumwangusha chini. Kuanguka chini kwa Rosa kunamrahisishia babake kazi kwa sabaabu anamshika kwa urahisi. Uchunguzi huu uligundua kuwa Zakaria hakuchukua muda kujua ile barua ilikuwa na ujumbe gani kabla hajaanza kumwadhibu mwanawe. Hii ni kwa sababu alianza kumchapa kabla ya Rosa kusema lolote kana kwamba alikuwa akijua yaliyokuwemo kwenye ile barua. Aidha, utafiti huu uligundua kuwa Zakaria alimnyima Rosa uhuru wa kujieleza. Kitendo hiki cha Zakaria kilimtia woga Rosa na kilimfanya baadaye akawa mnafiki. Mtunzi alikusudia kuwajuza wasomaji kuwa, hata kama wazazi wana nguvu kuliko watoto wao, yafaa wawe na uhuru katika mazungumzo yao.

### 4.2.3 Kutosomeshwa na Wazazi wao

Elimu ni muhimu sana maishani. Inaweza ikafananishwa na uti wa mgongo kwa binadamu. Elimu huwasaidia watu kufanya mambo mengi kama vile kutatua masuala magumu maishani. Aidha, watu walioelimika huweza kujikimu kimaisha.Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, wazazi hawakutilia maanani suala la masomo ya baadhi ya watoto wao. TunamwonaKaliaalivyokuwa mtovu wa nidhamu akiwa bado mdogo. Kama angepelekwa shule hangepata muda wa kuzurura bila sababu na kufanya maovu yote aliyoyafanya.Kalia hakuenda mbali katika masomo yake kwa sababu alimaliza darasa la sabatu. Aliposhindwa alianza kujishughulisha nyumbani na kazi ndogo ndogo.

Kwa mintarafu hii, tunaona ya kwamba Kalia alinyimwa haki ya kupata elimu na wazazi wake. Hii ni kwa sababu aliwachashule akiwa darasa la saba. Umri wake ulikuwa mdogo na hakuwa amekomaa kimwili na kiakili. Hata kama alijishughulisha na ushonaji wa viatu na unyoaji, haikuwa vizuri kwani hakuwa na tajiriba yoyote wala fedha za kuanzisha biashara kama hiyo. Wazazi wengi kwa kutojua athari za kutowasomesha watoto wao, hata hivi leo huwaangalia watoto wao bila kusema lolote wanapoacha kwenda shule wakisema kuwa wamekosa pesa za kuwalipia. Wazazi waliwawachia majukumu watoto wakubwa kuwalipia karo za shule wadogo zao. Kwa mfano, Rukia anapoenda darasa la tisa, analipiwa karo na Kazimoto, nduguye. Ndio maana anapopachikwa mimba anahuzunika sana na Kazimoto ndiye wa kwanza kuandikiwa barua ya kumjuza kuhusu mimba hiyo.

Watoto wana haki ya kusomeshwa na wazazi wao. Utafiti huu uligundua kwamba baadhi ya wazazi walikwepa majukumuyao na kuwatwisha watoto wao mzigo wa kuwalipia wenzao karo. Shule aliyopelekwa Rukia ilichangia kupachikwa kwake mimba. Hii ni kwa sababu alipokosa mahali pa kuishi, kaka yake, Kazimoto, aliamua Rukia aishi kwa Manase bila kujua kuwa alimwachia fisi kumchunga mbuzi. Vilevile, katika riwaya ya *Rosa Mistika*, watoto wanaachishwa shule siku moja ili wamsaidie Rosa kulima eka moja ya shamba. Utafiti huu uligundua kuwa wazazi hawakutilia maanani suala la masomo. Huu ni udhaifu wa wazazi kwa sababu watoto wana haki ya kuhudhuria shule kila siku.Hata kama watoto wenyewe waling’ang’ana kwenda shule, mzazi kama vile Zakaria alikuwa na mielekeo hasi kuhusu elimu. Alikwepa majukumu yake kama baba mzazi.Hii ni kwa sababu tunamwona mamake Rosa akienda kumwombea Rosa pesa za matumizi wakatiRosa alipotaka kurudi shuleni. Zakaria alimpatia shilingi ishirini tu. Ni wajibu wa baba yeyote mzazi kujua mahitaji ya mtoto wake wakati anapoenda shule, lakini Zakaria anajifanya kana kwamba hakujua kuwa Rosa alistahili kurudi shule hadi aambiwe na mkewe. Wazazi wengi katika nchi za Afrika Mashariki hupendelea watoto wao wasomee shule za mabweni. Hii huwafanya kuonana na watoto wao mwisho wa muhula au wanapopewa likizo fupi katikati ya muhula. Kuna wazazi kama Zakaria ambao hukosa kuwapa watoto wao pesa za kutosha za matumizi. Mtunzi alitaka wazazi wawajibike kwa majukumu yao ya kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata mahitaji yao ya kimsingi hata wanapokuwa kwenye shule za mabweni.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, baada ya mama ya Rehema kufariki, Rehema anateswa sana na mama yake wa kambo, Bibi Adila. Rehema hakupewa fursa ya kwenda shule hata siku moja. Badala yake, baba yake na Adila walimkabidhi mikononi mwa watumishi nacheo

chake kikawa ni mtumishi wa watumishi hadi ufagio ukamfanya suguru mikononi. Rehema alikuwa na wakati mgumu na watumishi wengine kwa sababu kutwa yake ilipita kwa uvumilivu wa misonko na mikemeo ya hawa watumishi.

Kutokana na kutosomeshwa, Rehema anakuwa na mawazo mabaya. Pengine angekuwa anajishughulisha na masomo, hangefikiria kutoroka kwao. Rehemaaliota juu ya maisha mema yaliyoko nje ya gereza lile na kutafakari juu ya njia za kutoroka. Hakujua pa kwenda lakinialiamua kujitokomeza msitu wa nyika, kutafuta chochote kile angekipata. Babake Rehema alimnyima haki ya kusoma kama watoto wengine. Hii ni kwa sababu licha ya baba yake kuwa na pesa nyingi, alikataa kumpeleka shule kwa kufuata msimamo wa mama yake wa kambo.

Kutosomeshwa kunamfanya Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* kuamua kuajiriwa akiwa mtoto. Mwajiri wake kwa jina Rozi, anamwajiri tu kwa vile hana namna. Hili linadhihirika wazi Rozi anaposema kuwa angetaka mtu mzima anayejua kulea na wala si mtoto mdogo aliyekuwa akihitaji malezi. Hii inaonyesha wazi kuwa Rehema hakupelekwa shule na wazazi wake. Rehema ananyanyaswa kwa vile amenyimwa haki yake ya kusomeshwa na wazazi wake. Hii inapelekea Rehema kupata malipo duni, kwanza kwa sababu yeye ni mtoto, na pili kwa sababu hakuenda shule yoyote. Rehema aliajiriwa kazi kwa shilingi hamsini kila mwezi. Haikuwa rahisi kukamilisha masharti ya Rozi, lakini shida alizokuwa nazo zilimfunga na kumlazimisha asalimu amri. Hii ni kwa sababu alifahamu kuwa ilimbidi ajitegemee yeye mwenyewe.

Katika riwaya ya *Kiu*, mhusika Bahati hakusomeshwa kwa sababu babake mzazi hakutilia maanani suala la masomo. Babake Bahati alitoweka na ikawa ni chanzo cha matatizo na umaskini. Kupotea kwa baba yake huenda ndiko kulipelekea Bahati kuanguka mtihani.
Babake Bahati alipotoweka alimwachia mamake mzigo wa kumlea mtoto wao peke yake. Tukitilia maanani kuwa mama ya Bahati hakuwa na kazi nzuri ya kujipatia riziki, ilikuwa vigumu kwake kumsomesha Bahati. Bahati alinyimwa haki za kimsingi kwa sababu kando na kutosomeshwa, hakulala pahali pazuri. Bahati hakusomeshwa kwa sababu ya ufukara wa wazazi wake. Huenda ikawa babake Bahati aliamua kutoroka alipoona maisha yamekuwa magumu. Kupitia kwa lugha fasaha, mwandishi aliazimia kutoa onyo kwa akina baba kuwa ni sharti washirikiane na wake zao katika malezi ya watoto wao. Alikuwa akitaka kukashifu

vitendo vya wazazi wa kiume ambao hukwepa majukumu yao kama wazazi yaani kazi yao ni kuzaa tu kisha wao hutoroka na kuwaachiaakina mama majukumu yote.

### 4.2.4 Kupokonywa Urithi

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, tunaona Zakaria, Regina na Rosa wanakufa kwa wakati mmoja. Watoto wa marehemu Zakaria waliteswa na jamaa zao. Baada ya mazishi ya hawa watatu, jamaa wengine za marehemu walibaki ili kugawana urithi. Watu walijua kiasi cha pesa ambacho Zakaria alikuwa amewacha benkini kuwa zilikuwa shilingi mia saba nazo zilikuwa zimewekwa kwa jina la Emmanuel. Jamaa hawa walimlazimisha Flora aende kuzitoa zile pesa benkini ili waje wazigawane. Flora alipokwenda benki hakuweza kuzipata. Jambo hili liliwafanya jamaa zake wawe na hamaki.Walimtukana wakitumia maneno kama vile; mwizi, malaya na mshenzi. Tunaambiwa kwamba;

> Hawa jamaa walirithi … Jamaa waligawana vitu. Walirithi kila kitu kilichokuwa ndani ya nyumba.Walirithi michungwa na miembe. Walirithi migomba yote. Walirithi paka na mbwa. Walirithi majani yaliyokuwa juu ya paa, na miti yoteiliyofanya nyumba isimame.Walirithi kuku; walirithi hata mbolea ya ngo’mbe… Lakini hapakuwa hata na mtu mmoja aliyeweza kusema atamchukua mtoto mmoja amtunze … (uk 96).

Ni dhahiri shahiri kuwa jamaa hawa hawakuona haja ya kuwacha chochote nyuma kwa sababu waliona kwamba ulikuwa mji wa wanawake. Utafiti huu uligundua kuwa watoto wa Zakaria walipokonywa urithi kwa sababu ya jinsia yao ya kike. Marehemu Zakaria alikuwa na mtoto mmoja wa kiume yaani Emmanuel, lakini alikuwa mdogo sana na hivyo basi hangeweza kutetea urithi wake.Ujumbe anaopitisha mwandishi huyu hapa ni kwamba watoto wanastahili kurithi mali ya wazazi wao bila kuzingatia jinsia yao. Vilevile, mtunzi alitaka watu waone umuhimu wa kuacha mila na itikadi zilizopitwa na wakati. Jamaa za Marehemu Zakaria walifanya kosa kubwa kuwapokonya urithi watoto wake.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* mamake Rehema anapokufa, Bi Kiza-shogake mamake alimtunza Rehema na kumwonyesha huruma. Anamhimiza aende akadai haki zake. Anamwambia kuwa hawezi kuiona haki yake ikienda Mwambao akiitazama kwa macho tu.Alimhakikishia kuwa Ramwe ilikuwa yake na hivyo ndivyo alikusudia marehemu mamake Rehema. Kutokana na maoni ya Bi Kiza, tunaona kuwa licha ya mamake Rehema kufa, kuna wale waliokuwa wakimtakia Rehema mazuri. Bi Kiza anamfunulia Rehema kuwa mama yake marehemu alikuwa ameacha shamba na lilikuwa ni jukumu la Rehema kwenda kudai urithi

huo. Hii ni ishara ya urafiki mzuri kwa sababu hata baada ya mamake Rehema kufa, bado Bi Kiza anadumisha uhusiano mwema kati ya aila hizo mbili. Rehema alidai haki yake na kuonyeshwa na babake Bwana Fuad. Mwandishi amedhihirisha kuwa watu wote hawawezi kuwa maadui zamtu, angalau kuna mmoja anayeweza kuwa na nia nzuri kama vile Bi Kiza alivyokuwa mkarimu kwa Rehema na kwa marehemu mamake. Hii ni njia moja ya kuwapa watu moyo kuwa wanapokataliwa na wengine, kunao wachache wanaowajali. Hakika Bi Kiza alifanya jambo la busara yaani kumwambia Rehema kuhusu urithi wake.

Kwa bahati mbaya, babake Rehema anakuwa mgonjwa na anaaga dunia. Baada ya kifo cha baba yake, ndugu yake wa kambo-Samir anataka kumpokonya urithi wake.Ilikuwa siku moja Rehema alipowasikia Samir na kikundi cha watu alichokuja nacho wakinong'onezana kuhusu ramani. Baada ya kukagua lile shamba, kile kikundi kilirudi. Rehema hakuwaona ila tu alisika wakiongea kwa ulimi mwepesi. Kuna mambo matatu tu aliyoweza kuyasikia kutoka vinywani mwao ambayo ni:  Ramani, mipaka, na urithi. Kuhusiana na Maneno haya matatu, mhusika Rehema alielewa janga lililomkabili. Rehema alijua kwamba kile kikundi cha watu kilikuja kukagua shamba lake na hivyo, angeweza kupokonywa lile shamba wakati wowote. Hili lilitimia wakati Rehema alipokwenda kortini kumshtaki ndugu yake wa kambo na wenzake. Mkuu wa wilaya alishirikiana nao kumpokonya urithi wake. Hili linajitokeza wazi anaposema hivi;

> ….Nadhani huielewi adhabu anayoweza kupewa mtu pindi ikithibiti korti kuwa amefanya majaribio ya kutaka kumiliki mali isiyokuwa yake chini ya kuhifadhi mali ya mtu binafsi namba 49, kifungu cha 5 c…..(uk 146).

Unukuzi huu unadhihirisha wazi kuwa hawa watu walipanga njama ya kumsumbua Rehema ili aogope na kuwawachia shamba lake. Walijaribu kumwoyesha athari za kumiliki shamba lisilokuwa lake. Huu wote ulikuwa ni ujanja waliokuwa wanataka kutumia kumpokonya urithi wake. Utafiti huu uligundua kuwa watu wenye uwezo hasa wa kifedha hushirikiana na wanasheria kama wakuu wa sheria na mawakili kuwanyanyasa wananchi wasiokuwa na pesa au hata masomo. Mkuu wa wilaya alikiuka maadili ya kazi na cheo chake kwa kushirikiana na wahalifu kumpokonya Rehema urithi wake. Habari muhimu anayotaka wasomaji waelewe ni kwamba, kuna ufisadi mwingi unaoendelezwa na wafanyikazi wa vyeo vya juu katika afisi zao.

Tukio hili lilimfanya Rehema akumbuke vile mamake alivyotendewa wakati alikuwa mgonjwa. Alikumbuka jinsi alivyotumiwa kupeleka mkono wa mamake ukabanwa madhubuti, dole lake la gumba likachovywa katika chepe chepe baridi, likaangushwa juu ya kitu kigumu hatimaye mkono wake ukaachiliwa. Hapa ndipo aligundua kuwa rangi ya zambarau iliyopakwa kwenye kidole gumba cha mama yake, ilikuwa ni sahihi ya talaka waliyokuja kuiba kutoka kwa mama yake. Kumbukumbu hizi zilimfanya Rehema atamauke sana. Mwandishi ametumia hali hii ya Rehema kumkumbusha kuwa hakuwa mwanaharamu bali mtoto halali wa Bwana Fuad na Bibi Aziza.

Baadaye tunamwona Karim mumewe Salma dadake Rehema wa kambo akitaka kumpokonya Rehema shamba lake anapomuuliza hivi;

> … unawajua wale watu waliokuwa wakikaa katika shamba lako la Ramwe walighili katika shamba lile kwa miaka chungu-nzima halafu wakanunua shamba jingine huko upande wa pakani?... (uk 164).

Huenda ikawa ni ukweli kwamba damu ni nzito kuliko maji kama isemavyo methali ya Kiswahili. Salma, dadake Rehema wa kambo anamkumbuka Rehema kwa mbali. Katika fahamu yake tunaona kuwa alimkumbuka mtu aitwaye Rehema. Alimfikiria alivyoteseka baadaye, alisema kuwa ukosefu hakika ni mateso makubwa, kwamba maskini yule Rehema nyota yake haikuwa na mtu tangu alipozaliwa. Hata kama Salma hakukubaliana na mumewe, Karim hakufa moyo kwani siku moja alifika Pakani jioni kwa ajili ya kukagua mipaka. Rehema aliyapitia mateso tangu utoto wake hadi alipokuwa mkubwa. Kilichomsumbua Rehema sana ni ujinga wa kutojua. Ujinga huu ulitokana na ukosefu wa elimu aliokuwa nao Rehema. Angekuwa amesoma angeweza kudai haki yake. Vilevile, ufisadi uliweza kutawala katika jamii hii. Waliokuwa na pesa ndio walisikizwa wakilinganishwa na wale maskini. Tunaweza kusema kuwa chanzo cha mateso yake yote ni babake aliyeamua kuoa mke wa pili –Bibi Adila baada ya kuona rangi nyeusi ya Rehema pindi tu alipozaliwa. Siku hizi pia watu hupokonywaurithi kwa kutojua haki zao. Aidha, watu huzaa watoto na kuwakana kuwa si wao. Hata hivyo, kwa sababu hali ya teknolojia imeimarika sana watoto na kina baba zao wanaweza kufanyiwa uchunguzi wa kisayansi na kujulikana mzazi halisi wa mtoto fulani. Ijapokuwa uchunguzi huu ni ghali mno, angalau umesaidia matatizo ya akina baba wengi ambao huwakana wanao. Pengine Rehema angefanyiwa uchunguzi kama huu, huenda ikawa hangepitia yale yote aliyoyapitia.

Katika riwaya ya *Kiu*, Idi alimtumia vibaya Bahati. Alipopata pesa kutoka kwa mzee Mwinyi, kupitia kwa Bahati, aliamua kumpa talaka na alimchukua msichana mwingine kwa jina Rehema. Bahati anapata mashauri kutoka kwa watu kuhusu kupokonywa urithi wake na Idi. Anaambiwa hivi:

> …..Anayekutenda mtende bibi….au umesahau kama ni haki yako? Aichukue mipesa yote akahonge yule hawara wake, wewe mwenye pesa zile akuone mjinga, mbaya na matusi juu, talaka juu! Kwa nini? Na ulimpa pesa zile kukaa nazo kwa jina lake? Unaona sasa wewe kakutupilia mbali, unakaa pahala kama hapa, nayeye huyo anastarehe na Rehema wake ….mdai haki yako! Ukimtisha hivyo atashtuka, na japo hutazipata zote utapata nusu yake zikufae (uk. 153)

Bahati alikuwa na penzi la dhati kwa Idi lakini Idi hakuwa akimpenda hata kidogo. Idi alimtumia Bahati kama kitegauchumi. Idi anapomkataa, Bahati hakutaka kwenda kortini kumshtaki. Hii ni ishara ya mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo kwa Idi. Bahati alipoanza mapenzi na Idi alikuwa msichana mdogo ambaye hakuelewa mapenzi ni nini na wala hakuwa na ujuzi wowote kuhusu mapenzi. Baadaye anakuwa gwiji wa mapenzi ambayo yanamfanya kupokonywa urithi wake na Idi

### 4.2.5 Kuchapwa Bila Sababu

Mhusika Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji* anaamua kuwa mtovu wa nidhamu. Tunaona kuwa alianza kuwaingilia wanawake na wasichana.  Alibandikwa jina 'Nunda Mla Watu". Alifanya hivi kwa kuwashurutisha wamtimizie haja yake bila kupiga kelele. Wakati mwingi alifanya hivi nyakati za usiku na alikuwa akitembea na kisu mkononi. Vitendo vyake vilimpelekea kuchapwa na wanakijiji ambao hawakufurahia aliyokuwa akifanya. Sikumoja alijaribu kumshika mwanamke mmoja kwa nguvu lakini mwanamke huyu alimshika Kalia sehemu za siri, jambo ambalo lilimfanya alie sana kwa maumivu. Aliomba msamaha lakini mwanamke hakumwacha mpaka wakati majirani walipokuja. Walimkuta Kalia amelia hadi macho yakawa mekundu, kwa sababu maumivu yalikuwa yamemzidia.

Kalia kwa kujiingiza katika mambo ya wanawake, ilimbidi aibe pesa za kuwapatia. Alipogunduliwa kuwa ni mwizi, alichapwa sana na babake. Hili linadhihirika wazi wakati Kazimoto anaposema kuwa alimsikia babake akimwambia Kalia avue nguo kisha alale chini. Aidha, alisikia akisema kuwa Kalia alikuwa amebakisha viboko vitano. Kutokana na aliyoyasikia Kazimoto, ni wazi kuwa babake Kalia alikuwa na hasirailiyomfanya

amlazimishe Kalia kuvua nguo kabla yeye (babake) hajaanza kumchapa Kalia. Kazimoto alishuhudia yote yaliyotendeka kwa muda mfupi. Alisikia fimbo ikilia wakati baba yao alikuwa akimchapa Kalia. Vilevile, alimwona Kalia akiinama chini na akitiririkwa na machozi. Hii ni dhuluma kwa mhusika mtoto Kalia kwa sababu hakuwa ameambiwa tangu mwanzo kuwa akiokota pesa alistahili kumwambia babake. Kama mzazi mzuri, angemwita amketishe na kumwelezea athari za kuchukua pesa zozote anapoziona ndani ya nyumba yao. Babake Kalia alimchapa akiwa na hasira, jambo ambalo lingeweza kumsababishia Kalia majeraha mabaya. Kuchapwa kwake Kalia hakukumsaidia kwa njia yoyote ile. Kalia alizidi kupotokwa na nidhamu. Mwandishi wa riwaya hii ametumia mbinu za kifasihi kuwajuza wazazi kuwa, si kiboko tu kinachoweza kutumiwa ili kurekebisha tabia. Aidha, alitaka kuwakumbusha wazazi kuwa samaki hukunjwa angali mbichi, yaani watoto wanastahili kuanza kufunzwa tabia nzuri wakiwa wachanga kwa umri.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, tunamwona Zakaria, babake Rosa, akimchapa bintiye Rosa eti kwa sababu aligundua kuwa Rosa alikuwa ameandikiwa barua na Charles. Zakaria aliudhika na kumwita Rosa mara moja na kabla hajasema lolote alipigwa na kuanguka chini. Alijaribu kuamka na kukimbia lakini shuka ilimtegatega na kumwangusha chini tena:

> Makofi yalikwenda mfululizo hata damu kumtoka puani na midomoni …kunyang'anywa shuka…Zakaria hakujali alichukua fimbo na kuongozana na bintiye mpaka chumba cha watoto hali akinguruma… (uk.6-7).

Kutokana na unukuzi huu, ni wazi kuwa Rosa hakutaka babake aione ile barua kwa hivyo, alijaribu kuitafuna lakini babake alimkaba kookwa sababu Rosa hakuitema. Zakaria aliendelea kumkaba Rosa koo hadi macho ya Rosa yakaanza kuwa mekundu. Barua ilianguka chini pindi tu ulimi ulipomtoka. Barua yenyewe haingeshikika kwa sababu mate yaliifanya itelezekama kuku aliyetapikiwa na chatu. Zakaria aliiokota mara moja. Hapa tunaona kuwa babake Rosa alimnyima haki yake ya kulala usiku huo kwani alimsababishia majeraha mwilini. Watoto hawastahili kuchapwa bila sababu. Ilikuwa mara ya kwanza kwa Rosa kuandikiwa barua na mvulana, kwa hivyo, kama mzazi angemzungumzia na kumwambia kuwa si vizuri kuanza uhusiano na wavulana akiwa angali mdogo. Mwandishi alikusudia kuwaarifu wasomaji kuwa si kila kosa linalofanywa na watoto linastahili adhabu ya kiboko. Utafiti huu uligundua kuwa adhabu ya kiboko isipotekelezwa kwa uangalifu inaweza kuathiri maisha ya baadaye ya mtoto. Zakaria alifanya vibaya kuona uchi wa bintiye. Pamoja na hayo, kumchapa kiasi cha kumtoa damu puani na midomoni haikuonyesha hekima yoyote.

Mwandishi vilevile, alitaka wazazi waone umuhimu wa kuchunguza chanzo cha kosa lolote kabla ya kuwachukulia hatua watoto wao.

Kwa kutoelewa athari  za kujiingiza katika suala la mapenzi na wanaume, Rosa  anapojiunga na Chuo cha Ualimu, anakuwa na uhusiano  wa kimapenzi na mwalimu mkuu, kwa bahati mbaya  au nzuri, mke wa mwalimu mkuu anawakuta wakishiriki mapenzi, na Rosa anachapwa sana. Rosa alijaribu kukimbia lakini alishikwa na yule mwanamke. Tunaelezwa hivi;

> Rosa aliangushwa chini. Yule mwanamke alimwinamia. Rosa alitiwa jino. Pale pale uso wa Rosa ulienea damu. Yule mwanamke alionekana kutema kitu fulani chini. Rosa alilia. Mwalimu alimtoa mke wake juu ya Rosa. Rosa alikimbia, kabla hajawahi kutoka nje redio ilimpata mgongoni. Ilianguka chini na kupasuka. (Uk.54).

Kuhusiana na kitendo hiki, ni dhahiri shahiri kuwa Rosa aliumizwa na mke wa mwalimu mkuu. Hii ni kwa sababu alipojiangalia ndani ya kioo hakuweza kuamini kwamba hiyo ilikuwa kweli sura yake. Alipaza sauti na kulia kwa sababualikuwa ameng'olewa sikio lote la nje na mke wa mwalimu mkuu. Alikaa muda mrefu akihisi maumivu makali lakini hatimaye aliweza kupona. Rosa alibaki na sikio moja, jambo ambalo lilimfanya afunge kitambaa kichwani kila siku. Hakika mkewe mwalimu mkuu alikosea sana kumchapa Rosa hasa ikizingatiwa kwamba Rosa alikuwa na umri mdogo sana akilinganishwa na mwalimu mkuu. Kama mkewe mwalimu mkuu angekuwa shujaa kamili, basi angekabiliana na mumewe na wala sio Rosa. Hapa mtunzi aliazimia kuwapasha habari wasomaji kuwa katika jamii, wanyonge ndio huumia. Vilevile, alitaka kuonyesha jinsi walimu wanavyotumia vibaya mamlaka yao wakiwa na wanafunzi wao.

Zakaria alikuwa mwepesi sana wa kuchapa watoto. Hata watoto wa watu wengine aliwachapa tu bila sababu. Tunaona Zakaria akiwachapa vijana wawili wanapokuja kwake. Walipomwambia kuwa walihitaji mayai ya kununua, Zakaria aliingia ndani ya nyumba na kutoka nje na mayai matatu mkononi. Vijana waliamua kuchunguza kama mayai yale yalikuwa mazuri. Walianza kuyapima yale mayai kwa kuelekeza juani hali jicho moja wamefumba. Zakaria aliwachapa wale vijana pasi na matarajio yao maanake walishtukia viboko vikilia juu ya miili yao. Zakaria aliwauliza kama walikuwa wakifikiria yeye alikuwa mjinga. Aliwafukuza na kuwaambia waondoke pale. Kwa mintarafu ya kitendo hiki, ni wazi kuwa Zakaria alikuwa na tabia ya kuchapa watoto bila. Zakaria alipoteza heshima zake kwa

sababu tunaona vijana aliowachapa wakimtukana. Wanamwita mshenzi, na kumwambia kuwa ataoza na binti zake. Zakaria hakuweza kujidhibiti kwa sababu anapotukanwa na vijana wawili aliowachapa, anaelekeza hasira zake kwa mkewe Regina na kuanza kumtusi kwa kumwita mshenzi na kumlaumu kwa kumzalia wasichana tu. Zakaria anadai kuwa mkewe anamletea taabu nyumbani kwake. Maneno ya Zakaria kwa wale wavulana wawili kuwa walifikiri kwamba alikuwa mjinga, yanaonyesha kuwa Zakariaalifikiria wale vijana walikuja nyumbani kwake kuwatafuta binti zake. Huenda ikawa ndio maana aliamua kuwachapa bila mazungumzo yoyote. Suala la kuwa na binti wengi linamsumbua sana. Kwa mfano, wale vijana wawili wanapomtukana naye anamtukana mkewe kwa kumzalia wasichana wengi. Zakaria anawadhulumu watoto wake hata kisaikolojia kwa sababu anapomlaumu mkewe kwa kumzalia wasichana, binti yake Rosa anasikiliza. Hili ni jambo ambalo lingefanya binti zake Zakaria kujidharau wakifikiri kuwa wasichana si watu wa maana maishani. Mtunzi alikuwa na nia ya kuwajuza wasomaji kuwa wazazi wawapende watoto wao sawa, yaani wasiwapendelee watotokwa kuegemea jinsia yao.

### 4.2.6 Kudhulumiwa Kimapenzi

Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, mhusika Rukia anadhulumiwa kimapenzi na Manase. Haya yanajitokeza dhahiri shahiri wakati Rukia aliposema kuwa hajui Manase ni mtu wa namna gani.Hapo ndipo Kazimoto alipoanza kuhisi kiini cha shida ya Rukia. Kazimoto aligundua kwamba Manase alikuwa akijaribu kufanya mambo yasiyotakikana. Baadaye Rukia alimwandikia Kazimoto barua na kumweleza jinsi alivyodhulumiwa kimapenzi na Manase. Anasema hivi;

> …..kaka ….nilikaa kwa raha muda wa juma moja tu. Baada ya juma hiloniliona Manase anaanza kunitazama kwa njia ya ajabu. Baada ya majuma mawili nilipokuwa naoga siku moja niliona jicho lake kwenye tundu la vifunguo…..…Alifika hata hatua ya kutumia nguvu! Na kweli alitumia nguvu bila utashi wangu (uk.25- 26).

Rukia anaposema kuwa aliona Manase akimtazama kwa njia ya ajabu, anamaanisha kuwa Manase alianza kumtamani. Manase alimnyanyasa Rukia kimapenzi kwa sababu msichanahakuridhia. Alimshika kwa nguvu bila hiari yake. Huenda ikawa Manase aliamua kufanya hivi kwa sababu Rukia hangeweza kujinasua kutoka kwake. Pengine aliona familia ya kina Rukia haingeweza kumfanyia chochote. Walikuwa maskini maanake hawangeweza kumtafutia nyumba ya kuishi peke yake au hata kumpeleka shule nzuri. Mtunzi ametumia lugha kifasaha kupitisha ujumbe kuwa watoto wengi hudhulumiwa kimapenzi wanapoachwa

na watu ambao huaminika nawazazi wao. Watu hawa mara nyingi huwa wana uhusiano wa kifamilia na hivyo, huwa ni tatizo kwa sababu watoto hawafungui roho zao na kuwaelezea wazazi au wanaowatunzatatizo hili. Mhusika Rukia ni mfano mzuri katika riwaya hii ya *Kichwa Maji*. Pana uwezekano kwamba Rukia asingepata mimba, jamaa yake hawangegundua kuwa alikuwa akidhulumiwa kimapenzi na Manase.Wakati mwingi tatizo kama hili hugunduliwa baadaye wakati tayari mambo yameshakwenda mrama kama ilivyokuwa kwa Rukia.

Mhusika Kalia anamnajisi msichana mdogo lakiniKazimoto anamwokoa msichana huyu.Tunamuona Kazimoto akishuhudia haya kwa sababu alikimbia mara moja kwenda kumwokoa huyo msichana.Alipofika mahali pale, Kazimoto alichanganyikiwa kwa sababu hakujua la kufanya. Alimkuta yule msichana mdogo akiwaamelala kifudifudi akilia. Kalia naye kwa upande mwingine alikuwa akivaa kaptula yake. Kazimoto anapomkaripia Kalia, Kalia anamkumbusha maovu ambayo yeye huyafanya na hajawahikusema lolote hata kwa baba yao. Kalia anamkashifu Kazimoto kwa kumchapa ilhali yeye hufanya uovu kama huo na hakuna anayemchapa.

Si watoto wa kike tu waliodhulumiwa kimapenzi, hata watoto wavulana hawakuepuka dhuluma hii. Mhusika Kalia alikuwa akidhulumiwa na mwanamke mzee aliyemzidi umri. Mwanamke huyu alimfanya Kalia kuiba pesa na kumpelekea. Kazimoto alipomfuata polepole kisiri kutoka nyuma, aligundua kuwa Kalia alikuwa akitumiwa vibaya na Tegemea. Hili linadhihirika wazi wakati Kazimoto alimsikia Kalia akizungumza chumbani mwa Tegemea. Vilevile, alisikia Kalia akiruka kitandani. Kwa kutaka kuhakikisha yaliyokuwa yakijiri chumbani mwa Tegemea, ilimbidi Kazimoto aendelee kujibanza ukutani na alimsikia Tegemea akisema kwamba;

> Angalia usivunje kitanda changu. Unafahamu, Kalia, kwa nini ninakupenda? Unanikumbusha siku zangu za zamani nilipokuwa nikitembea na vijana wadogo kama wewe. Mimi huwa ninafurahi kuona kijana mzuri akirukaruka juu ya kifua changu. Huwa kama ninanyonyesha mtoto mdogo……haraka gani Kalia, mimi nipo kwa ajili yako? (Uk.108).

Kutokana na nukuu hii, tunaona ya kwamba kuna dhuluma ya kimapenzi inayoendelezwa kati ya Tegemea na mtoto Kalia. Maneno "… zamani nilipokuwa nikitembea na vijana wadogo … ninanyonyesha mtoto mdogo…" yanadhihirisha ukweli huu, kwamba, Tegemea alikuwa mama mzee akilinganishwa na Kalia. Hapa ndipo Kazimoto alipogundua Kalia

alipokuwa akipeleka pesa alizokuwa akiiba. Alimsikia Kalia akimwambia Tegemea kwamba shilingi hamsini alizokuwa amemletea zilifanya apigwe sana na baba yake alipotambua. Hii ni dhuluma ya kimapenzi kwa sababu Tegemea anapoambiwa ukweli na Kalia anamkejeli na kumwita bwanake, na kwamba hayo ndiyo mapenzi halisi. Vilevile, alimwambia kuwa mapenzi ni kuvumiliana ili  kutunza heshima na siri za marafiki.

Kwake Tegemea ni biashara hata kama anajifanya kuwa anampenda Kalia. Tunamwona Tegemea akimkumbusha Kalia kuwa shilingi zake zilikuwa karibu kwisha. Kando na kudhulumiwa kimapenzi, inamlazimu Kalia atafute pesa za kulipia mapenzi, na njia tu yenye anaweza pata pesa kwa urahisi ni kuiba. Kwa hivyo, huenda ikawa Tegemea ndiye alichangia wizi wa Kalia. Mbali na kunyanyaswa kimapenzi na Tegemea, Kalia pia alimnyanyasa msichana mdogo na hapo ndipo alipatana na mauti yake. Kalia alipomnajisi msichana mmoja mdogo wa darasa la nne aliyekuwa akitoka shule jioni na kumbikiri, kijiji kizima kiligadhabika kupita kiasi. Huyu msichana aliharibiwa kabisa na Kalia. Kwa muda wa siku tatu hakuweza kutembea. Kalia alitafutwa kwa mikuki na wazazi wa binti huyu lakini hakuonekana.

Sawa na watoto wa kike, wavulana pia walidhulumiwa kimapenzi na kina mama wazee bila wazazi wao kugundua. Mfano mzuri ni mhusika Kalia aliyenyanyaswa kimapenzi na Tegemea mama mzee. Ujumbe anaoupitisha mtunzi huyu ni kwamba, si watoto wa kike tu ambao hudhulumiwa kimapenzi, wavulana vilevile hujikuta wamenaswa kwenye mtego huu. Mtunzi pia anataka kuwaambia wazazi kuwa ni jukumu lao kuwafunza watoto wao kuwa walinzi wa ndugu zao. Hii ni kwasababu kama Kazimoto angekuwa na ujasiri, angemwambia baba yao na pengine Kalia angeonywa na kuwachana na suala la kujiingiza katika mapenzi na mama mzee kama Tegemea.

Dhuluma nyingine inayojitokeza ingawaje si ya njia ya moja kwa moja ni ile ambayo watoto wakubwa walishiriki mapenzina marafiki zao huku wadogo zao wakifahamu. Kwa mfano, Kazimoto alizoea kwenda kwa Tegemea kumtafuta Vumilia wakiwa na mdogo wake Kalia. Tunaona kuwa Kazimoto anajutia sana Kalia anapouawa. Kazimoto anaona kama yeye ndiye chanzo cha ndugu yake Kalia kuuawa. Hii ni kwa sababu licha ya Kazimoto kuwa mkubwa kwa umri, alizoea kutembea na wasichana na kufanya mapenzi nao bila kumficha Kalia. Kazimoto anathibitisha ukweli huu anaposema kuwa;

> …mimi ninasema hivi kwa sababu nimemwona mdogo wangu akiuawa kwa sababu ya kufuata matendo yangu mabaya. Mimi mwenyewe nilikuwa nunda mla watu. Lakini nilikuwa bado sijafikiria kwamba ubaya wanguuliweza kuleta maafa kwa mwanadamu mwingine na kwa taifa zima, pia kwa wajukuu wetu. Matendo huigika kwa urahisi hasa matendo mabaya (uk. 144-145).

Kwa mintarafu hii, Kazimoto anakuja kujuta baada ya maziwa kumwagika. Anaposema kuwa yeye ndiye alikuwa nunda mla watu, anamaanisha kuwa yeye alikuwa akiwadhuru watulakini hakuweza kuuona uovu wake alipokuwa akishiriki. Maneno "kufuata matendo yangu mabaya" yanaashiria mienendo ya Kazimoto ya awali. Kazimoto alizoea kwenda na Kalia kuwatafuta wasichana. Hivyo basi, Kalia aliwafahamu wasichana wote waliokuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kazimoto. Hapa Kazimoto anakiri kwa kinywa chake kuwa yeye ndiye alimfunza mdogo wake Kalia mienendo mibaya na kuwa ndiye alisababisha kifo chake. Hili ndilo tatizo kubwa duniani kwamba mtu anapotenda uovu fulani haoni ubaya wake, lakini uovu ule ule unapotendwa na mtu mwingine, yeye huwa mstari wa mbele kumnyoshea kidole cha lawama. Mwandishi alikuwa na nia ya kuwajuza wasomaji kuwa watu wazima wanapofanya mambo hasa ya uhusiano wa kimapenzi, wajaribu sana kuyafanyia faraghani.

Vumilia aliyekuwa ametoroka kwao kwa muda mrefu, siku moja alikutana na wavulana wawili wahalifu na waliweza kumdhulumu kimapenzi. Tunaona kuwa anaokolewa na Moyokonde ambaye baadaye anamuoana kuwa mumewe. Tegemea na Kazimoto waliamua kwenda kumtafuta. Wawili hawa walipotaka kujua ni vipi Moyokonde alivyoamua kuishi na Vumilia bila kumjulisha Tegemea mama yake, Moyokonde anajaribu kuelezea walivyokutana na Vumilia na jinsi alivyomwokoa kutoka hatarini. Aliwaambia jinsi vijana wawili walivyotaka kumwangamiza Vumilia baada ya kumnajisi eti kwa sababu alikuwa amekwisha chukua pesa zao nyingi mno lakini hakujua kuwa mambo yangemwendea mrama kama yalivyofanyika. Kunyanyaswa kimapenzi kwa Vumilia kulisababishwa na umaskini, yaani alihitaji pesa sana. Mtoto wa nyoka ni nyoka kama vile Waswahili wasemavyo. Tegemea mamake Vumilia alikuwa kahaba wa hali ya juu. Hangemkubali mwanaume bila kuona pesa. Huenda mwanawe Vumilia alifuata tabia za mama yake, jambo ambalo nusura limgharimu maisha yake. Utafiti huu uligundua kuwa wazazi wengi waliwadhulumu watoto wao kimapenzi na kisaikolojia wanapowaleta wapenzi wao nyumbani na kulala nao huku watoto wao wakiwa huko. Mfano mzuri katika riwaya hii ya *Kichwa Maji* ni Tegemea aliyezoea kumleta mzee Kabenga chumbani mwake nyakatizausiku Vumilia bintiye akiwemo. Wakati mwingine hawa hawa wapenzi wa mama zao huwatumia vibaya na hili

husababisha mambo mengi kama vile uhasama kati ya mama na bintiye, au hata usambazaji wa magonjwa ya zinaa. Wazazi wanastahili kuwa mifano bora ya kuigwa na watoto wao.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, watoto wanawakilishwa wakidhulumiwa kimapenzi. Mhusika Rosa akiwa bado mwanafunzi wa Rosary, anaenda kujiburudisha na akiwa pale anakutanana Deogratias kwa mara ya kwanza. Deogratias anamtoa nje, anamkumbatia na kumbusu mara moja. Kutokana na busu alilopata kutoka kwa Deogratias, anashindwa kulala usiku ule hadi anaenda kwa Thereza msichana mwenzake na kumwomba usaidizi. Sauti ya Rosa ilikuwa ikitetemeka alipokuwa akiongea na Thereza ambaye alikuwa bado hajaelewa chochote kama anavyosema mwandishi kwamba;

> …Rosa alipomrukia na kumkumbatia. Waliangushana kitandani. Rosa alianza kumbusu, lakini tamaa yake haikuweza kupungua. Rosa alihitaji ule mkwaruzokwaruzo wa ndevu na manyoya ya tumboni. (uk.33)

Kutokana na unukuzi huu ni wazi kuwa Rosa alihitaji mwanamume.Mwandishi anaposema kuwa moto ulikuwa ukiwaka upande wa kusini lakini wao walikuwa wakizimisha upande wakaskazini, anamaanisha kuwa wote ni wa jinsia moja na wanajaribu kutekeleza kitendo ambacho hakikuwezekana kati yao wawili. Hapa Rosa anamdhulumu mwenzake Thereza kimapenzi. Ni dhuluma kwa sababu Thereza hakufahamu chanzo cha matendo ya Rosa. Dhuluma hii iliambukizwa kutoka kwa Deogratias kwenda kwa Rosa na hatimaye kwa Thereza. Utafiti huu uligundua kuwa suala la wazee kuwadhulumu wasichana kimapenzi lilikita mizizi katika jamii hii. Utafiti huu uligundua kuwa wazee wa jamii hii hawakuwa na aibu. Ni wazee wanaomezea mate matiti ya watoto wadogo, wanapoteza muda wao katika mambo ya anasa kama dansi badala ya kukaa nyumbani na kushughulikia aila zao. Aidha, utafiti huu uligundua kuwawazee walitumia pesa na vyeo vyao kuwadhulumu kimapenzi watoto. Walimu nao walilegea kwa kuangalia nidhamu ya wanafunzi wao. Kwa mfano, wakati wanafunzi wa shule ya Rosary walipoenda kuburudika, walimu walistahili kuwa macho kwa wasichana wa shule.Kama hili lingefanyika, pengine Deogratias hangepata fursa ya kuzungumza na Rosa. Watoto hawa walihitaji mwelekeo hivi kwamba, hata kama ni kuzungumza na wanaume, wasijiingize katika suala la uhusiano wa kimapenzi. Rosa anapomwambia Thereza amsaidie, anamaanisha Thereza akubali kufanya mapenzi naye jambo ambalo halingewezekana kwa sababu wote walikuwa wa jinsia moja. Mwandishi anaposema kuwa moto ulikuwa ukiwaka upande wa Kusini nao walikuwa wakizimisha upande wa Kaskazini, ina maana kuwa walihitaji wanaume kutimiza haja zao za kimwili na wala si watu wa jinsia ya kike kama wao.

Dhuluma ya aina hii iliwaathiri wazazi na watoto wavulana kiakili. Hii ni kwa sababu baadhi ya hawa wazee viongozi walikuwa wakitoa vitisho kwa wavulana. Vilevile, wanatumia vyeo vyao kuwanyanyasa wazazi wa kiumewanaokataa kuwaoza mabinti zao. Kwa mfano, Deogratias aliwahamisha wazee wawili kutoka Mwanza kwa sababu ya kupinga asiwachukue binti zao. Vijana wengi walitafutiwa sababu za kuwekwa jela ili wasilete ushindani katika suala la kung'ang'ania wasichana. Deogratias alipendasana dansi, hasa zile za watoto wa shule kwa sababu hii ndiyo ilikuwa mbinu yake ya kuwatafuta wasichana wadogo. Ni wazi kuwa watoto hapa wanadhulumiwa kimapenzi kwa sababu za kiuchumi - yaani wazazi wao hawana uwezo wa kuwazuia viongozi wenye pesa kuwanyanyasa watoto wao kimapenzi.

Rosa anapokuwa katika chuo cha ualimu, mwalimu mkuu anatumia cheo chake kumdhulumu kimapenzi. Anatumia uamuzi uliokuwa umetolewa na walimu wengine hapo awali. Mwalimu mkuu anamwambia Rosa kuwa walimu wengi wanamchukia nayeanajaribu kumwonyesha Rosa vile anamjali kuliko walimu wote waliokata shauri afukuzweshule eti kwa sababu aliavya mimba. Anamhakikishia kuwa yeye akiwa kama mwalimu mkuu wa shule, hatakubali Rosa afukuzwe. Rosa kusikia hivyo alimkumbatia mwalimu mkuu. Rosa alifumbwa kwa maneno machache tu na akakubali kushiriki mapenzi na mwalimu mkuu.Rosa aliona kama alipata ushindi. Hili lilidhihirika wazi wakati Rosa alipompangusa jasho mwalimu mkuu wa chuo.Katika muktadha huu, Rosa alikuwa kwa Thomas yaani mwalimu mkuu. Walikuwa wamekamilisha kitendo cha kushiriki mapenzi na ndiposa Rosa alikuwa akimpangusa mwalimu mkuu jasho. Ushindi unaozungumziwa hapa ni kwamba Rosa aliweza kulala na mwalimumkuu na hivyo akaamini kuwa hangefukuzwa shule. Hapa Mwalimu mkuu anatumia cheo chake na udhaifu wa Rosa kumnyanyasa kimapenzi. Kama mwalimu mkuu alistahili awe kielelezo kwa walimu wengine na wanafunzi lakini alifanya kinyume. Rosa alikubali kushiriki mapenzi na mwalimu ili asifukuzwe shule. Mtunzi anaazimia kuwajuza wasomaji kuwa wakati mwingine wanafunzi hukubali kunyanyaswa kimapenzi na walimu mradi tu wasifukuzwe shule au wazazi wao wasijuzwe kuhusu mienendo yao mibaya.

Kwa sababu ya kudhulumiwa kimapenzi, wasichana wa shule wanapata mimba kama anavyokiri Flora kuwa wasichana hawa baada ya kupachikwa mimba walifukuzwa kutokashuleni.Kuhusiana na habari hizi za Flora, ni bayana kuwa wasichana wa shule walikuwa wamepotokwa na nidhamu. Hii inamaanisha kuwa walishiriki mapenzi bila kujali madhara au matokeo yake. Hii ni kwa sababu tumeona ya kwamba walipata mimba wakiwa

bado shuleni.Wasichana walikuwa wakichukuliwa na wapishi wa Wahindi mjini. Walimu walijaribu kukaa macho, suala lililopelekea wasichana kumpenda mtu yeyote yule aliyepata bahati ya kuonana nao.Walichanganyikiwa hadi wakapoteza uwezo wao wa kuchagua. Kupata mimba kwa wasichana wa shule ni dhihirisho kuwa kulikuwa na uozo wa tabia katika shule nyingi. Kutokana na dhuluma hii ya kimapenzi, wasichana wengi wanalazimika kukatisha masomo yao kwa muda ili wawachunge watoto wao kwanza. Kwa wengine huwa ndio mwisho wa masomo yao kwa sababu ni sharti wawatafutie watoto wao mahitaji ya kimsingi.Katika shule ya kina Flora, wasichana walikuwa wakichukuliwa na watu kutoka nje. Huu ni udhaifu wa walimu wa shule ile. Pengine wangeweza kuzuia mimba walizozipata wasichana hawa kama wangeshtaki wale wapishi wa Mhindi waliokuwa wanawachukua wasichana wa shule. Kuwafukuza shuleni wasichana waliopata mimba haikukuwa suluhisho. Pengine serikali ingeanzisha kituo cha malezi ya watoto waliozaliwa na wasichana wa shule karibu na kila shule ya upili. Huenda ikawa wasichana wengine wangeogopa kupata mimba wakiwa wanafunzi.

Rosa alipomaliza chuo cha ualimu, alipata kazi. Rosa sasa alikuwa ameanza kujitunza vizuri lakini wanaume bado wanataka kumdhulumu kimapenzi. Wanaume walifika mara nyingi usiku na kubisha  mlango wake, lakini yeye hakuwa na hamu ya wanaume tena kwa hivyo, hakufungua hata siku moja. Baada ya muda vijana walianza kumchukia na kumtukana, kwa sababu aliweza kuwapuuza walipomwonyesha nia ya kumtaka. Rosa alikuwa amedhulumiwa kimapenzi sana. Huenda ikawa ndio maana aliamua kuwakataa wanaume waliomtaka lakini alikuwa amechelewa sana. Wasichana wengi hutumiwa vibaya na wanaume wakati wangali wadogo. Wanapokua, wao hugundua walivyokuwa wapumbavu lakini huwa hakuna wawezalo kufanya ili kurekebisha vitendo walivyovitenda awali.

Katika mazungumzo kati yaFlora na Charles, ni dhahiri kuwa watu wazima ndio huwadhulumu watoto kimapenzi. Haya yanajitokeza wazi kama ifuatavyo:

> … ninaona  kwamba watu wakubwa wakubwa ndio wapatiao wasichana mimba. Wala sio wanafunzi. Wanafunzi mara nyingi husingiziwa tu … wafanyakazi wakubwa, wengi wameoa … (Uk. 83)

Charles anaposema kuwa watu wakubwa ndio huwapatia wasichana mimba, anamaanisha wale watu wenye vyeo vikubwa serikalini yaani matajiri. Hii ni kwa sababuya uwezo walio nao wa kifedha. Hili ni jambo la kukashifiwa kwa sababu wafanyikazi hawa wakubwa wakubwa, watoto wao huwa hawachezewi na wanaume wengine. Anasema kuwa wanafunzi

husingiziwa tu kwa sababu wakati mwingi wasichana huwa na wanafunzi wavulana katika shughuli mbalimbali za kimasomo. Aidha, wavulana husingiziwa kuwa ndio huwapatia mimba wasichana kwa sababu hawana usemi wowote mbele ya wafanyikazi matajiri.Hapa mwandishi anataka wasomaji waelewe kuwa mimba nyingi za wasichana wa shule hutokana na watu wazima waliooa na wenye vyeo serikalini.

Charles anapotaka kumwoa Rosa, vijana wenzake wanamwambia jinsi Rosa alivyokuwa hawara. Charles anataka kujithibitishia kama Rosa alikuwa bikira. Anahakikisha Rosa amelewa chakari na anamdhulumu kimapenzi. Kabla Charles kufanya mapenzi na Rosa, dhamiri yake ilimsumbua sana kwa sababu Rosa alikuwa usingizini. Alijua bila shakakuwa Rosa alikuwa amelewa sana kiasi cha kutoweza kugundua kesho yake. Tunaambiwa kuwa;

> Sidhani kwamba yumo katika hali ya kuweza kunizuia. Nafikiri huu ndio wakati wa kuhakikisha … alivua suruali. Alipanda kitandani. Alipandisha gauni la Rosa juu mpaka kifuani … Charles alivumbua siri kubwa…(uk 85-86).

Unukuzi huu, ni dhihirisho kuwa Charles hakuwa na imani na Rosa kutokana na aliyokuwa ameyasikia kumhusu Rosa. Hii ilikuwa ni dhuluma kubwa kwa Rosa maanake Charles alimnywesha pombe kuzidi kiasi kabla hajamfanyia unyama huu. Hata kama Rosa alikuwa amezoea kufanya hivyo hapo awali, Charles hakumfanyia vizuri kwa sababu hawakukubaliana na Rosa. Siri iliyogunduliwa na Charles ni kwamba Rosa hakuwa bikira kama alivyokuwa akimdanganya. Utafiti huu ulivumbua kuwa Rosa alimdanganya Charles kwamba alikuwa bikira kwa sababu alitaka sana aolewe naye. Charles alifanya kosa kubwa kwa sababu, alipofanya mapenzi na Rosa bila Rosa kufahamu kutokana na ulevi wake, hata yeye hakuendelea kuwa bikira. Vilevile, utafiti huu uligundua kuwavijana wavulana walishiriki mapenzi na wasichana lakini walipotaka kuoa baadaye, walitafuta wasichana mabikira. Jambo hili halikuwezekana katika riwaya hii ya *Rosa Mistika* kwa sababu Charles anapotaka kumwoa Rosa, anagundua kuwa Rosa hakuwa bikira.Kutokana na kule kudhulumiwa kimapenzi, Rosa anafunuliwa ukweli na Charles kupitia kwa barua kuwa yeye hakuwa bikira na hili linasababisha kifo chake. Kabla ya kifo chake alimwandikia Charles kijibarua na kumwambia kuwa kuoa bikira ni bahati. Rosa hakujiua kwa kumpenda Charles bali kwa sababu alikuwa amedhulumiwa kimapenzi kwa muda mrefu na alipotaka kutulia, Charles anamkataa.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, tunamwona Kidawa akidhulumiwa kimapenzi anapoozwa bila hiari yake. Hili linadhihirika wazi anapomsimulia Rehema kuhusu maisha yake ya awali. Anasema kuwa;

> … kwa ubarazuli wangu n'kapewa mume hata chuchuya ziwa sijaota-dume lenyewe zumbukuku, hakuna liwezalo isipokuwa kucheza bao na kupiganisha majogoo. Nikaona e-e-e, heri inshalla, kinipacho nini Kidawa? Dunia wasaa n'kaidai talaka yangu mpaka nikaipata … (uk. 41-42).

Kidawa anaposema kuwa hata chuchu ya ziwa hakuwa ameota, anamaanisha kuwa hakuwa amekomaa kuitwa mke wa mtu. Alilazimishwa na wazazi wake kuolewa na mtu ambaye hakumpenda yeye. Mwanaume huyu alimdhulumu kimapenzi kwa vile Kidawa hakuchagua kuishi naye ila tu ni kwa masharti ya wazazi wake. Kidawa anamwambia Rehema kuwa mume aliyepewa alikuwa akipiganisha majogoo, maanake alipenda kuwaingilia wake za watu wengine.

Rehema alipoajiriwa, Mansuri alijaribu kumhadaa Rehema kwa kumnunulia nguo mpya ili aweze kumnyanyasa kimapenzi. Rehema alifanyiwa hayo bila kutarajia.Mansuri alitumianguvu kumbusu Rehema.Hii ilikuwa ni dhuluma kwa Rehema kwa sababu tunaona jinsi alivyosumbuka kimawazo na kuduwaa pale kwa muda. Mansuri aliendelea kumtaka Rehema. Siku moja alimchukua Rehema katika chumba chake cha kulala.Rehema alijaribu kujinasua lakini haikuwezekana kama yanavyodhihirisha mazungumzo yao:

> … ngojea kwanza bwana Mansuri … akishindwa kuuzuia mwili mzito uliokuwa ukimwelemea… Usijifanye mtoto Rehema … lakini nasaha hazikumwombea Rehemana nguvu za kujipapatua zilikuwa zikimwishia. (uk. 65)

Nukuu hii ni ushahidi kwamba tendo la Mansuri kutumia nguvu kwa Rehema lilimkera sana. Rehema aliamua kumuuma Mansuri na kukimbia kwa kasi hadi chumbani alimokuwa amelala mtoto. Aliamua kufunga mlango akaanza kulia.Alipomwambia angoje kwanza, Rehema alikuwa na nia ya kuhepa. Kwa upande mwingine, Mansuri alikuwana nguvu kumzidi Rehema. Rehema aliamua kumuuma kwa sababu aliona kuwa hii ndiyo njia angetumia kujikomboa kutoka mikononi mwa Mansuri. Kitendo hiki cha kumuuma Mansuri kinaonyesha wazi kuwa Rehema hakuwa tayari kushirikiana na Mansuri. Rehema hapa alidhulumiwa kimapenzi kwa sababu ya unyonge wake kimwili na kwa sababu ya umaskini uliokuwa umemlazimisha kuajiriwa pale ili aweze kupata riziki yake. Uchunguzi huu uligundua kuwa wafanyikazi wa nyumbani hasa wale wa kike hukumbana na dhuluma ya

kimapenzi kutoka kwa waajiriwao. Mfano mzuri ni mhusika Rehema na mwajiri wake Bwana Mansuri.

Rehema hakupenda kuacha kazi yake ya ulezi maanake hakuwa na lingine alilotegemea. Rozi alipokwenda kazini, Rehema aliwachunga vizuri Bwana Mansuri na mwanaye.Bila shaka kinolewacho hupata; usiku mmoja Rozi akiwa kazini, Rehema aliendа kulala na Mansuri chumbani mwa Rozi. Usingizi uliwazidi na asubuhi Rozi aliporejea kutoka kazini, aliwakuta mle kitandani mwake.Kwa ghadhabu, Rozi alitaka kumchapa Rehema lakini mumewe alimzuia. Rozi hakufikiria kama mtu mzima kwa sababu alifahamu vizuri kuwa Rehema alikuwa mdogo kwa umri, na badala ya kumgonga mumewe, alitaka kumgonga Rehema. Hapa Rehema anaonewa kwa sababu hangeweza kukabiliana na Rozi.

Rehema anapotaka kukomboa urithi wake, alienda kwa Idrisa msaidizi wa mkuu wa Idara ya Urithi na Nyaraka.Idrisaalijaribu kumdhulumu Rehema kimapenzi kutokana na vitendo na mazungumzo yake. Tunaambiwa hivi;

> … Rehema alirudi nyuma kuikimbia mikono ya Idrisa, "No, darling, hivyo sivyo wanavyokutana watu baada ya kupoteana miaka chungunzima … Idrisa alipiga hatua mbele ya Rehema akamshika kwa nguvu na hamu, na kuigandamiza midomo yake juu ya midomo ya Rehema … now darling, kaa juu ya kiti unieleze shida yako (uk. 136-137).

Kwa mintarafu hii, Rehema alirudi nyuma na kuikimbia mikono ya Idrisa kwa sababu hapa anaweza kutambua mema na mabaya. Hata kama Idrisa alikuwa mpenzi wake wa zamani, hayo yalikuwa ya kitambo na Rehema alitaka tu kusaidiwa kukomboa urithi wake. Idrisa anamdhulumu kimapenzi Rehema, kwa sababu alirudi nyuma kuonyesha hakuwa tayari lakini Idrisa alimshika kwa nguvu na kuigandamiza midomo yake juu ya midomo ya Rehema. Kumshika mtu sehemu za mwili bila idhini au kumbusu ni dhuluma ya kimapenzi na hivyo Idrisa alimdhulumu Rehema kimapenzi. Idrisa alitumia cheo chake kazini na nguvu zake kama mwanaume kumdhulumu mhusika Rehema.

Mhusika Bahati katika riwaya ya *Kiu* anadhulumiwa kimapenzi na Mzee Mwinyi. Analazimishwa na Idi kushiriki mapenzi na Mwinyi ili Idi aweze kupata pesa. Kwake yeye Bahati anatumika kama kitega uchumi. Bahati anamkumbusha Idi kuwa urafiki wao uliisha wakati alipomlazimisha kufanya mapenzi na mzee mchimvi. Bahati alikubali kufanya mapenzi na mzee Mwinyi kwa sababu hakutaka kumpoteza Idi. Hili linajitokeza wazi mtunzi

anaposema kwamba Bahati alikubali pasina hiari. Kumaanisha kwamba Bahati alishurutishwa. Mwinyi alikuwa na penzi la dhati kwa Bahati lakini Idi alimtumia vibaya Bahati. Idi anatawala mawazo ya Bahati kwa sababu yeye ndiye anamwambia hata maneno ya kumwambia Mwinyi. Bahati anapomwambia Mwinyi kwamba anampenda, Mwinyi anampatia Idi hundi ya shilingi elfu ishirini ili ampelekee Bahati. Bahati alikubali shingo upande kufanya mapenzi na Mwinyi. Hii ni kwa sababu roho yake ilichafuka kumaanisha Bahati hakumtaka Mzee Mwinyi hata kidogo. Mtunzi anakusudia kuwaarifu wasomaji kuhusu suala la watu kuwahadaa watoto kufanya mapenzi na watu wasiowajua. Bahati alidhulumiwa kimapenzi kwa sababu ya penzi lake la dhati kwa Idi, na kwa sababu ya hali yake ya kiuchumi. Aidha mwandishi ametumia hali hii kuwajuza wasomaji kuwa wakati mwingine, watu hujifanya rafiki wa karibu kumbe watu kama hawa hutaka kujinufaisha tu kifedha kisha waende zao.

### 4.2.7 Kunyimwa Uhuru wa Kutangamana na Marafiki Zao

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* tunamwona Zakaria anavyowanyima binti zake uhuru wa kutangamana na marafiki zao. Hakuwapa wakati wa kupumua. Aliwachunga binti zake mithili ya wanyama. Hakuwapa mwelekeo wakati ule walipokuwa na haja. Pamoja na kuwapiga, aliwakataza kuzungumza na mvulana yeyote. Watoto wake Zakaria walitumia nguvu kujinusuru kutoka kwa dhuluma ya kuzuiwa kutangamana na rafiki zao.Wanafananishwa na mti ambao hujaribu kujirefusha ili kupata mwanga. Watoto hawa hawakuweza kuonywa na mtu yeyote. Hii inamaanisha kuwa Zakaria kama msitu wenye miti mingi, alikuwa amewasonga binti zake kwa masharti magumu. Walipopata fursa kidogo tu, waliyapapia maisha bila kujali athari zake.

Mwenendo wa Rosa ulimfanya Zakaria ajitahidi zaidi katika kazi ya kuwachunga binti zake.Flora akiwa katika shule ya wasichana ya Mwanza, aliweza kukaripiwa kwa maneno ya kuogopesha na matusi. Honarata vilevile alichungwa vikali na alizuiwa kuzungumza na mvulana yeyote. Zakaria alidhani alikuwa akiwalea watoto wake vizuri lakini alikuwa akiwaharibu. Aliwaharibu kwa sababu walijifanya wazuri baba yao alipokuwa karibu tu, lakini wakiwa mbali naye walikuwa wabaya sana. Suala hili liliwafanyawatoto wa Zakaria kukosa imani naye. Kwa sababu hata kama wangekuwa na shida huko nje na wanaume hawangemwambia baba yao kwa maanake walikuwa wakimwogopa wakati yeye alidhani walikuwa wakimheshimu. Utafiti huu uling'amua kuwa kadiri Zakaria alivyozidi kuwachunga binti zake, ndivyo walivyozidi kuwa wabaya. Mtunzi ametumia lugha kwa

ufasaha kupitisha habari kwa wazazi kwamba wanastahili kuwa waangalifu katika malezi ya watoto wao hasa katika suala la uhusiano wa jinsia tofauti.

Watoto wa shulewananyimwa uhuru wa kutangamana na wenzao kama anavyokiri Flora anapomwambia Rosa kuwa shule yao ilikuwa ya ajabu kwa sababu alidai kuwa walilindwa kama watoto wadogo. Flora alishangaa kama hata wakati wa livu walimu wangewachunga. Kutokana na tetesi za Flora, anajiona kama mtu mzima lakini ukweli ni kwamba alikuwa mtoto. Anaposema kuwa walifikiri wangewachunga hata wakati wa livu, anamaanisha kuwa wakiwa mbali na shule huenda walikuwa na uhuru wa kufanya mambo mabaya. Shule ya Flora iliitwa "jela" na wanafunzi, kumaanisha kuwa hawakuruhusiwa kutoka nje ya shule. Kuwachunga watoto wa shule si vibaya mradi kule kuwachunga kufanywe kwa kiasi na wanafunzi waelezwe faida zake. Pana uwezekano kuwa wanafunzi wa shule ya akina Flora walichungwa kupita kiasi, au hawakuonyeshwa faida zake. Isitoshe, shule yenyewe ilikuwa ni ya kimishenari-Katoliki ambapo wengi wa walimu wao walikuwa ni watawa na hivyo, hawangependa wasichana wao waranderande na wanaume wasije wakaharibu sifa za shule yao.

Rosa akiwa katika chuo cha walimu alinyimwa uhuru wa kutangamana na wenzake wakati walimu wake walipoketi na kuamua Rosa afukuzwe chuoni. Uamuzi huu ulimfanya Rosa kutaka kujiua kwa sababuza aibu. Alishughulika sana, kutafutakifaa cha kutumia kujiualakini hatimaye aliamua kujiua akitumia kisu kilichokuwa sandukuni mwake. Rosa aliogopa kujidunga kisu. Binadamu hupenda kuishi kama jamii. Kwa hivyo, uamuzi wa walimu wa kumfukuza Rosa haukufaa kwa sababu walikuwa wakitaka kumtenga kutoka kwa wanafunzi wenzake.Walimu wengi huchukua hatua waliyoichukua walimu wa Rosa. Kuwafukuza watoto kutoka shule kunaweza kuwafanya wanafunzi kujitoa uhai njiani. Kama ni lazima mwanafunzi afukuzwe shule basi walimu wanastahili wamwite mzazi aandamane na mtoto wake, au wampeleke mpaka kwa wazazi wake. Rosa hakuwa mtoto katika kiwango hiki lakini mwandishi alitaka kuonyesha madhara ya kuwafukuza watoto shuleni.

Mhusika Bahati katika riwaya ya *Kiu,* anaonekana kunyimwa uhuru na Idi na ndio maana anataka kwenda Kisiwani akiandamana na mpishi wake. Anamwambia waende wakakae peke yao mahali ambapo wangekula matunda kama watu wa kale. Hapa Bahati anamaanisha kuwa alikuwa amechoshwa na matendo ya Idi na sasa alitaka kuwa mbali naye. Anaposema wakale matunda ya mwituni alikuwa na hasira. Kawaida matunda ya mwituni huliwa na

wanyamapori. Aidha, matunda haya huwa si matamu na mengine huwa na sumu. Kwa hivyo,Bahati anapofanya uamuzi wake, anamaanisha kuwa tabia za Idi zilikuwa mbaya na aliona heri kuishi mwituni, ale matunda ya mwituni kuliko kuishi na mwanadamu mwenzake aliyekosa utu.

### 4.2.8 Kubaguliwa kwa Jumla

Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* alibaguliwa kielimu na babake kwa sababu ya jinsia yake. Licha ya kuwa babake alikuwa mwalimu, hangempa pesa za matumizi shuleni.Rosa alipotaka kurudi shuleni mama yake alimwombea pesa za matumizi ndiposa Zakaria akampatia shilingi ishirini. Dada zake Rosa vilevile, hawakushughulikiwa na wazazi wao na sababu kubwa ilikuwa ni jinsia yao ya kike. Zakaria kama mzazi alihepa majukumu yake kwa sababualipenda sana binti zake waolewe upesi iwezekanavyo iliapunguziwe mzigo begani. Alizoea kulalamika kila mara kuwa kuzaa wasichana ilikuwa ni taabu sana. Mtunzi ametumia hali hii ya watoto kubaguliwa kutuzindua ili tuwachane na mila na desturi zilizopitwa na wakati.Nia ya mtunzi ilikuwa ni kukashifu uzembe kati ya wazazi ambao hukataa kutekeleza majukumu yao. Hii ni dhuluma kwa sababu Zakaria aliwanyima watoto wake fursa ya kuendelea na masomo na hivyo basi alikiuka haki za watoto.

Katika riwaya ya *Kichwa Maji,* mhusika Rukia anabaguliwa kielimu ilhali ndugu yake Kazimoto anapelekwa shuleni na kusoma hadi chuo kikuu. Kubaguliwa huku kielimu kunamfanya kakake kumhurumia na kuamua kumlipia karo ya shule. Hapo ndipo anapokutana na Manase ambaye anampachika mimba na mimba hiyo inasababisha kifo chake. Rukia alisema kuwa maisha yake yalikuwa yameharibika. Vilevile, alisema kwamba alikuwa amekwisha acha shule. Katika muktadha huu,Rukia anamaanisha kuwa tayari alikuwa amepachikwa mimba na hivyo basi, hangeweza kuendelea na masomo yake. Aliwacha shule ili aweze kuilea mimba yake. Rukia alimwandikia ndugu yake barua kumjulisha habari za kupata mimba ndio asijisumbue kumtumia pesa za karo. Utafiti huu uling’amua kwamba, tatizo la wasichana wa shule kupachikwa mimba na watu wazima linawanyima fursa ya kuendelea na masomo yao.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema,* mhusika Rehema anabaguliwa kielimu na babake kwa sababu ya rangi yake nyeusi. Dadake na ndugu yake wa kambo wanapelekwa shule nzuri wakati yeye hakupelekwa hata ile mbaya. Rehema baadaye anagundua kuwa Bibi Adila na watoto wake walikuwa na uwezo na hivyo basi hangeweza kupambana nao. Rehema anadai

kuwa ndugu zake na mamake wa kambo walikuwa na nguvu za mali, elimu na hadhi. Katika hali hii, mtunzi ana nia ya kutufunulia kuwa, kubaguliwa kielimu kwa Rehema kunamfanya akose mali, elimu na hadhi. Mambo haya matatu yanamfanya Rehema ajidharau na kuwaona wenzake kama watu wa maana kuliko yeye. Rehema anabaguliwa kielimu kwa sababu ya maumbile yake. Dhuluma hii inamfanya Rehema baadaye akose ujasiri na ari ya kujitetea alipokuwa katika matatizo.

### 4.2.9 Kutukanwa

Katika riwaya ya *Kichwa Maji* watoto wanatukanwa. Manase alipoulizwa na Kazimoto kuhusu mimba aliyompachika Rukia, Manase anajitetea kuwa Rukia alikuwa malaya tangu alipoota maziwa. Mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* alitukanwa na watu wengi. Mkewe mwalimu mkuu anapomfumania na mumewe anamtukana anapomuuliza kama alikuwa akitaka kumpelekea umalaya wake. Baba yake pia tunamwona akimtukana anaposema kuwa malaya hajawa mgeni wake wala mtoto wake. Aidha, katika riwaya hii mhusika Flora anatukanwa na jamaa za marehemu babake. Wanamwita ‘mwizi’, ‘malaya’ na ‘mshenzi’. Kwa mintarafu hii, mtunzi wa riwaya hizi ametumia neno “malaya” kuonyesha ya kwamba jamii hii haikufurahishwa na waliojishughulisha na uovu huu. Wahusika hawa watatu yaani Rukia, Rosa na Flora ni watoto kwa hivyo, mtunzi anataka kupitisha ujumbe kuwa watoto wanajihusisha na umalaya. Tusi “malaya” huibua hisia mbalimbali linapotajwa. Huenda ikawa mtunzi alilitumia kama njia ya kuwakumbusha watoto kuwa hawastahili kujihusisha na ukahaba. Uchunguzi huu uligundua kuwa mhusika Rukia hakupata mimba kwa kupenda ila tu Manase alitumia nguvu. Aidha, iligunduliwa kuwa kuwatukana watoto hakukuwasaidia kubadilisha mienendo yao maanake walibaki vile vile. Hii ilikuwa ni dhuluma kwa sababu watoto hawastahili kutukanwa bila sababu.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* mhusika Rehema anatukanwa mara kadhaa kwa sababu ya rangi yake nyeusi. Mamake wa kambo hakumpenda hata kidogo. Hili linadhihirika wazi anapomwambia mumewe kuwa tumbo lilimkeketa alipoliona lile toto lake la haramu likicheza na mwanaweSalma na yeye (Fuad) hakufanya lolote. Aidha, Rehema anatukanwa na kukemewa na watumishi wa babake walipomwita kizanda. Kutokana na tusi hili, Rehema hakuweza kuvumilia zaidi kwa sababu aliamua kuondoka kwao na kwenda zake.

Hapa tunaona kuwa, licha ya Rehema kuwa mtoto wa tajiri, anatukanwa na watumishi wa babake. Madharau aliyoonyeshwa Rehema na watumishi, yalitokana na mama yake wa

kambo - yaani walizoea kumwona na kumsikia akimzungumzia kwa hali ya kumdhalilisha Rehema na hivyo basi, nao wakaona kwamba hawakuwa na budi kumtukana Rehema. Rehema alipotusiwa 'kizanda' aliudhika sana hadi akaamua kutoroka kwao.Aidha, Rehema haepuki matusi kwa sababu anapoajiriwa kwa bwana Mansuri anatukanwa na kukaripiwa na Rozi endapo angekawia kufika kazini. Mtunzi ametumia matusi haya kuashiria jamii za Waafrika jinsi zinavyowadhalilisha watoto hasa wakati hawana mtetezi.

Mhusika Bahati katika riwaya ya *Kiu* anatukanwa na kuonyeshwa madharau na Idi anapolalamika kwamba ametaabika miaka mingi, na wala hangekubali kutaabishwa na paka kama Bahati. Matusi haya yanaonyesha wazi kuwa Idi hakuwa na penzi la dhati kwa Bahati na hivyo aliona kama ni taabu kuishi naye kwa sababu alimtumia Bahati kama kitega uchumi. Alipoona amemtumia kupata mali kutoka kwa Mwinyi kama alivyokusudia, alianza kumtukana na kumwonyesha madharau ya kila aina. Anaposema kwamba hangekubali kutaabishwa na paka kama bahati, alikuwa tayari ameamua kuwa angemfukuza Bahati, lakini Bahati hakufahamu vile. Hili linajitokeza wazi wakati Bahati anapomfumania Idi na hawara kwa jina la Rehema, halafu anamsikia Idi akimwita yeye paka na kuwa angemfukuza wakati huo. Kwa kawaida, paka hufugwa kwa sababu za kumsaidia binadamu kufukuza panya. Endapo paka atashindwa kufanya kazi yake, aliyemleta paka yule humfukuza au hata kumuua. Idi anapomfananisha Bahati na paka anamaanisha kuwa Bahati alikuwa pale kwa maksudi tu - yaani kumnufaisha Idi na alipoona kuwa hangeendelea kumnufaisha kifedha aliamua kumfukuza. Utafiti huu ulitambua kuwa chochote king'aacho si dhahabu. Hii ni kwa sababu mwanzoni Idi alijifanya mzuri sana kwa Bahati, lakini baadaye Bahati alifahamu kuwa Idi hakumpenda hata kidogo. Hii ni dhuluma ya kimapenzi kwa sababu Bahati alianza kwa kutumiwa vibaya na Idi – kumlazimisha kufanya mapenzi na mzee Mwinyi kisha baadaye anamtesa na kumtukana.

### 4.2.10Jedwali 1: Muhtasari wa Matatizo Yanayowasibu Wahusika WatotoKatika Riwaya za Kisasa za Kiswahili.

Jedwali hili linaonyesha muhtasari wa matatizo yanayowakumba wahusika watoto. Limeonyesha aina za dhuluma, majina ya riwaya na kurasa zinapopatikana dhuluma hizo. Hatimaye jedwali limeonyesha majina ya wahusika waliodhulumiwa.

| **Dhuluma** | **Riwaya** | **Ukurasa** | **Jina la mhusika** |
|---|---|---|---|
| Kufukuzwa nyumbani | Kichwa Maji<br>Rosa Mistika<br>Nyota ya Rehema | 124<br>58<br>22,24 | Kalia<br>Rosa<br>Rehema |
| Kunyimwa uhuru wa kujieleza | Nyota ya Rehema<br>Rosa Mistika | 42,49<br>6 | Kidawa<br>Rehema |
| Kutosomeshwa na wazazi wao | Kichwa Maji,<br>Rosa Mistika,<br>Kiu,<br>Nyota ya Rehema | 42<br>25<br>118<br>22 | Kalia<br>Rosa<br>Bahati<br>Rehema |
| Kupokonywa Urithi | Rosa Mistika<br>Nyota ya Rehema<br>Kiu | 95/96<br>23, 135<br>153 | Flora na wadogo wake<br>Rehema<br>Bahati |
| Kuchapwa ovyo ovyo | Kichwa Maji<br>Rosa Mistika | 123,103<br>6,7,23, 4,55 | Kalia<br>Rosa na wavulana wawili |
| Kudhulumiwa kimapenzi | Kichwa Maji<br><br>Rosa Mistika<br>Nyota ya Rehema<br>Kiu | 24,26,90,109,124,180,190<br><br>32,33,41,51,52,63,72,83,85,86<br><br>41,42,61,63,65,72,136,137<br>14,48,49,56,63,64. | Rukia, Msichana mdogo, Kalia, Vumilia<br>Rosa, Thereza, wasichana wa shule<br>Kidawa, Rehema<br>Bahati |
| Kutopewa Uhuru wa kutangamana na marafiki zao | Rosa Mistika<br><br>Kiu | 24,36,62,82<br><br>133 | Rosa, Flora, Honarata, Wasichana wa shule<br>Bahati |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutukanwa | Kichwa Maji<br>Rosa Mistika<br>Nyota ya Rehema<br>Kiu | 22<br>4,57<br><br>22,50<br>97/148 | Rukia<br>Flora, Rosa<br><br>Rehema<br>Bahati |

Kutokana na jedwali hili, ilibainika kuwa watoto walisibwa na matatizo mbalimbali. Kati ya riwaya nne zilizochunguzwa, tatu zilionyesha kuwa wahusika watoto walifukuzwa nyumbani. Riwaya hizi ni; Kichwa *Maji, Rosa Mistika* na *Nyota ya Rehema* ambapo wahusika walikuwa ni Kalia, Rosa na Rehema mtawalia.

Kuhusiana na dhuluma ya kunyimwa uhuru wa kujieleza, riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Rosa Mistika* zilifichua kwamba mhusika Kidawa na Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* walinyimwa uhuru wa kujieleza. Vilevile, mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* alinyimwa uhuru huu. Dhuluma ya watoto kutosomeshwa na wazazi wao ilijitokeza katika riwaya zote nne zilizochunguzwa. Wahusika walioathiriwa ni Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji*, Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Bahati katika riwaya ya *Kiu* na Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*.

Kulingana na jedwali hili, ni wazi kuwa watoto walipokonywa urithi wao. Hili liligunduliwa katika riwaya tatu zilizochunguzwa. Katika riwaya ya *Rosa Mistika,* Flora na wadogo zake walipokonywa urithi wao na jamaa za marehemubaba yao. Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, Rehema alipokonywa urithi na ndugu zake wa kambo. Aidha, mhusika Bahati katika riwaya ya *Kiu* alipokonywa urithi. Suala la kuchapwa bila sababu lilijitokeza katika riwaya mbili kati ya riwaya nne zilizochunguzwa. Riwaya hizi ni *Kichwa Maji* na *Rosa Mistika*. Wahusika waliochapwa bila sababu ni Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji*, Rosa na wavulana wawili katika riwaya ya *RosaMistika*.

Katika riwaya nne zilizochunguzwa, zote zilithibitisha kuwa wahusika watoto walidhulumiwa kimapenzi. Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, wahusika kadhaa walijikuta katika dhuluma hii. Hawa ni: Rukia, Msichana Mdogo, Kalia na Vumilia. Riwaya ya *Rosa Mistika* ilionyesha kuwa, Rosa, Thereza na wasichana wa shule walidhulumiwa. Kidawa na Rehema katika riwaya ya*Nyota ya Rehema* nao walidhulumiwa kimapenzi. Aidha, katika riwaya ya *Kiu*, mhusika Bahati alidhulumiwa kimapenzi.

Kufuatana na jedwali hili, ni wazikuwa riwaya mbili kati ya zile nne zilizochunguzwa, zilionyesha kuwa watoto hawakupewa uhuru wa kutangamana na wenzao. Riwaya hizi ni

*Rosa Mistika* na *Kiu*. Wahusika walioathirika katika riwaya ya *Rosa Mistika* ni Rosa, Flora, Honarata na wasichana wa shule. Katika riwaya ya *Kiu*, mhusika aliyeathirika ni Bahati.

Dhuluma ya watoto kutukanwa katika riwaya zote nne zilizochunguzwa vile vile iliweza kujitokeza. Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, mhusika Rukia alitukanwa. Flora na Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* nao pia walitukanwa. Aidha, katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Kiu*, wahusika Rehema na Bahati walitukanwa mtawalia.
Kutokana na jedwali A, ni muhimu kutaja kuwa, watoto walisibwa na matatizo mbalimbali. Dhuluma iliyokithiri katika riwaya zote zilizochunguzwa ni watoto kudhulumiwa kimapenzi. Hii ni kwa sababu jedwali linaonyesha kuwa wahusika watoto walidhulumiwa mara kadhaa katika riwaya zote nne.

## 4.3Majukumu Yanayotekelezwa na Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Neno majukumu katika utafiti huu linaashiria matendo wafanyayo wahusika watoto ili kujikimu kimaisha. Matendo haya yanaweza kuwa ya makosa au ya kutekeleza wajibu. Watotowanatekeleza majukumu kadhaa katika riwaya zilizochunguzwa. Majukumu haya ni kuchuma rasilimali kwa njia yoyote ile. Kwa mfano,ukahaba, kulima, kupika na kuuza pombena wizi. Majukumu mengine ni kama vile; kuwalea wadogo zao, kusoma na kuteka maji. Baadhi ya majukumu hayo yaliweza kujidhihirisha kama ifuatavyo:

### 4.3.1 Kuchuma Rasilimali

Baadhi ya wahusika watoto katika riwaya zilizochunguzwa waliamua kutumia mbinu duni kuchuma rasilimali. Walilazimishwa na hali yao ya maisha kutumia mbinu hizi.Katika utafiti huu, mbinu duni zilizotumika katika uchumaji rasilimali ni; ukahaba, kulima, kupika na kuuza pombe.Aidha, wiziulitekelezwa kama mojawapo ya mbinu za kuchuma rasilimali.

#### i) Ukahaba

Kwa mintarafu ya madhumuni ya pili ya utafiti huu, ukahaba ni kati ya majukumu mengi wanayoyatekeleza watoto. Kwa mujibu wa utafiti huu, ukahaba ni jukumu kwa sababu watoto wanasukumwa na hali yao mbaya ya kiuchumi kushiriki ukahaba. Ukahaba hapa uligawanywa katika sehemu nne- yaani kuegemea riwaya zote nne zilizochunguzwa.

### a)Ukahaba Katika Riwaya ya *Kichwa Maji*

Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, watoto wanajiingiza katika ukahaba wakiwa bado wachanga. Suala hili linachochewa na hali yao ya maisha. Vilevile, mazingira wanamoishi hamna anayejali hali yao. Hili linaonekana Manase na Kazimoto wanapozozana kuhusiana na mimba aliyompachika Rukia. Manase anasema kuwa Rukia alikuwa malaya tangu alipoota maziwa. Kufuatana na tetesi za Manase, yaani kumwita Rukia 'malaya'ni mbinu tu anabuni kwa kutaka kuonyesha kuwa Rukia hakuwa mwaminifu tangu alipokuwa mdogo. Manase anatamka maneno haya kama njia tu ya kujitetea kwa sababu hakuna sehemu katika riwaya hii inayomwonyesha Rukia akifanya umalaya. Hata hivyo, mtunzi anataka kupitisha ujumbe kuwa katika jamii hii kuna watoto waliofanya ukahaba wakiwa bado wadogo kwa umri. Hii ni taswira ambayo imetumiwa na mtunzi kuonyesha hali ya watu wanaojiweza kuwapachika wasichana mimba na kukana kuwa hawakuhusika. Utafiti huu uligundua kuwa ukahaba ulirithiwa kutoka kwa ndugu wakubwa hadi kwa wadogo zao.

Katik ariwaya ya *Kichwa Maji*, Kalia nduguye Kazimoto haoni ubaya wowote kumshika Vumilia rafikiye Kazimoto kiunoni. Kalia anamwambia Vumilia kuwa yeye ni shemeji yake kwa hivyo hakustahili kujali sana. Kalia baada ya kushuhudia kakake Kazimoto akijihusisha na mambo ya wasichana, anamwambia kuwa hatakuwa akimpeleka kuwachukua wanawake akidai kuwa hakuwa akipata usingizi vizuri siku yoyote aliyomsaidia Kazimoto kuleta msichana. Kalia alitaka Kazimoto awe akimsaidia kupata wasichana. Yaani siku ambayo Kazimoto analeta naye awe akileta. Jambo hili linamfanya anung'unike sana. Suala hili pia linamfanya Kalia abadilike na kuwa mbaya zaidi kwa upande wa wanawake. Wakati Kazimoto walikuwa wakiendesha mapenzi, kitu fulani cha ajabu kilikuwa kikitendeka kijijini. Kalia alianza kufanya maovu yaliyompelekea kutaniwa 'nunda'mlawatu. Mwanzoni hakuwa akijulikana. Aliingia nyumba za watu usiku hasa zile nyumba ambamo walikuwa wakilala wanawake watupu.

Wakati wote alipopanga kuwaingilia, alijihami na kisu na kuwashurutisha wamtimizie haja yake bila kupiga kelele. Isingekuwa Kazimoto, Kalia hangejiingiza kwa mambo ya wanawake mapema na pengine hangeitwa "nunda mla watu." Mtunzi ametumia haya maneno kusisitiza jinsi tabia za Kalia zilivyobadilika na kuwa kama za mnyama. Aidha, anataka kuonyesha kuwa watoto wakubwa wanaweza kuwaharibu wadogo zao ikiwa watawachiliwa kufanya watakavyo. Kwa hivyo, ni jukumu kwa wazazi kuelewa tabia za watoto wao na kuwapa mwelekeo unaofaa maishani. Hata hivyo, ukahaba pia uliendelezwa kati ya vijana na

watu wazima. Tunamwona Tegemea anavyopewa pesa na Kalia ambaye ni mtoto mdogo ili waweze kushiriki mapenzi. Hata wakati Kalia anapombaka msichana na kutafutwa, Tegemea ndiye alimpa mahali pa kulala lakini alighadhabisha watu. Kwa sababu ya ukahaba, Kalia aliendelea kuwa na uchu mkubwa hadi ikapelekea kifo chake. Lakini ukahaba huu ulitokana na ndugu yake mkubwa Kazimoto kama anavyokiri:

> ….Mwisho wake uliendelea kunisumbua moyoni, kifo chake kilihusika sana na matendo yangu. Ilikuwa kama mimi mwenyewe nilimwua mdogo wangu ……….mimi ninasema hivi kwa sababu nimemwona mdogo wangu akiuawa kwa sababu ya kufuata matendo yangu mabaya. Mimi mwenyewe nilikuwa nunda mla watu … (uk. 129, 144-145).

Kulingana na kifungu hiki cha maneno, matendo mabaya yanarejelea ukahaba aliojihusisha nao Kazimoto. Anaposema kuwa kifo cha Kalia kilitokana na matendo yake (Kazimoto), anamaanisha kuwa kumchukua Kalia kwenda kuwatafuta wasichana pamoja kulichangia Kalia pia kuwa na hamu ya kuwatafuta wasichana. Suala ambalo hakuweza kujidhibiti kwalo na hatimaye likasababisha kifo chake. Kazimoto anaposema kuwa yeye mwenyewe ndiye alimuua ndugu yake anamaanisha kuwa yeye ndiye alikuwa kielelezo kibaya kwa Kalia. Utafiti huu uligundua kwamba katika familia nyingi, watoto huiga tabia za ndugu zao wakubwa. Hii ina maana kuwa tabia za mtoto wa kwanza zikiwa mbaya au nzuri, basi watoto wengine hufuata mkondo huo huo. Mwandishi hapa anataka kuwapasha wasomaji habari kuwa wazazi wanapogundua tabia mbaya miongoni mwa watoto wao, wanastahili kuikashifu na kuwaeleza watoto wengine wasijihusishe na tabia kama hizo.

Mhusika mtoto Vumilia anaamua kuwa kahaba kwa muda mrefu na mwishowe anaamua kuolewa na mtu ambaye ni maskini sana. Mama yake Vumilia anaamua kwenda kumtafuta kakini Vumilia ana sababu zake za kuolewa na kukimya tu bila kumjuza mamake mzazi. Vumilia anamwambia Kazimoto na mamake kuwa kati yao hakuna aliyempenda. Anawaambia kuwa Maisha yake yalianza kuharibika tangu zamani na wakati huo hawakusema lolote. Alishangaa ni kwa nini waliamua kwenda kumtafuta na kumchukua. Anawaambia kuwa mwili aliokuwa nao ni wake na kwamba atakapokufa wapige ngoma, wakatangaze kote kijijini kwamba mbwa wa maskini amelamba mchanga. Alirudia tena kumwuuliza mamake swali kuwa baba yake (Vumilia) ni nani. Aliwafahamisha kwamba maisha yake yalianza kuharibika alipokosa kumfahamu baba yake. Uchunguzi huu ulitambua kuwa ukahaba wa Vumilia ulitokana na tabia za mama yake mzazi. Vumilia aligundua kuwa mama yake alikuwa kahaba na ndio maana hakutaka kumweleza baba yake alikuwa nani.

Mtunzi anatumia taswira hii kupitisha ujumbe kuwa wazazi wakiwa na tabia mbaya kama vile ukahaba, wanastahili kuchunga sana wasiwaathiri watoto wao. Vilevile, watoto wengi ambao mama zao ni makahaba humalizia kuwa makahaba kama mhusika Vumilia.

**b)Ukahaba Katika Riwaya ya *Rosa Mistika***

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rosa anaanza ukahaba akiwa mwanafunzi. Ukahaba huu ni kati ya wazee matajiri na watoto wa kike. Mmoja wao alikuwa ni Deogratias aliyedai kuwa watoto wa shule ndio walikuwa na joto. Deogratias anakuwa mwanamume wa kwanza kumshika Rosa mikononi. Kutokana na malezi ya kuchungwa aliyopata, Rosa anampenda yule mwanaume wa kwanza kuonana naye. Mtunzi anaposema "malezi mazuri" anarejelea maisha ya kuchungwa kupita kiasi aliyoyapitia Rosa. Baba yake alichangia Rosa kuwa kahaba kwa sababu alimwonyesha kuwa wanaume ni wabaya na hivyo, Rosa alipopata fursa ya kuongea nao, alikuwa mbaya zaidi. Kutokana na maisha yake ya awali, Rosa aliishi akiwachukia na kuwaogopa wanaume lakini ilifika mahali alitaka kuwadhihirishia wanaume kuwa angeweza kukabiliana nao katika masuala ya mapenzi. Rosa anaogopa kuonekana kana kwamba hajui lolote na hivyo basi, anajaribu kujitetea na kuonyesha kuwa anaweza kufanya jambo. Siku moja akiwa ndani ya baa, anakutana na mwanamume mmoja na anamwambia afike siku iliyofuata ili aone anavyonoga. Tunaona ya kwamba Rosa alifunzwa na wanawake wazee ambao walikuwa wamezoea ukahaba. Hapa ndipo Rosa alifahamu mapenzi ya unyonyaji. Rosa aliona kama mapenzi ya mwanamke mara nyingi huenda pamoja na unyonyaji. Mtunzi anaposema "mapenzi ya unyonyaji" anamaanisha kuwa wanawake huwahadaa wanaume eti wanawapenda kumbe wao hufanya hivyo ili wapate pesa kutoka kwao. Anatuchorea picha kwamba wanaume huumizwa na wanawake katika suala hili la ukahaba.

Dhana hii haina mashiko kwa sababu hapa hali ya kuogopa kuonekana kana kwamba yeye ni zuzu katika mambo ya mapenzi inamlazimisha Rosa kuwapenda wanaume. Uchunguzi huu uligundua kwamba Rosa alikosa uwezo wa kudhibiti mawazo na matendo yake. Hii ni kwa sababu Rosa alipenda kupendeza kila mvulana maanake kati ya wasichana Rosa ndiye alikuwa wa kwanza kujulikana. Iligunduliwa kwamba, kutokana na ukahaba Rosa alipata mimba na akaamua kuitoa. Haikuwa rahisi kutoa ile mimba kwa sababu aliathirika kiafya. Mimba hii nusura igharimu maisha yake kwa sababu alikaa hospitalini akiwa mahututi kwa kutoa mimba ya miezi miwili. Akiwa pale, wavulana wengi walimkosa Rosa na walimwombea apone upesi. Utafiti huu ulitambua ya kwamba wavulana walikuwa

wakimkejeli walipomwombea kwa sababu walimchukia kiasi cha kumwita “lab.” Rosa alizoea kutukanwa na alijipa moyo kwa kusema kuwa waliokuwa wakimtukana walikuwa wakifanya kazi bure. Suala hili lautoaji mimba lilikuwa kama kawaida kwa wasichana wa shule. Wasichana hawakuona haja ya kuzaa watoto wakiwa bado shuleni. Flora dadake Rosa naye huko shule ya wasichana ya jela (hili lilikuwa jina la utani la shule ya wasichana huko Mwanza iliyokuwa inalindwa na polisi) alikuwa amekwishatoa mimba. Anaonekana kutojali sana anapomalizia barua yake akisema kuwa mimba haingemfanya ajiharibie maisha yake kwa kuacha shule.

Kutokana na maneno aliyoyatamka Flora, ni wazi kuwa watoto wa shule walishiriki mapenzi kiholela holela. Hawakutaka kujua matokeo yake kama vile mimba zisizotakikana. Ni kutokana na ukahaba wa watoto wa shule ambapo Flora anapata mimba. Anaposema kuwa “mimba haiwezi kunifanya nijiharibie maisha” anaamanisha kuwa yeye akipata mimba ataitoa. Mtunzi amewachora wasichana wakiwa katika hali ya kutojijali. Haya ni mawazo mabaya waliyokuwa nayo. Rosa alipotoa mimba mara ya kwanza hakujifunza lolote kwa sababu akiwa katika mwaka wa pili alitoa mimba tena. Jambo hili lilifanya sifa za Rosa zilijulikane Morogoro nzima hadi padri mmoja anatumwa kwenda kumwonyesha mwanga wa wokovu. Ukahaba ulimfanya Rosa akafikia mahali ambapo hakujithamini yeye mwenyewe. Alikuwa ametamauka maishani wakati Padri anapojaribu kumzungumzia kuhusu maisha yake. Rosa kupitia kwa mazungumzo kati yake na Padri alikuwa ametamauka kama inavyodhihirika:

> “Rosa nimekuja kukusaidia; nimekuja kukuonyesha tena mwanga wa wokovu.”
>
> “Umekuja kunisaidia! Mimi maskini?”
>
> “Ndiyo wewe maskini wa roho.”
>
> “Umejuaje, wewe Mungu?”
>
> “Mwovu huonekana kwa matendo”
>
> “Umeyafahamuje matendo yangu?”
>
> “Dalili ya moto ni moshi. Hujapata mimba wewe hata mara moja?”
>
> “Ya nani…Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto nitakwenda!” (uk. 49)

Kuhusiana na maswali haya ya Rosa ni dhahiri kuwa Rosa hakuona kitu chochote kizuri tena maishani mwake. Alikuwa tayari kwenda motoni kwa sababu alijiona mbaya sana. Rosa anasema kuwa amepata taabu sana maishani. Kulingana naye, ni kama shida zake zote

zilisababishwa na watu wengine lakini sivyo. Shida zingine alizisababisha yeye mwenyewe. Padri alijaribu kumwonyesha Rosa kwamba kulikuwa na nafasi ya kurekebisha maisha yake lakini Rosa alikuwa tayari ametamauka. Hii ni kwa sababu Rosa alifanya ukahaba na watu wa umri wote- vijana, wazee, hata na walimu wake. Jambo hili linamfanya kupigwa na kuumizwa mwili wake. Rosa alizoea kwenda densi na kulala na wanaume ovyoovyo. Hili linadhihirika wazi mtunzi anaposema kuwa Rosa aliona kwamba ameshinda wakati alikuwa akimpangusa jasho mwalimu mkuu wa chuo. Huu ni ushahidi kuwa, Rosa alifanya mapenzi na mwalimu mkuu ili amtetee asifukuzwe shuleni na hivyo angekuwa mshindi kwa sababu angeendelea kuonekana chuoni licha ya walimu kuamua afukuzwe. Uchunguzi huu ulitambua kuwa Rosa alikubali kushiriki mapenzi na mwalimu mkuu kwa sababu alitaka angalau asifukuzwe ili aweze kuendelea na masomo yake. Kwa upande mwingine naye mwalimu mkuu alichukua fursa hii kuendeleza ukahaba. Mwalimu mkuu alistahili awe kielelezo kizuri kwa mwanafunzi wake Rosa na wala si kutumia unyonge wake kutimiza haja zake za kimapenzi.

Watu wazima ndio chanzo cha tatizo hili la ukahaba kama inavyodhihirika kutoka kwa kijana mmoja basini aliposema hivi;

> Shule hii hapa! Bure sana ingawa wanalindwa. Wanachukuliwa na wapishi wa Wahindi mjini kwa sababu ya kulindwa wamekuwa kama wanyama, wanapenda mtu yeyote yule apataye bahati kuonana nao. Wamepoteza uwezo waowa kuchagua.
> (uk.63).

Kwa mintarafu ya kifungu hiki cha maneno, mwandishi anapowafananisha wasichana wa shule na wanyama anamaanisha kuwa matendo yao si kama ya watu wenye akili timamu. Kulingana naye, kulindwa ndio kumewafanya kuwa na tabia hii. Huenda ikawa wasichana hawa wa shule hawakuelewa madhara ya kuchukuliwa na wanaume yaani wapishi wa Wahindi. Hivyo basi, walimu walistahili kuwaambia ni kwa nini walikuwa wakiwachunga hivyo. Pengine wasichana hawa wa shule wangejidhibiti katika masuala ya mapenzi na wanaume hawa wazee ambao nia yao ilikuwa ni kuwatumia tu kisha wawaache. Watoto wengine katika riwaya hii kama vile Rosa alianza kujua mambo ya mapenzi akiwa katika darasa la tano. Hili analikumbuka wanapokutana na Charles baada ya miaka kadhaa. Rosa anamwambia Charles kuwa mapenzi yao yalikatwa kwa nguvu yakiwa yangali mabichi.Charles alikuwa akikumbuka vizuri sana. Rosa aliwakashifu watu wazima na kusema kwamba wazazi wanastahili kutumia madaraka yao kwa uangalifu. Hata hivyo, Rosa hakukumbuka kuwa yeye alikuwa bado mtoto na kuwa hakustahili kujiingiza katika suala la

mapenzi akiwa bado mchanga. Mtunzi anataka kupitisha ujumbe kuwa watoto hukaidi amri na kuwalaumu wazazi wao wakati mwingine bila sababu.

Baada ya kufanya ukahaba kwa muda mrefu, Rosa anagundua kuwa hakuna faida yoyote anapata. Anataka kutulia ili aolewe. Kwa bahati mbaya mambo hayamwendei vizuri kwa sababu waliofahamu maisha yake ya awali, waliingilia kati na kumweleza Charles ukweli wa mambo. Hili linajitokeza wazi wakati kijana mmoja alipomwambia hivi;

> Ninakuonea huruma sana, huyo mwanamke si wa kuoa. Kama unaniamini, afadhali umwache tangu kesho. Rosa, siyo Rosa jina lake? Sasa unafikiri mimi nilimfahamuje, tulipokuwa Morogoro alikuwa anagawa kweli! (uk.79).

Katika unukuzi huu, tunaona ya kwamba Rosa kweli alijulikana sana kwa matendo yake maovu kwa sababu haikuwa mara ya kwanza wala ya mwisho kwa Charles kuambiwa hasara ambayo angepata angemwoa Rosa. Maneno "huyo mwanamke si wa kuoa" yanamrejelea Rosa na yanamaanisha kuwa Rosa alikuwa amefanya ukahaba kwa muda mrefu, alikuwa ameavya mimba mara mbili na kwa hivyo, hakufaa kuolewa na kuwa mke wa mtu. Pengine kijana huyu alimhurumia Charles kwa kuona kuwa hata kama Rosa angeolewa angemwacha mumewe na kuendelea na ukahaba wake. Ukahaba unasababisha kifo cha Rosa. Charles alipogundua kuwa Rosa si bikira, alimwandikia barua ya kumjuza ukweli aliougundua yeye mwenyewe. Rosa alipoisoma alisononeka sana moyoni mwake kwa kujua kuwa Charles hakuwa tayari kumwoa.

Rosa anaamua kujiua kwa kusaga chupa, kuweka kwa glasi na kuweka maji ili kuinywa. Anakumbuka wale wanaume woteameshiriki nao ukahaba na anatamka maneno kadhaa. Kabla ya kukata kamba, anasema kwamba;

> Sasa ninakufa; ninakufa sasa. Maisha yangu yalikuwa magumu. Sasa nimeona wazi kwamba malezi yangu yalikuwa chanzo cha taabu. Malezi siyo malezi ya mama, lakini malezi ya baba yangu. Kweli baba yangu alinichunga. Nilichungwa kama wasichana wa jela. Nilipopata uhuru nilishindwa kuutumia. Deogratias, Thomas, Charles wote hao nimewapoteza(uk.91).

Katika muktadha huu, Rosa anajaribu kukumbuka maisha yake tangu utotoni mwake kufikia utu uzima. Anakiri kuwa malezi ya babake ndiyo yalimfanya awe kahaba alivyokuwa. Anasema kuwa baba yake alizoea kumchunga na anapopata uhuru anashindwa kuutumia. Uhuru anaozungumzia Rosa ni kule kuwa mbali na baba yake. Kule kushindwa kuutumia ule uhuru ni kukosa uwezo wa kuwa na msimamo. Hajui ampende mwanamume yupi na

amwache nani kwa sababu alimpenda yeyote aliyemtaka kimapenzi. Hili linajitokeza wazi muda mfupi tu kabla ya kifo chake, anawakumbuka baadhi ya wanaume ambao amekuwa na uhusiano nao. Kama alivyokuwa Rosa, watoto wengi wanapoenda kwa shule za mabweni wao hufikiria kuwa wamepata uhuru na kufanya maovu watakayo eti kwa sababu wazazi wao hawawaoni. Mwandishi alitaka kuwajuza wasomaji ya kwamba mtaka yote wakati mwingine hukosa yote. Hii ni kwa sababu kati ya wanaume wote Rosa alihusiana nao, hakuna aliyemwoa. Anataka watoto waweze kuwajibika hata kama wako mbali na wazazi wao.

### c) Ukahaba Katika Riwaya ya *Nyota ya Rehema*

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, ukahaba uliendelezwa kati ya wasichana wadogona watu wazima. Rehema kwa kutokuwa na wa kumtegemea, alijiunga na wasichana wengine kuendeleza ukahaba. Hakufanya hivi kwa hiari yake, bali kwa kutaka kutosheleza mahitaji yake ya kimsingi. Wasichana hawa, Ruzuna, Chiku na Kidawa walizoea kuwaleta wanaume kwa chumba chao kidogo. Walikitumia kwa zamu lakini wengine walilalamika eti wengine walipoingia mle ndani walikawia kutoka. Ingawa wasichana hawa walikuwa marafiki, ukahaba uliwafanya kuchukiana ndani ya nyoyo zao. Hili linadhihirika wazi Ruzuna anapowakashifu Chiku na rafiki yake wa kiume akisema kuwa;

> … Isitoshe Kidawa huyo keshakuja na wake, anamsubiri Chiku atoke, na Kidawa hana dogo, akiingia sasa hivi sijui atoke saa ngapi. Uchu huu uchu gani usokuwa na nadhari? (uk. 55)

Kifungu hiki cha maneno kinamaanisha kuwa Kidawa alikuwa gwiji kwa mambo ya mapenzi na hivyo alipoingia chumbani hakutarajiwa kutoka mle haraka. Hili lilimfanya Kidawa kuwa tishio kwa Ruzuna.Maneno “Uchu usokuwa na nadhari” yanaashiria kuwa hata kama Kidawa alifanya mapenzi, alipungukiwa na busara. Jambo ambalo Ruzuna hakukumbuka ni kwamba wote walifanya ukahaba na kwa hivyo, hakuna aliyekuwa mzuri kuliko mwingine. Rehema hakuwa na ujuzi wowote kuhusu mambo haya kwa hivyo hakuelewa kilichokuwa kikiwasumbua wasichana wenzake. Hakujua yaliyokuwa yakijiri katika chumba kidogo mlango ulipokuwa umekomewa kwa ndani.

Mtunzi anasema kwamba dunia ilikuwa haijamfichulia sehemu kubwa ya uhai wa kiumbe. Hapa mwandishi anamaanisha kwamba Rehema hakuwa na tajiriba yoyote kuhusu ukahaba. Hakufahamu uzuri au ubaya wake. Maneno haya yanaonyesha dhahiri shahiri kwamba Rehema hakuwa kahaba na hakuwa tayari kujiingiza katika suala hili. Watoto wengi kama

Rehema hujipata katikati ya marafiki wanaofanya uovu na wao hushindwa kujitenga kwa kuhofia kuwachwa na rafiki zao.

Chumba cha wasichana kilikuwa kama danguro. Waliwabadilisha wanaume kama nguo. Wanaume walifika huko bila woga wowote. Ukahaba huu uliwafanya wanaume wapigane kwa ajili ya watoto hawa wasichana. Kwa mfano, wanaume wawili wanaanza kupigana hadi watu wanasikia mishindo ya ngumi. Kilichosababisha vita kati ya wanaume hawa wawili ni kwamba wote wawili walikuwa wamekuja kwa ajili ya Chiku. Mmoja wao alipogundua kwamba Chiku alikuwa mle chumbani akiendesha ukahaba, aligonga mlango hadi pete ikakatika na hapo ndipo walianza kupigana. Chiku anaonekana kuwa na uzoevu wa vita vya wanaume waking'ang'ania wasichana. Hii ni kwa sababu wakati walipokuwa wakipigana yeye alikuwa akiwashangilia. Wasichana hawa wamezoea kuyaona haya isipokuwa Rehema aliyetoka mbio kuingia chumbani, Kidawa alipiga 'mtume' na Chiku aliziba kinywa kwa mkono ili kukizuia kicheko kilichokuwa kikimsonga katika koo lake. Utafiti huu uligundua kuwa hali yao ya umaskini iliwafanyawatoto hawa waendeshe ukahaba katika vyumba vidogo vyenye walikuwa wamevikodisha. Hili linadhihirika wazi kwa sababu walitumia kitanda kimoja kwa zamu. Rehema kwa unyonge wake yeye hakuweza kung'ang'ania. Ruzuna anamhimiza Rehema ajifunze kupigania haki zake. Hili linadhihirika wazi wakati Ruzuna anamwambia kuwa si dunia ya wanyonge. Ruzuna hapa anamtaka Rehema pia aweze kupigania kupata nafasi ya kukitumia kile kitanda kama wale wengine. Siku moja Rehema alirudi nyumbani na kumkuta mwanamume mgeni akimngoja kitandani, Rehema alishikwa na hofu. Aliamua kumshitakia kwa Chiku. Neno "kumshitakia" linaashiria kuwa Rehema hakuwa na umaarufu wowote katika masuala ya ukahaba.

#### d)Ukahaba Katika Riwaya ya *Kiu*

Katika riwaya ya *Kiu*, Idi anamshurutisha Bahati kushiriki mapenzi na mzee Mwinyi. Katika muktadha huu, Idi ndiye anachochea ukahaba  kwa sababu anasema;

> lakini nimekueleza kuwa huu ni mpango tu. Ukiukubali tutatajirika mimi na wewe na kisha tuoane, tustarehe. Kwa nini tuache mifedha ya mzee yule? Wewe huoni ilivyo rahisi kuipata? (uk. 14).

Kutokana na unukuzi huu, Idi moyoni mwake anajua anachokipanga. Anamaanisha kuwa Bahati akikubali kufanya mapenzi na Mwinyi, watapata pesa kutoka kwa Mwinyi. Anapomuuliza Bahati kuwa yeye hakuona ilivyokuwa rahisi, anamaanisha kuwa Bahati alihitajika tu kushiriki mapenzi na kisha wazipate zile pesa.  Hana mapenziya dhati kwa

Bahati. Baada ya kutoelewana kuhusiana na suala la Bahati kumkubali mzee Mwinyi, Bahati anarudi kwa Idi kama ishara ya kumwomba msamaha. Idi anaangua kicheko cha dharau na kusema maneno ya kitoto. Idi alimwambia Bahati wazi kwambamapenzi na starehe havipatikani kwa mikono mitupu. Vilevile, alimwambia kwamba maisha si kupigana na tumbo tu, kutamani na kumezea mate. Maneno "huu ni mpango…ukiukubali…" yaliyotamkwa na Idi, yanamaanisha kuwa Idi alikuwa akimpangia Bahati kushiriki ukahaba lakini Bahati hakupendezwa na uamuzi huu. Idi alimtaka Bahati akubali kufanya mapenzi na Mwinyi. Hapa Idi ndiye aliyechochea ukahaba akiwa na nia ya kujitajirisha kutoka kwa mzee Mwinyi. Alichochea kwa sababu Bahati anapoonyesha kuwa na moyo mgumu, Idi anamshtua kuwa angemwacha. Jambo hili huwafanya wasichana wengi kushiriki mapenzi hata kama hawakukusudia. Idi hakuona kama walikuwa wakimwibia Mwinyi kwa hivyo, alitumia maneno matamu ili Bahati akubali. Hata kama Bahati alikaa mgumu mwanzo mwanzo, hatimaye alikubali matakwa ya Idi kwa kuogopa kuwachwa na Idi.

**ii)Kulima**

Katika riwaya *ya Rosa Mistika,* mtoto Rosa anapofaulu kujiunga na shule ya sekondari, babake Zakaria alimwambia alime shambani ili kupata pesa za matumizi. Alimwambia Rosa kuchimba eka moja. Dada zake walimsaidia ingawaje kazi hii ilichukua muda mrefu. Kuchimba, kutoa maganda, kukausha na kuuza mihogo haikuwa kazi rahisi. Baada ya majuma matatu udaga ulikuwa tayari lakini wanunuzi hawakupatikana. Jambo hili lilimfanya Rosa atamauke. Hapa inaonekana wazi kwamba wazazi hata kama walikuwa na uwezo hawakuwa tayari kuwalipia watoto wao karo hivyo waliwapa kazi ngumu ya kulima shamba. Eka moja ni sehemu kubwa ya ardhi inayostahili kulimwa na trekta na wala sio watoto wadogo. Suala hili linakuwa na athari kwa watoto hawa kwa sababu hawatiliiielimu maanani na huenda ikawa ndio maana Flora anapoanguka mtihani katika shule ya sekondari hajali. Hili linadhihirika wazi tunapoambiwa hivi;

> Majibu ya mtihani wa Cambridge yalipokuja … majibu hayakumshtusha hata kidogo. Flora alishindwa, hata GCE hakupita … "Tutajali nini sisi hali tumekwishajikabidhi!" (uk.85)

Honarata naye baadaye anawacha shule akiwa katika shule ya msingi. Zakaria anakiuka haki za watoto kwa sababu anawafanyiza kazi nyingi kuzidi uwezo na umri wao. Mtunzi amewatumia wahusika watoto katika riwaya hii kupitisha ujumbe kuwa watoto wengi katika nchi za Afrika Mashariki na bara lote la Afrika hulazimishwa kufanya kazi ngumu na wazazi

wao. Aidha, ametumia hali hii ya watoto kuwacha shule na kuanguka mtihani kuwazindua wazazi na watoto wengine ili watilie maanani suala la elimu.

### iii) Kupika na Kuuza Pombe

Watoto katika riwaya ya *Rosa Mistika* wanapewa majukumu ya kupika. Tunamwona Regina akimsifu mmoja kati ya mabinti zake Flora, alipopika ugali siku moja na kuupakua. Regina alimsifu na kumwambia kwamba bwana ambaye angemwoa angepata bahati. Si chakula tu walipika,bali hata pombe. Wakati Rosa alikuwa anastahili kwenda shule, Zakaria babake alifungua sanduku la Rosa nakuzichukua pesa ambazo zingetumika kukidhi mahitaji yake. Mamake Rosa kwa upande mwingine alipenda sana watoto wake wasome. Alitafuta mbinu ya kupata pesa haraka nayo ilikuwa kupika na kuuza pombe. Alisaidiwa na Rosa kufanya kazi hii.

Rosa hakupika au kuuza pombe kwa hiari, alilazimika kufanya hivyo kwa ajili ya kupata pesa za kutumia. Walitayarisha pombe mapipa matatu naRosa mwenyewe ndiye alikuwa akiuza. Kazi hii ya kuuza pombe iliwazuia watoto wa Zakaria kwenda shule ili nao pia washiriki katika ile biasharaya kuuza pombe. Waliamriwa kusalia nyumbani ili wasaidie kuchota maji na kuosha vyombo vilivyotumiwa na wateja wa mama yao. Hata kama ni kutokana na mapenzi, mama yao alipowahusisha katika upishi na uuzaji wa pombe, alikiuka haki za hawa watoto. Alistahili kushtakiwa kwa sababu baadaye hawa watoto hasa Rosa na Flora wanakuwa walevi wa kupindukia. Vilevile, kutayarishwa pombe kwa Zakaria kwa mara ya kwanza kulileta athari kubwa kwa watoto wake. Ilikuwa mara ya kwanza kwa Stella kuona walevi, matendo yao na kusikia aina za maneno wayazungumzayo walevi.Honarata alipokuwa akiosha bakuli, Stella alimwambia aone mtu mmoja aliyekuwa akikojoa karibu nao.Stella mwishowe aliwazoea, kwani aliwaona wakikojolea michungwa, migomba, maua na hata nyumba. Haikuwa picha nzuri watoto kuona uchi wa watu wazima.

Kushiriki katika upishi wa pombe kuliwafanya watoto waanze kuinywa hata kama walikuwa na visingizio vya kuwafanya wanywe pombe. Kwa mfano, mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* alipenda kunywa pombe. Jambo hili linajitokeza wazi mwandishi anaposema kwamba;

> ……alikusudia kwenda kujifurahisha kidogo ili asahau msiba alioupata….Rosa aliingia “bar” moja iitwayo “Green Bar”. Humo ndani aliona mengi: ujanja wa wanawake na ujinga wa wanaume; unyonyaji wa wanawake

> na unyonywaji wa wanaume … Hapo alikaa akinywa chupa yake ya 'Kilimanjaro' kwa raha … (uk 42).

Kwa mintarafu ya kifungu hiki, maneno "asahau msiba alioupata" yanarejelea kuavya mimba kwa Rosa. Aliamua kunywa pombe ili awache kufikiria mambo yote mabaya aliyokuwa amefanya. Ujanja na ujinga anaozungumzia mwandishi ni kwamba wanawake hujifanya kuwapenda wanaume wakiwa na nia ya kununuliwa pombe ilhali wanaume hupumbazwa na wanawake na kutumia pesa zao nyingi kuwanunulia pombe. Mtunzi anawaita wanawake wanyonyaji kwa sababu wanategemea kupata pombe ya bure kutoka kwa wanaume. Wanaume nao anawaita wanyonywaji kwa sababu hawaoni kama wanatumiwa vibaya na wanawake. Wakati mwingine Rosa alikunywa pombe ili aweze kujisahaulisha matatizo yake. Unywaji wa pombe haukuwa suluhisho kama Rosa alivyodhani kwani baada ya pombe kumwisha, angerudiwa na fahamu zake na hivyo basi kuendelea kusumbuka moyoni. Kwa sababu ya ulevi, Rosa anaumizwa na sehemu zingine za mwili wake kulemazwa. Anapoenda kwa mwalimu mkuu, mke wa mwalimu mkuu anagundua kuwa Rosa alikuwa akishiriki mapenzi na mumewe. Hapo ndipo mkewe mwalimu mkuu anaamua kupasua mlango kwa shoka. Mlango ulipoharibika, mkewe mwalimu aliingia na shoka lake mkononi. Alitaka kumgonga Rosa kichwani, lakini mwalimu alilidaka lile shoka. Mwalimu alimwona mkewe akitema sikio la Rosa. Rosa alikuwa ameumizwa na mke wa mwalimu. Kwa bahati nzuri mwalimu alimtoa mke wake juu ya Rosa. Mkewe mwalimu alipokosa fimbo ya kumchapia Rosa, alichukia redio na kumgonga nayo mgongoni hadi akamwangusha chini. Rosa tayari alikuwa amebakishiwa sikio moja na mke wa mwalimu. Hii ni kwa sababu lingine lote lilikuwa limekatwana kutupwa chini. Baada ya kupona, aliamua kuwa kitambaa hakingemtoka kichwani mwake siku zote.

Rosa hakuogopa kunywa pombe mbele ya dadake mdogo Flora. Ilikuwa ni kama desturi yao. Hata Flora alikuwa ameanza kunywa pombe. Tunaambiwa kuwa;

> ….Flora alikunywa lakini kwa kiasi tu…Rosa alikunywa kwa pupa. Alikuwa akijikumbusha maisha ya zamani. Zamani aliweza kunywa chupa saba za bia. Zamani mvinyo ulikuwa haumleweshi sana. Chupa ya kwanza ilipokwisha, Charles alileta ya pili. Hii chupa ya pili ilimalizwa karibu na Rosa peke yake. Charles alimwacha mchumba wake anywe (Uk. 84)

Kwa mujibu wa unukuzi huu, Charles alimnywesha Rosa pombe nyingi kwa sababu alikuwa akitaka kuhakikisha kama kweli Rosa alikuwa bikira. Rosa baada ya kuchoka na maisha ya ukahaba, aliamua kutulia ili apate mchumba wa kumwoa. Alianza kudanganya kuwa alikuwa

bikira na kwamba hangefanya mapenzi kabla ya kufunga ndoa. Charles alikuwa ameamua kumwoa lakini akajuzwa na marafiki zake kuwa Rosa hakuwa bikira na ndiposa Charles akamnywesha mvinyo apate fursa ya kuhahakikisha mwenyewe kama Rosa alikuwa au hakuwa bikira.

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* unywaji wa pombe ni jambo la kawaida lakini Rehema hakuwa amejiingiza katika suala hili. Hii ni kwa sababu alijiona kila wakati yumo katika msokotano na mkondo uliotaka kumvuta. Chiku, Ruzuna na Kidawa walimnasihi aonje kidogo ili aone raha ya dunia. Rehema alijua kuwa ilimpasa asisogee karibu na vitu vile. Wasichana hawa walikunywa pombe kwa ajili ya kujifurahisha tu. Hili linadhihirika wazi wakati Rehema anaambiwa na wenzake aonje kidogo ili aone raha. Mtunzi anataka kusema kwamba ulevi wakati mwingine huchochewa na marafiki na kwamba watu hunywa kwa ajili ya kujifurahisha tu. Mwanzoni Rehema alikuwa na msimamo mkali kuhusu unywaji wa pombe yaani, hakutaka kuikaribia hata kidogo. Siku moja Rehema aliporejea nyumbani alimkuta mwanamume asiyemjua akimgoja kitandani, chupa ya ulevi mkononi akitaka awe mshirika wake. Rehema alishikwa na hofu hadi akamwendea Chiku kumshtaki. Rehema alidhani Chiku angemwokoa lakini hili halikuwezekana kwani Chiku alikuwa gwiji katika suala la uhusiano na wanaume.

**iv) Wizi**

Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, wizi unajitokeza mara kadhaa. Mhusika Kalia alichapwa na baba yake kwa kuokota noti ya shilingi hamsini. Babake Kalia anataka kumfunza Kalia tabia nzuri lakini anatumia mbinu mbaya kwa sababu anangoja hadi tendo baya litendeke ndio amchape Kalia. Wizi huu ulimghadhabisha na alikashifu kitendo hiki cha Kalia. Noti ya shilingi hamsini aliyookota Kalia ilikuwa imesukumwa mpaka chumba cha maongezi na upepo uliokuwa ukivuma. Kalia alipoiona aliiokota na kuitia mfukoni mwake na ajabu ni kwamba mahali alikopeleka pesa hizo hakuna aliyefahamu kwa sababu alikataa kusema. Tegemea mama mzee, ndiye alijua pesa alizoiba Kalia, zilienda wapi. Hii ni kwa sababu anashiriki mapenzi na Kalia. Shughuli hii inamfanya Kalia kuiba pesa za ndugu yake Kazimoto ili ampe na kumfurahisha Tegemea. Kazimoto anapoamua kumfuata nyuma kisirisiri usiku mmoja, anasikia Kalia akimwambia Tegemea kwamba;

> …..zile shilingi hamsini nilizoleta siku moja, nilipigwa na baba yangu alipotambua.Halafu tena zile shilingi hamsini zingine nilizopewa na kaka yangu nikakuletea zitakuwa za mwisho. Siku hizi ni vigumu kupata pesa (uk 108-109)

Unukuzi huu unaweka mambo wazi kuwa kitendo cha wizi kilikuwa kimefanyika zaidi ya mara moja. Watoto wa aila moja walikuwa wakiwasiliana vizuri bila kujali umri wao. Watotowadogo hawakuwaogopa ndugu zao wakubwa. Kalia na ndugu zake wadogo walizoea kuingia katika chumba cha kulala cha kaka yao mkubwa bila masharti yoyote. Huku kuingia bila vikwazo kunampa Kalia fursa ya kuanza wizi. Kalia anaingia na kuiba shilingi mia mbili lakini anasahau kulifunga sanduku. Siku moja Kazimoto alishtukia sanduku lake limefunguliwa na alipotazama ndani aliona kwamba shilingi zake zilikuwa zimebaki mia moja tu. Mia mbili zilikuwa zimechukuliwa. Alipomwuliza Kalia, alikana kwamba si yeye. Wizi huu ulimfanya Kalia asilale nyumbani kwao kwa muda. Kazimoto alivumbua baada ya siku mbili kwamba Kalia alikuwa halali chumbani mwake wakati wa usiku. Mwandishi anaashiria kuwa ingawa kuna watoto ambao huonekana kuwa wabaya machoni pa watu, ubaya huo husababishwa na watu wazima. Mhusika Kalia alilazimika kuiba ili amlipe Tegemea baada ya kushiriki mapenzi naye. Pengine kama Tegemea hangekuwako, Kalia hangekuwa mwizi au pengine kama Tegemea hangekuwa kahaba, Kalia naye hangeiba.

Katika riwaya ya *Kiu* kuna wizi ambao haujidhihirishi kabisa kuwa ni wizi wakati Idi anapopanga kumtumia Bahati kupata mali ya mzee Mwinyi. Bahati anapotishia kuwa urafiki wao ulivunjika zamani wakati alipomtaka afanye mapenzi na yule mzee mchimvi. Idi hamwambii kuwa ni wizi wanautekeleza kwa sababu hasemi moja kwa moja kwani anamjibu hivi;

> … lakini nimekueleza kuwa huu ni mpango tu. Ukiukubali tutatajirika mimi na wewe na kisha tuoane, tustarehe. Kwa nini tuache mifedha ya mzee yule? Wewe huoni ilivyo rahisi kuipata? (uk 14).

Maneno "ukiukubali tutatajirika" yanamaanisha Bahati akiitikia kujifanya kuwa anampenda Mwinyi na kushiriki mapenzi naye, watapata pesa zake ili wajinufaishe wao wenyewe. Huu ni wizi kwa sababu Idi alikuwa na nia mbaya hata kama alitumia maneno matamu kuzipata zile pesa kutoka kwa Mwinyi. Mwandishi alikusudia kuwapasha habari wasomaji kuwa kuna uwezekano wa watu wazima na matajiri kuwatumia vibaya wasichana wadogo kujitajirisha. Katika ulimwengu wa sasa tumeshuhudia watu wakiwatumia watoto kujitajirisha. Kwa mfano, Mhusika Maimuna katika riwaya ya *Utengano* (Mohamed, 1981) alipotoroka kwao,

Mhusika Jane alimuuza kwa wanaume na yeye ndiye alikuwa akilipwa. Huu pia ulikuwa wizi kwa sababu aliwauza watoto wa wenyewe kutumika kimapenzi na kujinufaisha yeye mwenyewe.

### 4.3.2 Kuwalea Wadogo Zao

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* baadaya Zakaria, Regina na Rosa kufariki, Flora ndiye anachukua usukani wa kuwalea wadogo zake. Flora aliwaomba masista waliokuwa wakikaa Kagunguli wamsaidie kutunza dada zake kwa muda wa miaka miwili. Baada ya siku moja Honarata, Stella, Sperantia na Emmanuel walipelekwa huko. Kuwajibika kwa Flora kulimfanya mumewe ampende zaidi na akamwahidi kuwa baada ya muda wa miaka miwili ya kazi, angemsaidia kuwatunza wadogo zake. Flora analazimika kuwalea wadogo zake kwa sababu baada ya vifo vya wazazi wao, jamaa zao walirithi kila kitu na kumwachia Flora mzigo mkubwa wa kuwalea wadogo zake bila pesa zozote. Hapa, Flora alinyimwa haki zake kwani hakuwa tayari kwa jukumu hili. Ni bayana kuwa serikali haikuwa ikitilia maanani suala la haki za watoto kwani watoto kama hawa walipobaki mayatima, serikali ndiyo ingewajibika na kuanza kuwatunza. Uchunguzi huu ulitambua kwamba wanajamii katika riwaya ya *Rosa Mistika* walikuwa na ubinafsi wa kupindukia. Vilevile, Mhusika Flora alikuwa na utu kwa sababu aliwajali wadogo zake baada ya wazazi wao kuaga dunia.

### 4.3.3 Kusoma

Watoto katika riwaya ya *Rosa Mistika* walipelekwa shule ingawaje si wazazi wote walioona umuhimu wa masomo.Rosa alikuwa mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu-mwenye haya. Alikuwa na miaka kumi na mitanoakiwa katika darasa la saba. Watoto walijitolea kusoma lakini wazazi wengine kama vile Zakaria hawakujali suala la masoma sana kwa sababu tunaelezwa kuwa;

> Jirani zake walisema alijali pombe kuliko watoto; alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia watoto ada ya shule…… (uk 6).

Kufuatana na maneno “hajatoa hata chapa kuwalipia ada ya shule” ni dhihirisho kamili kuwa watoto walikuwa wakienda shule ingawa baba yao hakujishughulisha na masomo yao. Zakaria alifungwa na pombe kiasi cha kutotoa pesa hata kidogo kwa ajili ya masomo ya watoto wake. Flora dadake Rosa naye alisoma hadi darasa la kumi na mbili ingawa hakupita. Huenda ikawa kuanguka kwake mtihani kulitokana na dhana kuwa baba yao hakuwaonyesha umuhimu wa masomo. Flora anaposema kuwa wanalindwa sana katika shule yao, ni hakikisho kuwa alikuwa mwanafunzi katika shule ya wasichana ya Mwanza.Wanafunzi kama

Rosa na wengine hawakutilia masomo mengine maanani. Rosa alipokuwa akifanya mtihani wa Historia hakuweza kujibu swali lolote. Mwishowe alichagua maswali manne. Alianza kuandika kitu fulani kama historia. Rosa aliona masomo yote magumu isipokuwa Kiswahili. Majibu ya mtihani yalipokuja, Rosa alijikuta ameshinda masomo matatu –Swahili, 'Needle work' na 'English.' Rosa alifurahi kuona amewazidi wengine waliokuwa pale shuleni muda wote wa masomo. Hatimaye Rosa alichaguliwa kwenda Morogoro TTC. Angelitilia masomo maanani pengine angelikuwa mwanafunzi bora katika mtihani huo. Watoto wengine hawakumaliza shule hata kama walipelekwa huko. Rosa alipofunga shule aligundua kutoka kwa Stella kuwa dadake mmoja kwa jina Honarata alikuwa amewacha kuhudhuria shule. Mwandishi anaposema kuwa Honarata amekwishashindwa, anamaanisha kuwa aliacha kwenda shule. Hii ni ishara kuwa watoto walikuwa wakienda shule lakini hawakuelimishwa na kuonyeshwa umuhimu wa masomo. Wangeonyeshwa, watoto kama Honarata hangewacha shule katika umri wake mdogo. Mtunzi anataka jamii iweze kutambua umuhimu wa masomo kwa watoto wao. Aidha, katika riwaya ya *Kichwa Maji* watoto wanasoma lakini si wote wanaofaulu. Wengine wanawachia njiani kwa sababu moja au nyingine. Rukia analazimika kuwacha shule kwa sababu ya kutiwa mimba na Manase. Hili ni jambo linalomhuzunisha sana. Kutokana na maneno anayoyaandika yeye mwenyewe katika barua aliyomtumia Kazimoto, anamwambia kuwa maisha yake yalikuwa tayari yameharibika, na alikuwa amekwisha acha.

Kulingana na maneno yaliyoandikwa na Rukia, ni wazi kuwa Rukia alikuwa na hamu ya kusoma lakini Manase akamkatizia masomo kwa kumpachika mimba. Mtunzi anataka watu wawe makini wakati wanapowawachia watu watoto wao, wanastahili kwanza wawafahamuni watu wa aina gani. Hata hivyo, kuna wale waliofaulu katika masomo yao. Manase na Kazimoto walisoma hadi chuo kikuu na wakafanikiwa kupata kazi.

Katika *Nyota ya Rehema*, Salma na Samir ndugu zake Rehema wa kambo walipelekwa shule za bei ghali. Bwana Fuad mwenyewe alimhakikishia mkewe Bi Adila kuwa wangemtia Salma'Royal media'. Baadaye Samir alienda Ulaya kusoma naye Salma alikuwa mjini akisoma. Wazazi wa Salma na Samir walikuwa na uwezo wa kuwapeleka shule nzuri. Kama ilivyo siku hizi, watu wenye uwezo kifedha huwapeleka watoto wao katika shule za bei ghali kama vile shule za kibinafsi. Hata hivyo, huenda ikawa hawakuwa werevu vile, licha ya kupelekwa shule za kifahari. Hii ni kwa sababu Salma anapokuwa mtu mzima hakuajiriwa kufanya kazi yoyote, alikuwa mke nyumbani tu aliyemtegemea mumewe kwa kila kitu.

### 4.3.4 Kuteka Maji

Mhusika Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* alipotoroka kwao na kwenda mjini, alikutana na watoto wakichota maji. Kuna kijana aliyekuwa akimimina ndoo ya maji upesi upesi katika mtungi wake. Alikuwa akitumia mtungi uliokuwa ukifuja kwani alikuwa akichungulia ndooni kuhakikisha kuwa udongo ulikuwa ungali ufani. Mazingira walimokuwa hayakuridhisha maanake tunaelezwa kwamba;

> Rehema alisogea ukingoni na kuchungulia. Ndani ya kisima mlikuwa kiza hadi jicho lilipofika; hamkuonekana kitu isipokuwa mwani ulitambaliwa na majani mapana. (uk.40)

Kuteka maji katika muktadha huu, ni pujufu kwa watoto kwa sababu kisima kilikuwa kirefu mno na endapo wangeteleza na kuanguka mle ndani, wangeumia au hata kupoteza maisha yao. Hapa mwandishi ametuchorea taswira hii kuashiria umaskini katika jamii husika. Hakuna mtu mzima aliyefikiria kununua ndoo mpya. Utafiti huu ulitambua kuwa wakati mwingi watoto ndio walikuwa wakiteka maji wakilinganishwana watu wazima.

### 4.3.5Jedwali 2: Muhtasari wa Majukumu Yanayotekelezwa na Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Jedwali hili linaonyesha muhtasari wa majukumu yanayotekelezwa na wahusika watoto katika kazi zilizoshughulikiwa. Linaonyesha aina za majukumu, majina ya riwaya, kurasa na majina ya wahusika.

| **Majukumu** | **Riwaya** | **Ukurasa** | **Jina la Mhusika** |
|---|---|---|---|
| Ukahaba | Kichwa Maji<br>Rosa Mistika<br>Nyota ya Rehema<br>Kiu | 22,80,81,123,124,129, 144,145<br>4,45,47,48,49,53,78,79 90,91<br>54,55,57,59<br>14,15, 16,32 | Rukia Kazimoto, Kalia Vumilia<br>Rosa<br>Rehema, Ruzuna, Chiku, Kidawa<br>Bahati |
| Kupika na kuuza pombe | Rosa mistika | 11, 19 | Flora, Rosa, Honarata, Sperantia |
| Kuwalea wadogo zao | Rosa Mistika | 96 | Flora |
| Unywaji wa pombe | Rosa Mistika | 42,54,55,59 | Rosa, Flora |
| Wizi | Kichwa Maji<br>Kiu | 104,107,108,110<br>14 | Kalia<br>Idi, Bahati |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kusoma | Rosa Mistika<br><br>Kichwa Maji<br>Nyota ya Rehema | 6,37,63<br><br>26<br>3 | Rosa, Flora, Sperantia, Charles<br>Rukia, Kazimoto, Manase<br>Salma, Samir |

Jedwali B linaonyesha majukumu mbalimbali ambayo wahusika watoto walihusishwa nayo. Baadhi yao walitekeleza majukumu hayo. Jukumu la ukahaba lilitekelezwa katika riwaya zote nne zilizochunguzwa. Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, wahusika waliotekeleza jukumu hili ni Rukia, Kazimoto, Kaliana Vumilia. Katika riwaya ya *Rosa Mistika* mhusika Rosa ndiye alijihusisha na ukahaba. Katika riwaya *ya Nyota ya Rehema*, wahusika Rehema, Ruzuna, Chiku na Kidawa walitekeleza jukumu la ukahaba. Vilevile, katika riwaya ya *Kiu,* Bahati alijihusisha na ukahaba.

Kuhusiana na upishi na uuzaji wa pombe, riwaya moja tu kati ya riwaya nne zilizochunguzwa, ilionyesha kuwa wahusika watoto walihusishwa katika shughuli hii. Hii ni riwaya ya *Rosa Misitika.* Wahusika waliojishughulisha na upishi nauuzaji wa pombe ni Flora, Rosa, Honarata na Sperantia.

Jukumu la watoto kuwalea wadogo zao nalo lilijitokeza katika riwaya moja kati ya zile nne zilizochunguzwa. Riwaya hii ni *Rosa Misitika*. Wahusika waliojiingiza katika unywaji wa pombe ni Rosa na Flora. Suala la watoto na vijana kuiba liliweza kujitokeza katika riwaya mbili ambazo ni *Kichwa Maji* na *Kiu*. Mhusika Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji,* Idi na Bahati katika riwaya ya *Kiu* walitekeleza wizi mara si moja.

Wahusika wengi walikuwa wakisoma hata kama wengine hawakutilia masomo yao maanani. Riwaya tatu kati ya nne zilizochunguzwa ziliyathibitisha haya. Katika riwaya ya *RosaMisitika*, wahusika waliojihusisha na masomo ni Rosa, Flora, Sperantia na Charles. Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, wahusika Rukia, Kazimoto na Manase walikuwa wakisoma ingawaje si wote waliofaulu. Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, wahusika Salma na Samir walijishughulisha na suala la kusoma.

Ni muhimu kutaja kwamba, katika riwaya zilizochunguzwa, ukahaba kati ya watu wazima na wahusika watoto ulikita mizizi katika jamii husika. Aidha, hiki ndicho kipengele kilichojitokeza zaidi kuliko vipengele vyote vilivyochunguzwa.

### 4.4 Mielekeo ya Watu Wazima na Matajiri kwa Watoto

Mwelekeo ni mtazamo au mawazo waliyo nayo watu wazima. Kwa mintarafu ya madhumuni ya tatu ya utafiti huu, mielekeo ya watu wazima na matajiri kwa watoto ilichunguzwa. Ili kutambua mielekeo hii, sentensi, msamiati na vifungu vya maneno vilichunguzwa na kuchanganuliwa katika riwaya husika.

#### 4.4.1 Mielekeo ya Watu Wazima Katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi

**i) *Rosa Mistika***

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* Zakaria alikashifiwa na jirani zake. Walisema kuwa alijali pombe kuliko watoto wake. Kulingana na maneno ya majirani zake, Zakaria hakutilia maanani elimu ya watoto wake. Aliona kama ni hasara kuwalipia watoto wake karo, na hivyo basi, akachagua kutumia pesa zake kwa pombe. Majirani wanaonekana kuwajali watoto wa Zakaria kuliko yeye mwenyewe. Ubaya wa majirani hawa ni kwamba walikuwa wakimsengenya Zakaria badala ya kumwambia. Hapa kulikuwa na mchanganyiko wa mielekeo ya watu wazima kwa sababu majirani walimtaka Zakaria awajibike ilhali Zakaria hakutaka kuwajibika. Kwa hivyo, majirani walikuwa na mielekeo chanya naye Zakaria alikuwa na mielekeo hasi kwa watoto.

Rosa alipokuwa katika darasa la tano aliandikiwa barua na Charles lakini Zakaria hakufurahishwa naye. Alitumia lugha chafu kama inavyodhihirika katika maneno yaliyotoka kinywani mwake. Alimuuliza kama alikuwa akitaka kumletea umalaya kama mama yake.Kutokana na matamshi haya, ni wazi kuwa Zakaria alikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Hakuonyesha heshima mbele ya mtoto wake. Vilevile, hakufikiria athari ambazo angemsababishia mtoto wake, kumwambia kuwa alikuwa malaya kama mama yake. Tusi hili lingemfanya Rosa akose kumwamini na kumheshimu mama yake. Mtunzi anataka wazazi wawaheshimu watoto licha ya umri wao mdogo. Kinyume na Zakaria, Regina aliwapenda watoto wake kwa sababu walipofanya vizuri aliwasifu. Kwa mfano, Flora alipopika ugali vizuri, mamake alimsifu. Lakini walipokosa hakuchelea kuwarekebisha. Hii inaonyesha kuwa yeye aliwatakia watoto wake maisha mazuri. Alifanya hivi kwa sababu alielewa kuwa mti hukunjwa ukiwa mchanga. Katika malezi yake, Regina aliwaonya watoto wake kuhusu mambo mengi kama vile, uongo, uvivu na kutowaheshimu wakubwa wao.

Zakaria hakuwapenda watoto wake hasa wale wa kike kwa sababu kila mara, alimtukana mkewe akimwitamshenzi aliyemzalia wasichana. Kwake yeye aliona kama ni taabu kubwa.

Kwa mintarafu ya maneno yake, Zakaria anapomtukana mkewe na kumwita mshenzi anayemzalia wasichana ni dhihirisho kuwa hakuwapenda watoto wake kwa sababu ya jinsia yao ya kike. Aliposema kuwa bibi yake alimletea taabu bure tu, alimaanisha kuwa watoto wasichana hawakuwa na faida zozote kwake. Ni hatia kwa mtu yeyote kuwachukia watoto kwa misingi ya jinsia zao. Zakaria alistahili aelewe kuwa jinsia ya mtoto yeyote yule hutegemea chembechembe za uzazi za mzazi wa kiume.

Rosa alipata mimba akiwa shuleni na kuiavya. Walimu waliketi na kuamua afukuzwe.Mwalimu mkuu alitumia fursa hiyokumtumia Rosa alivyotaka. Kwa bahati mbaya au nzuri, mke wa mwalimu mkuu anawafumania na kughadhabishwa mno na kitendo chao. Ghadhabu zake zinadhihirishwa na maneno anayoyatamka kutoka kinywani mwake anapomuuliza kama alikuwa akitaka kumletea umalaya. Neno “malaya” linaashiria kuwa Rosa sasa alikuwa na tabia mbaya ya kuwanyakua mabwana za watu. Mke wa mwalimu alikosea kwa kumtukana Rosa, maanake Rosa hakuenda kumtafuta mwalimu mkuu, bali mwalimu ndiye alitumia cheo chake kumdanganya Rosa. Rosa aliitwamalaya na watu kadhaa kama vile baba yake, mke wa mwalimu mkuu na watu wengine. Aidha, wahusika watoto wengine katika riwaya zilizochunguzwa kama vile mhusika Rukia katika riwaya ya *Kichwa Maji*, Bahati katika riwaya ya *Kiu* na Flora katika riwaya ya *Rosa Mistika*, waliitwa malaya. Ni jukumu la kila mtu mzima kuwapa watoto mwelekeo wanaostahili kuufuata maishani. Idadi kubwa ya watu wazima haikuchukua muda wao kuwaelimisha watoto kuhusiana na athari za kushiriki mapenzi na watu wazima kabla ya kuoa na kuolewa. Hii inadhihirisha wazi kwamba baadhi ya watu wazima walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Waandishi wa riwaya husika walikusudia kuwapasha wasomaji ujumbe kuwa, matusi hayasaidii kurekebisha tabia.

Uhusiano kati ya wazazi na watoto katika baadhi ya aila haukuwa mzuri. Mfano mzuri ni uhusiano kati ya Rosa na baba yakeZakaria. Kadiri Rosa alivyozidi kukua, babake alizidi kumwona mbaya. Anafikia hata kiwango cha kumkana Rosa kuwa hakuwa mwanawe. Kumkana huku, ni dhihirisho kuwa Zakaria alikuwa amechoshwa na vitendo vyaRosa. Hii inaonyesha kuwa Zakaria hakumpenda Rosa. Alimwambia hivyo mbele ya rafiki yake wa kiume aliyekuwa amekuja kumchukua Rosa. Pengine kama baba mzazi angezungumza na kumkanya kuhusu tabia zake mbaya, Rosa angekuwa mtoto mzuri. Kumkana pamoja na matusi ni ishara ya kuwa babake alikuwa na mielekeo hasi kwa mtoto Rosa na dada zake pia. Jambo hili lilimchochea Rosa kumjibu babake kwa kumwambia kuwa hata yeye (Zakaria)

hangekuwa baba yake. Mtunzi anatumia uhasama huu kati ya Zakaria na bintiye kupitisha ujumbe kwamba ikiwa mtu anataka kuheshimiwa na watoto wake ni lazima kwanza ajiheshimu.

**ii) *Kichwa Maji***

Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, mielekeo ya watu wazima vilevile ilijitokeza kupitia kwa msamiati, sentensi na vifungu vya maneno. Mhusika Kalia anaitwa 'mwehu'. Kwa mintarafuya neno 'mwehu', ni wazi kuwa watu wazima waliona kama Kalia ni mwendawazimu. Jina hili linatokana na tabia zake ambazo zilifanana na tabia za mwendawazimu. Ukweli ni kwamba hakuwa mwehu ila tu tabia zake zilibadilika kutokana na hali ya jamii. Yaani ni jamii ambayo watu wengi walijihusisha na ukahaba. Aidha Kalia anaitwa "nunda mla watu". Mtunzi anakusudia kupitisha ujumbe kuwa Kalia alikuwa hatari kwa maisha ya binadamu wenzake, na hivyo basi, wanajamii walistahili kujihadhari naye. Majina haya yote yanaonyesha kuwa watu wazima walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto kwa sababu uozo wa tabia za Kalia ulichangiwa sana na mazingira alimoishi.

Mhusika Kamata katika riwaya ya *Kichwa Maji* anajaribu kuwaza kwa sauti anaposema kuwa hajui wasichana wanafikiri nini. Kwa mintarafu ya sentensi hii, Kamata alikuwa akimrejelea Rukia dadake Kazimoto. Alikuwa anajaribu kumlaumu Rukia kwa kupata mimba akiwa katika darasa la tisa au kidato cha kwanza. Kamata alimlaumu Rukia kwa kumkosea shukrani kakake Kazimoto ambaye alikuwa akimlipia karo. Kamata hakuelewa ya kwamba Manase alitumia nguvu kumpachika Rukia mimba. Mtunzi anataka tuamini kuwa wakati mwingine watu wazima huwanyoshea watoto kidole cha lawama bila kutafuta chanzo cha makosa yao. Hivyo basi anataka watu wasiwe wepesi wa kutoa lawama kwa kosa lolote lile kabla ya kufanya uchunguzi.

Suala linaloibuka hapa ni kuwa, baadhi ya watu wazima hawakufurahishwa na matendo ya vijana hasa wavulana kama anavyofichua mamake Kazimoto anaposema kuwa kulikuwa na ugonjwa ulioletwa na vijana na kwamba ungewamaliza kina mama wenye mabinti. Kufuatana na sentensi hii, ugonjwa anaouzungumzia mamake Kazimoto ni suala la wasichana kupata mimba za mapema. Alisema kuwa ugonjwa huo uliletwa na vijana kumaanisha kuwa wao ndio waliwapachika wasichana mimba, na hatimaye zikawa kama ugonjwa kwa sababu Rukia alisusia chakula na afya yake ilizoroteka sana. Anaposema kuwa ugonjwa ungewamaliza kina mama wenye mabinti anamaanisha kuwa akina mama vilevile

waliathirika. Hii ni kwa sababu walitumia wakati mwingi kulia na binti zao waliokuwa wameshika mimba. Wazazi hapa walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto kwa sababu waliwaona kama wauaji - yaani ndio wangesababisha vifo vyao. Mtunzi anapitisha ujumbe kuwa watu wazima hawastahili kulegea kuwaelekeza watoto wao, ili wasije kuwalaumu baadaye kama alivyofanya mamake Rukia.

Mhusika Kalia alipouawa, Kabenga anaenda kuwajuza Kazimoto na babake. Anatamka kwa midomo yake kuwa watu walikuwa wameuona mwili wa Kalia lakini hakuna mtu angependa kujiweka hatarini. Katika kifungu hiki cha maneno, Kabenga anazungumzia kuhusu mwili wa Kalia ulioonekana ukielea kwenye maji. Hatari anayozungumzia Kabenga ni kwamba hakuna mtu ambaye angeenda kuutoa pale kwani kitendo cha ubakaji alichokitenda hadi akauawa kilionekana kuwa kibaya mno. Kwa hivyo, kwenda kuutoa mwili wa Kalia majini kulikuwa tishio kwa wanajamii kwani waliogopa kudhaniwa kuwa washirika wa Kalia. Hapa, watu wazima wanaonyesha wazi kuwa mielekeo yao dhidi ya watoto ni hasi kwa sababu hata waliogopa kutoa mwili wa Kalia majini. Hili ni kosa maanake, licha ya Kalia kupigwa hadi kifo kwa ajili ya uovu wake, bado alikuwa ni mtoto. Kuongeza na hayo, alikuwa maiti na hivyo basi kuendelea kumchukia hakungemsaidia kwa chochote.

### 4.4.2 Mielekeo ya Watu Wazima Katika Riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed

**i)** ***Nyota ya Rehema***

Katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, mielekeo ya watu wazima na matajiri inajitokeza katika kifungu cha maneno kifuatacho;

> Tumbo linanikeketa nikiliona lile toto lake la haramu likicheza na mwanangu Salma. (uk. 2)

Kwa mintarafu ya kifungu hiki cha maneno, Bibi Adila hakumpenda Rehema hata kidogo. Maneno “toto lake la haramu” yanamrejelea Rehema. Adila alimwambia mumewe Fuad kuwa alipomwona Rehema tumbo lake lilimkeketa. Anamwita Rehema mtoto haramu kwa sababu rangi yake nyeusi ilikuwa tofauti na ya wazazi wake hasa Fuad. Adila alikuwa akitafuta njia za kumtenganisha Rehema na babake. Maneno “toto haramu” yanaonyesha kuwa Bibi Adila alikuwa na mielekeo hasi kwa Rehema. Si yeye peke yake, hata Fuad babake Rehema. Hili linadhihirika wazi anapomwambia Aziza kuwa Rehema alikuwa mtoto wake peke yake. Aidha, alikuwa na hasira kwa sababu hakukawia mle hospitalini.

Kulingana na hatua aliyoichukua Bwana Fuad, akiwa hospitalini wakati mke wake Aziza alipojifungua, ni wazi kuwa Fuad aliamini kuwa hakuwa baba ya Rehema. Kwake yeye

aliamini kuwa Aziza hakuwa mwaminifu kwake. Alimwona Rehema kama mwanaharamu. Rangi nyeusi ya mtoto Rehema ilimkasirisha kwa sababu baada ya kutamka manenohayo alitoka na kwenda zake. Ni wazi kuwa hakuna sehemu ya mwili wa Rehema iliyomfurahisha Bwana Fuad. Hii ni kwa sababu tunaelezwa ya kwamba Rehema alikuwa;

> ….Kiduchu, kidhofu, kihadharani, chenye nywele mbunyembunye, zilizosokotana, pua fupi iliyoshikana na ngozi ya uso na midomo yenye maini. Kilikuwa tofauti na wazazi wake (uk 15).

Kwa mujibu wa kifungu hiki cha maneno, ni wazi kwamba Bwana Fuad alijaribu kadiri ya uwezo wake kumuepuka Rehema. Kwa ujumla, rangi nyeusi ya Rehema iliyafanya maisha yake yote yaharibike. Kilichomfanya Fuad kumshuku Rehema ni kwamba alikuwa mweusi ilhali yeye kama babake na mamake walikuwa weupe. Hii inaonyesha kuwa Fuad alikuwa na mielekeo hasi kwa Rehema. Mwandishi ametumia hali hii ya mhusika Rehema na babake bwana Fuad, kuonyesha jinsi jamii hii ilivyowachukia wanaharamu.

Si watu wote wazima waliokuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Bi Kiza shogake marehemu mama ya Rehema, alimtunza na kumwonyesha Rehema huruma. Anamhimiza Rehema kwenda kudai haki yake. Bi Kiza ni mtu mmoja kati ya watu wengi aliyekuwa na mielekeo chanya kwa mtoto Rehema. Mhusika Kidawa anaozwa akiwa mdogo kama anavyokiri yeye mwenyewe anaposema kuwa, alipewa mume kabla ya kuota chuchu. Hii inaonyesha kuwa wazazi wa Kidawa walimlazimisha kuolewa akiwa bado mdogo. Ni wazi kuwa watu wazima hawakuwapa watoto fursa ya kujiamulia mambo. Isitoshe, Kidawa hakuwa ametoshea kuolewa kwa sababu hakuwa amekomaa. Hili linadhihirika wazi kutokana na maneno aliyosema yeye mwenyewe kuwa wakati alipokuwa akiozwa hakuwa ameota maziwa. Uamuzi aliofanyiwa Kidawa na wazazi wake ni dhahiri shahiri kuwa watu wazima katika jamii hii walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Aidha, mhusika Rehema katika riwaya hii anakumbana na tatizo sawia na hili. Kwa sababu ya shida alizokuwa nazo, Rehema alitafuta kazi ambayo ingemwezesha kujikimu kimaisha. Bwana Mansuri alitaka sana Rehema aajiriwe kama mlezi kwa mtoto wake lakini mkewe Rozi hakuwa tayari. Hili ni kutokana na matamshi yake anaposema kuwa;

> ….Mimi nilitaka mtu mzima anayejua kulea si mtoto mdogo asiyemaliza kulelewa…Ah, Bwana Mansuri, nikitafuta wa kunipokea ulezi siyo wa kuniongezea(uk. 48).

Unukuzi huu unathibitisha kuwa Rozi mkewe Mansuri anapomwona Rehema, anamwona kweli ni mtoto na ndio maana anasema kuwa anataka mtu mzima. Bwana Mansuri alijua na

aliona kweli kuwa Rehema alikuwa mtoto lakini alisisitiza kuwa aajiriwe kwaajili ya kumchunga mtoto wao. Rozi kwa upande wake aliona kuwa Rehema hangeweza kutekeleza majukumu yote ya nyumbani kwa sababu ya umri wake mdogo. Rozi alikuwa na mielekeo chanya hapa kwa sababu alielewa kuwa watoto wadogo kama Rehema hawangeweza kazi ngumu za nyumbani. Mansuri naye licha ya kuelewa kuwa Rehema alikuwa mtoto, alihakikisha kijakazi huyu ameajiriwa. Kwa hivyo, alikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Ujumbe tunaoupata kutokana na hii sentensi ni kwamba binadamu wa kawaida ana ubaya na uzuri wake. Hii ni kwa sababu hata kama wakati mwingine Rozi alikuwa mkali, hapa alionyesha jambo la busara kukataa mhusika mtoto aajiriwe kumfanyia kazi za nyumbani.

Rehema alipoajiriwa, muda mwingi walikuwa pale nyumbani na Bwana Mansuri mkewe akiwa kazini. Mansuri alianza kumnunulia zawadi kama vile kanzu. Alifanya hivi kama njia ya kumhadaa Rehema. Hili linajitokeza wazi wakati Rehema anavua kanzu mpya aliyokuwa amenunuliwa na Bwana Mansuri. Kutokana na hali hii, Mansuri anapomwambia Rehema kuwa angeendelea kuvaa kanzu mpya aliyomnunulia, inaonyesha kuwa umaskini aliokuwa nao Rehema, ungemchochea amkubali pindi tu baada ya kuona kanzu ile. Hii ni ishara kuwa Bwana Mansuri aliwadunisha watoto hasa kwa misingi ya hali yao ya kiuchumi. Si Mansuri tu aliyemtamani Rehema. Kuna watu wengi waliomtamani kama inavyodhihirika katika sentensi ifuatayo:

> Hapana kati ya hao aliyekaa naye faraghani muda mfupi tu asidhihirishe uchu wake wa kinyama (uk. 90)

Sentensi hii inaweka mambo bayana kuwa watu wazima hawakuwaheshimu watoto kama wanavyostahili. Waliwataka wawe washirika wao katika suala la mapenzi. Kwa hivyo, watu wazima walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto kwa sababu waliwatumia jinsi walivyopenda.

Rehema akiwa kwa Mansuri alijishughulisha na kazi mbalimbali bila kuangalia umri wake.
Alitekeleza majukumu yote mle nyumbani mwa Rozi yakiwemo kumchunga mtoto na mumewe.Mwandishi ametuchorea taswira kuwa, Rehema alimlea mtoto wa Rozi kwa upendo kama vile mamake mzazi angemlea. Hii inamaanisha kuwa Rehema alimtunza mtoto kana kwamba alikuwa wake hadi Mansuri mumewe Rozi akafurahia kazi yake. Aidha, Rehema alitumiwa na Mansuri kama mkewe- yaani alifanya mapenzi naye alivyotaka, ndio maana mtunzi anasema kuwa alichukua mahali pa uke kwa Mansuri.Kwa hivyo, watu matajiri hapa - yaani Bwana Mansuri alikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Kwa njia nyingine mtunzi

anawaonya wanawake wawe waangalifu wakati wa kuajiri vijakazi kwa sababu huenda ni kuwapatia waume zao fursa ya kuwatumia vibaya au hata kuwaoa.

Idrisa anatumia lugha ya kuonyesha mielekeo isiyo ya kuridhisha kwa mhusika Rehema. Anamwita "darling" wakati Rehema anasumbuliwa na tatizo la shamba. Idrisa anatumia neno hili kumpumbaza Rehema. Ana mielekeo hasi kwa sababu alifikiria Rehema angehadaiwa na maneno yake. Vilevile, anamwambia waziwazi kwamba watu huwapa wake zao talaka wakati wanapotaka kuwakata urithi watoto wasiowakiri au wasiowapenda. Kulingana na sentensi hii, huu ni wakati Rehema alienda kutafuta ushauri kuhusu kupokonywa shamba lake alilopewa na babake marehemu Bwana Fuad. Idrisa anaposema "watu hufanya hivyo" anamaanisha kuwa ikiwa mtu hakubali au hampendi mtoto wake, yeye humpa talaka mamake kama walivyosisitiza kuwa Bwana Fuad alikuwa amemtaliki Bibi Aziza marehemu mamake Rehema kabla ya Rehema kuzaliwa. Sentensi hii ilidhihirisha ya kwamba watu wazima na matajiri hawakujali maisha ya watoto kwa sababu walifika hata kiwango cha kuwakana watoto wao waliowazaa wao wenyewe.

**ii)** ***Kiu***

Katika riwaya ya *Kiu*, watu wazima wana mielekeo mbalimbali kwa watoto. Mhusika Mwinyi ambaye ni mzee wa miaka sitini, alimtamani Bahati kwa muda mrefu. Hata hivyo, hakuwa na uhakika kama Bahati angemkubali kwa sababu anamuuliza Idi kama Bahati angeweza kumpenda mzee kama yeye. Idi ana mawazo tofauti kutokana jibu alilompa mzee Mwinyi. Anamwambia kuwa Bahati ni mtoto wa kimaskini na iwapo angempa pesa, angempata pasi na wasi wasiwowote. Kufuatana na kifungu hiki cha maneno, ni wazi kuwa watu wazima waliegemeahali yao ya kiuchumi kuwanyanyasa watoto wa kike. Idi anasema kuwa silaha ya kumpata Bahati ni fedha tu. Hii inaonyesha kuwa watu wazima hawakujali maisha ya baadaye ya watoto hawa. Walijua kuwa wakiwaonyesha pesa kidogo watakuwa wameteka nyara mawazo yao na hivyo basi, hawangewakataa.

Haya ni mawazo mabaya kwa sababu huyu Mwinyi alimsomesha mtoto wake (Rehema) hadi akaenda Ulaya lakini kwa sababu Bahati ni mtoto wa kimaskini anataka kufanya mapenzi naye na kumharibia maisha. Pengine Idi na Mwinyi wangetumia fedha zao kumlipia Bahati karo, wangeonyesha kuwa walijali umaskini wake. Mtunzi anataka watoto hasa wale wa kike wasihadaiwe kwa kisingizio cha umaskini. Bahati anapoonyesha ishara ya kumkataa Mwinyi, Idi anamwambia kuwa "mapenzi na starehe havipatikani kwa mikono mitupu." Idi

alipotamka maneno haya alikusudia Bahati akubali kufanya mapenzi na mzee Mwinyi ili yeye apate pesa kutoka kwa Mwinyi. Ukweli wa mambo ni kwamba Idi ndiye alikuwa akitaka pesa ila tu alikuwa akilitumia jina la Bahati kuzipata. Watu wazima na matajiri hapa walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto.

# SURA YA TANO
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imejihusisha na muhtasari wa tasnifuhii kwa kuangazia makisio na malengo ya uchanganuzi huu. Mtafiti amejadili alivyotimiza madhumuni ya utafiti na vilevile kuthibitisha makisio yaliyoongoza utafiti huu. Hatimaye mtafiti ametoa mapendekezo mbalimbali kwa mujibu wa maswala yaliyozuka kutokana na utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari

Katika utafiti huu, mtafiti amechunguza suala watoto katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zilizoandikwa na Mohamed Suleiman Mohamed, *Rosa Mistika* na *Kichwa Maji* zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Azimio kubwa la utafiti huu lilikuwa kwanza ni kuchunguza usawiri wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Utafiti huu ulijikita katika vipengele mbalimbali. Hizi ni haki za kimsingi ambazo watoto wamenyimwa katika riwaya zilizochunguzwa. Vipengele hivi ni, kufukuzwa nyumbani, kutosomeshwa na wazazi wao, kudhulumiwa kimapenzi, kupokonywa urithi, kubaguliwa kielimu na kuchapwa bila sababu.

Vilevile, utafiti huu ulibainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya zilizoteuliwa. Hapa, mtafiti alichunguza majukumu yanayotekelezwa na watoto kwa kuyagawanya katika vikundi mbalimbali. Mwisho, uchunguzi huu ulikusudia kutambua mielekeo ya wahusika matajiri na watu wazima kwa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Hizi ni riwaya zilizoandikwa kati ya 1970 na 1980. Riwaya hizi zilijihusisha na uongozi wa usaliti wa kisiasa. Katika tasnifu hii mtafiti amedondoa usawiri wa watoto na kuzingatia haki za watoto. Mtafiti alichagua vipengele vya kuchanganuliwa kutokana na vipengele anuwai vinavyoweza kuchanganuliwa katika riwaya. Sababu kuuya kufanya hivi ni kufanikisha malengo ya utafiti huu. Vipengele vilivyochanganuliwa na mtafiti ni uwakilishi wa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili, majukumu wanayotekeleza watoto katika riwaya nne teule za kisasa za Kiswahili na mielekeo ya watu wazima kwa watoto. Mtafiti ametimiza madhumuni ya uchunguzi huu kwa kumulika haki wanazonyimwa watoto na wanajamii ambazo ni: kufukuzwa nyumbani, kunyimwa uhuru wa kutangamana na marafiki zao, kutosomeshwa na wazazi wao, kupokonywa urithi, na kudhulumiwa kimapenzi. Nadharia ya uhalisia ilitumika katika utafiti huu. Ilidhihirika kuwa uhalisia kama

ulivyotumiwa na waandishi husika ni mbinu muhimu katika uwasilishaji wa ujumbe kwa wasomaji.

### 5.3 Hitimisho

Uchunguzi huu uliongozwa na makisio yafuatayo ambayo yaliibuka kutokana na madhumuni ya tasnifu hii. Kwanza, watoto huwakilishwa kwa njia duni katika riwaya zilizochunguzwa. Pili, baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya zilizochunguzwa ni ya aibu sana. Mwisho ni kwamba, baadhi ya wahusika matajiri na watu wazima wana mielekeo hasi kwa watoto. Katika sehemu hii, mtafiti alihitimisha uchunguzi wake kwa kuegemea madhumuni ya utafiti huu kama ifuatavyo:

#### 5.3.1 Kuchunguza Uwakilishi wa Watoto katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili.

Imedhihirika kuwa, watoto wamewakilishwa katika njia isiyofaa. Imejitokeza wazi kuwa, watoto hawajapewa nafasi mwafaka katika kazi zilizochunguzwa wakilinganishwa na watu wazima. Katika uchunguzi huu, mtafiti aligundua kuwa kuna haki za kimsingi ambazo watoto wamenyimwa. Haki hizi ni kama vile: kutolishwa vizuri, kufukuzwa nyumbani na wazazi na hata wanajamii, kutosomeshwa, kudhulumiwa kimapenzi, kupokonywa urithi na kuchapwa bila sababu. Hata hivyo kuhusiana na suala la masomo, kuna wale waliosomeshwa na wazazi wao hadi vyuo vikuu na kuna wale waliopuuzwa. Kwa mfano, mhusika Kazimoto katika riwaya ya *KichwaMaji*, alisoma hadi chuo kikuu ilhali ndugu zake wadogo hawakuweza kusoma kama yeye. Mhusika Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* hakusomeshwa lakini ndugu zake wa kambo Salma na Samir walisomeshwa vizuri hata mmoja wao akaenda ng’ambo.Vilevile, kuhusiana na suala la kupokonywa urithi, kuna wale waliowatakia watoto mazuri. Kwa mfano, Bi Kiza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* anamhimiza Rehema kwenda kudai haki yake.

#### 5.3.2. Kubainisha majukumu yanayotekelezwa na watoto katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili.

Kuhusiana na kipengele cha majukumu, utafiti huu umebainisha kuwa watoto wanahusishwa na majukumu kadhaa. Wengi wao wanalazimika kutekeleza majukumu hayo kwa sababu ya hali yao ya maisha-yaani wazazi wengi hawawezi kuwatimizia mahitaji yao ya kimsingi na hivyo inabidi wajiingize katika majukumu kama vile ya ukahaba, kupika pombe,wizi nakulima, ili kuyaendeleza maisha yao ya kila siku. Uchunguzi huu pia uligundua kuwa malezi ya mtoto akiwa mchanga huamua hali yake ya baadaye.

Vilevile, iligunduliwa kuwa uamuzi wa wazazi bila kuwahusisha watoto wao kulipelekea watoto kutekeleza majukumu duni. Kwa mfano, Kidawa katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* aliozwa na wazazi wake akiwa mdogo sana-kabla hajaota hata chuchu. Kuozwa bila hiari yake kulimfanya kudai talaka na kutorokea mjini ambapo alijiunga na ukahaba. Wazazi hawakuwa na hamu ya kuwasomesha watoto wao. Aidha, mhusika Zakaria licha ya kuwa mwalimu, hakutaka kumlipia bintiye Rosa karo ya shule. Hili linamlazimu Rosa achimbe eka moja ya shamba la mihogo iliauze ndio apate karo ya shule. Watoto wengine wanaachishwa kwenda shule ili wamsaidie Rosa kulima kipande cha shamba cha eka moja. Eka moja ni sehemu kubwa inayostahili kulimwa na trekta au watu wazima lakini si watoto wadogo. Suala hili linakuwa na athari kwa watoto hawa kwa sababu hawatilii elimu maanani na ndio maana Flora anapoanguka mtihani katika shule ya sekondari hajali. Honarata naye baadaye anaacha shule akiwa katika shule ya msingi. Mzazi huyu alikiuka haki za watoto kwa sababu aliwafanyiza kazi nyingi kuzidi uwezo na umri wao.

Jukumu lingine linalotekelezwa na watoto kulingana na matokeo ya utafiti huu ni jukumu la kupika na kuuza pombe. Rosa alipostahili kwenda shule ya upili, babake aliiba pesa zilizouzwa ng'ombe. Kutokana na mapenzi ya mamake kwa wanawe, aliamua kupika pombe ili auze apate karo ya Rosa. Katika kazi hii yote alimhusisha Rosa na dada zake. Dada zake wadogo wanakosa kuhudhuria masomo ili wasaidie kuchota maji na kuosha vyombo siku ya kuuza hiyo pombe. Hata kama ni kutokana na mapenzi, mama yao aliwahusisha katika upishi na uuzaji wa pombe na hivyo alikiuka haki za hawa watoto. Alistahili kushtakiwa kwa sababu baadaye hawa watoto hasa Rosa na Flora wanakuwa walevi wa kupindukia. Vilevile, wale wadogo kama Honarata na Stella ndio waliona vitendo vya walevi kwa mara ya kwanza. Vitendo kama vile kukojolea maua na ukuta wa nyumba yao hadharani. Huu ni ukiukaji wa haki za watoto wakati wanaona uchi wa watu wazima.

### 5.3.3. Kutambua mielekeo ya wahusika matajiri/watu wazima kwa watoto katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

Katika kuchunguza mielekeo ya matajiri na watu wazima, mtafiti amebainisha kuwa matajiri na watu wazima wana mielekeo hasi kuwahusu watoto. Mtafiti alitumia msamiati, vifungu vya maneno na sentensi kugundua haya. Watu wazima wanatumia neno “malaya”kurejelea wahusika watoto katika riwaya zilizochunguzwa. Wahusika hawa ni: Rukia katika riwaya *Kichwa Maji*, Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rehema katika riwaya ya *Nyota ya*

*Rehema* na Bahati katika riwaya ya *Kiu*. Ni jukumu la kila mtu mzima kuwapa watoto mwelekeo wanaostahili kuufuata maishani. Watu wazima hawakutumia muda wao hata kidogo kuwaonyesha watoto ubaya wa kushiriki mapenzi na watu wazima kabla ya ndoa. Hii inadhihirisha wazi kuwa watu wazima walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto.

Mhusika Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji* anaitwa "mwehu" tena anaitwa "nunda." Maneno haya yanaonyesha kuwa watu wazima wana mielekeo hasi kwa watoto. Tabia za mtoto Kalia zinachangiwa na hali mbaya ya kiuchumi katika jamii anamoishi. Aidha, kuiga mienendo ya kakake mkubwa ambaye ni Kazimoto kulisababisha Kalia kuwa na tabia mbaya.

Aidha neno "mkorofi" limetumika kumrejelea mhusika Kalia katika riwaya ya *Kichwa Maji*. Hii inadhihirisha mielekeo ya watu wazima kuwahusu watoto. Uchunguzi huu uligundua kwamba tabia za mhusika huyu zilisababishwa na mkubwa wake- Kazimoto pamoja na watu wazima kama vile Tegemea, mwanamke aliyezoea kushiriki mapenzi na Kaliana hatimaye kudai malipo kutoka kwa Kalia. Ilimbidi Kalia kuiba pesa za kumpelekea mwanamke huyu. Kwa hivyo, tabia zake zilisababishwa na watu wazima.Vifungu vya maneno katika riwaya zilizochanganuliwa pia vilionyesha mielekeo ya matajiri na watu wazima. .

Sentensi kadhaa katika riwaya zilizochanganuliwa zilitumika kutambua mielekeo ya watu wazima kuwahusu watoto. Utafiti huu uligundua kuwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* Zakaria hakutaka kuwalipia karo binti zake. Zakaria hakujali masomo ya watoto wake na kwa hivyo alikuwa na mielekeo hasi.

Utafiti huu ulitambua kuwa watu wazima walitumia lugha chafu kwa watoto.Katika riwaya zilizochunguzwa, wahusika wengi watoto waliitwa malaya. Huu ulikuwa udhaifu wa hali ya juu kwa sababu watu wazima wanastahili kuwaelekeza watoto na wala si kuwatukana kama walivyofanya katika kazi zilizochunguzwa. Matusi haya yote, yanaonyesha kuwa watu wazima waliwaona watoto kama malaya kwa hivyo walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto.

Watu wazima waliwaajiri watoto kuwafanyia kazi licha ya kuelewa vizuri umri wao. Rehema alipotoroka kwao, aliajiriwa kwa Mansuri. Utafiti huu uligundua kuwa Mansuri alikuwa na nia ya kumtaka Rehema lakini alijifanya kuwa alimhitaji Rehema kwa ajili ya kumlea mwanao. Mielekeo ya Mansuri na mkewe Rozi ilikuwa hasi kwa watoto.Vilevile, watu wazima waliona kama vijana ndio walisababisha maafa katika jamii. Hili ni dhihirisho kuwa

wazazi walikuwa na mielekeo hasi kwa watoto. Wazazi wa kike walionekana kuwa na upungufu wa kukosa kuwaambia binti zao kujilinda kutokana na mimba za mapema. Vilevile, katika riwaya ya *Rosa Mistika*, Rosa na dadake Flora wanapata mimba wakiwa shuleni na wanaziavya palepale shuleni.

Kwa ujumla deta iliyokusanywa imemwezesha mtafiti kuthibitisha madai ya jarida la UNICEF (1991) linalosema hivi;

> "Zaidi ya asilimia ishirini ya watoto katika Afrika Mashariki na Kusini wananyimwa haki zao za kimsingi.Watoto wanaajiriwa kwa sababu za kiuchumi. Asilimia sabini na tano ya wanaofanya kazi ni wale walioajiriwa katika familia, shamba au nyumbani.''

Aidha, mtafiti aliweza kuthibitisha madai ya King'ala (1986) anayedai kwamba;

> "watoto wengi hufanywa kuwa watumwa nakuwa wao hupagazwa na masharti mengi ya wazazi wao."

Matokeo ya uchanganuzi huu yalithibitisha ukweli wa baadhi ya mihimili iliyotumika katika utafiti huu. Kuhusiana na suala la msanii kuonyesha ukweli wa maisha katika jamii, kazi za watunzi wote wawili zilidhihirisha hili. Hii ni kwa sababu wanazungumzia kuhusu kuzaliwa, kukua na hata kufa kwa baadhi ya wahusika. Vilevile, wanajihusisha na shughuli za kila siku kama vile; kulima, kusoma, kwenda sokoni, kuwapeleka mifugo malishoni n.k.

Kupitia usanii wa watunzi hawa wawili, wanajamii wanaelewa mila na tamaduni zao. Kwa mfano, ni wanawake na wasichana ambao wanafanya kazi za nyumbani kama vile kuchota maji na kupika.

Mandhari yaliyotumika na watunzi wote wawili yanalingana na maelezo na majukumu katika riwaya zilizochunguzwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rosa Mistika*, tunaonyeshwa watoto ambao wanatekeleza majukumu ya kuuza pombe wakiwa katika sehemu za mashambani, wanaishi nyumba ambazo zinavuja. Katika riwaya ya *Kichwa Maji*, tunaonyeshwa wahusika watoto wakishiriki ukahaba katika maeneo ya mjini. Aidha, kuhusiana na usawiri wa wahusika, watunzi wote wawili waliwapa wahusika sifa za binadamu wa kawaida kutokana na vile wamewachora. Hivyo basi, nadharia hii ilifaa sana katika uchanganuzi huu.

### 5.4 Mapendekezo

Imebainika, kutokana na uchunguzi huu kwamba watoto hudhulumiwa kuegemea hali yao ya kijinsia, rangi yao nyeusi, na uchumi wa wazazi wao. Vilevile, imebainika kuwa waandishi hutumia kazi zao za fasihi kufichua uovu unaofanyika katika jamii. Uovu kama vile ulevi,

kuavya mimba, mauaji, ukahaba, kudhulumiwa kwa watoto kimapenzi na kuwapokonya urithi.

Kuna masuala anuwai yanayoweza kuchunguzwa katika riwaya. Mtafiti alichunguza uwakilishi wa watoto katika riwaya za miaka ya sabini. Kwa sababu ya muda na upeo wa utafiti ambao haungemruhusu kushughulikia mambo mengi, mtafiti amependekeza yafuatayo:

Pana haja ya watafiti chipukizi kufanya utafiti zaidi. Wanaweza kulinganisha na kulinganua uwakilishi wa watoto katika riwaya za miaka za kufunga karne ya ishirini na zile zilizoandikwa katika karne ya ishirini na moja. Katika kufanya hivi, watachunguza kama nadharia ya uhalisia bado ingali inatumiwa na waandishi wa kisasa kuwasilisha ujumbe wao katika fasihi.

Uchunguzi zaidi unaweza kufanyiwa riwaya zilizochunguzwa, yaani *Kichwa Maji*, *Rosa Mistika* ,*Nyota ya Rehema* na *Kiu* ili kutambua tamathali za semi zilivyotumika katika uwakilishi wa watoto. Aidha, riwaya tofauti za mtunzi mmoja au waandishi tofauti zinaweza kuchunguzwa. Ikizingatiwa kwamba uchunguzi huu ulijikita katika riwaya zilizoandikwa na wazaliwa wa Tanzania pekee, pana haja ya utafiti zaidi kufanywa ili kuchunguza usawiri wa watoto katika tamthilia au riwaya zilizoandikwa na watunzi wazaliwa wa Kenya na kuona kama usawiri wao wa watoto unafanana na usawiri wa watoto katika riwaya zilizoandikwa na watunzi wa nchi nyingine za Afrika Mashariki mathalan nchi ya Kenya.

# MAREJELEO

American Psychological Association (APA) 1994 *Publication Manual Psychological* Association (4th ed). Washington, DC: Author

Anderson, D.A. (2005). Gender Role Stereotyping of Parents in Children's Picture Books: The Invisible Father. Sex Roles, 52, 3-4.

Austen, J. (1975). *The Bicentenary of JaneAusten Birth:* Codex Publishers.

Bowen, D. (2003). "Usawiri wa Wahusika Watoto katika Tamthilia Zilizopendekezwa katikaShule za Upili: Visiki na Amezidi". M. A.ChuoKikuu cha Egerton. [Haijachapishwa].

Buttner, C. (1894). *Anthologie aus der Suaheli-Literatur*. Berlin: Verlag von Emil Felber.

Burnett, F.H. (1905). *A Little Princess*. OxfordUniversity Press.

-----------------(1911). *The SecretGarden*. OxfordUniversity Press.

Carol, B. (1997). *The State of the World's Children.*USA: OxfordUniversity Press.

Chacha, D. (1986). "Mazingira ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili; RosaMistika wa Kezilahabi". Makala katika mwamko Vol. 3 Chama cha Kiswahili; ChuoKikuu cha Nairobi.

Derek, L. (1990). *The Realist Image in Social Science.* London: The Macmillan Press Ltd.

Dickens, C. (1978). *Sketches by Boz Illustrative of Every-Day Life and Every-Day People*. London; OxfordUniversity.

Edward, S. (1870). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar*(Utangulizi), London.

Ernst, S. B. (1995). "Gender Issues in books for Children and Young adults." In S Lehr (Ed.) Battley dragons: Issues and Contraversy in Children's Literature. Portsmouth, NH: Heinmann [ED 379 657]

Forster, E.M.(1927). *Aspects of the Novel Penguin books*: Harmounds.

Fox, M. (1993)."Men who weep, boys who dance, The Gender Agenda Between the Lines in the Children's Literature" Language Art.

Grenby, M. O. (2008). *Children's Literature*. Edinbrg: Edinburg University Press.

Gwachi, J.M. (1991*). "*Ukengeushi wa wasomi Katika riwaya za Euphrase KezilahabiTasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Harry, B. (1991). *A History of Literary Criticism.* London: The Macmillan Press Ltd.

Hegels, G. W. F. (1998). *Aesthetics.*OxfordUniversity Press.

Himes, J.R. (1996*).* "The Implementing Convention on Rights of the Child Resource Mobilization in Low Income Countries" (UNICEF). *Jarida la FOOTSTEPS NO. 38 MARCH 1999 CHILD PARTCIPATION.* Vision for Children.

Hunt, P. (1991). *Critism Theory and Children's Literature*. Oxford: Black well.

----------- (1994). *An Introduction to Children's Literature*. New York: Oxford University Press.

----------- (1996). *International Companion Encyclopaedia of Children's Literature*. London: Routledge.

----------- (1996). *Defining Children's Literature and children.In P. Hunt (Ed.), International Companion Encyclopaedia of Children's Literature*. London: Routledge.

--------- (2001). *Children's Literature*. Oxford: Blackwell.

Ikambili, H.M. (1997). *Mwongozo wa Visiki*. East African Educational Publishers Ltd., Nairobi.

Jett, S., & Masland, S. (1993). *"*Girls are not dodo birds! Exploring Gender Equity Issues inthe Language Arts Classrooms*".* Language Arts.

John ,S. (1992a) "Advocating for Multiculturalism: Migrants in Australian Children's Literature after 1972", Children's Literature Association Quarterly.

John, S. (1992b). *Long Land Ideology in Children's Fiction*. Longman: London.

Kamunde, M. (1983). "Kilio cha Wanyonge Katika Riwaya za Said A. Mohamed". Tasnifu ya M.A.Chuo Kikuu cha Nairobi. [Haijachapishwa].

Kanga, M. N. (2005). *Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto Katika Shule za Msingi Nchini Kenya.* M.A.Thesis. Kenyatta University.

Karin, L.O. (1994). *Children's Literature: Criticism and the Fictional Child*.
Oxford: Clarendon Press.

Kavoi, M. (1996). "Muwala wa Vipengele vya Fani: Uhakiki wa kazi za S. A. Mohamed." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Egerton. [Haijachapishwa].

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

------------------(1974). *Kichwa Maji*. Nairobi: East Africa Publishing House.

Khamis, S. A. M. (2005). "Vionjo Vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." Research in African Literatures 36/1: 92-108.Bayreuth: BayreuthUniversity.

--------------- (2007). "Utandawazi au Utandawizi: Jinsi Lugha ya RiwayaMpya ya Kiswahili inavyodai." African Journalism Online Vol 70:

Kihore, Y.M. na Chuwa, A.R. (2004). *Kiswahili KatikaKarne ya Ishirini na Moja.*
Dar esSalaam: TUKI.

King'ala, Y. M. (1986). *Mbinu za Fasihi Uchambuzi wa Riwaya na Tamthilia.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kitsau, J. (1980). *Uasi*. Oxford University.

King'ei, K. (1996). *Mwongozo wa Buriani*. Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Lesnik, O. K. (1994). *Children's Literature*: Criticism and the Fictional Child. Oxford: Clarendom.

---------------- (2004). *Children's Literature*: New Approaches. London: Palgare.

Longhorn. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Luckacs, G. (1979). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

Lugano, R.S.(1989). ``MwanamkeKatika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya M .A . Chuo Kikuu cha Nairobi. [Haijachapishwa].

Lissa, P. (1987). "*Enigma Variations What Feminist Theory Knows About Children's Literature*" Signal 53: 186-201.

Marcas, M.(1998). *The Case of Peter Rabit*; *Changing Conditions of Literature for Children*. New Torie and London: Garland.

Marilyn, B. (1990). *JaneAusten and The War of Ideas*. USA: Oxford University Press.

Mazrui, A.M. na Syambo, B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

McGills, R. (1996). *The Nimble reader*. *Literary Theory and Children's Literature*. New Taki: Twaynes publishers.

Mdee, J. S. Et al. (2000). *English – Swahili Dictionary.* Dar es Salam: TUKI.

----------------- (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salam: TUKI.

---------------- (2011). *Kamusi ya Karne 21*. (toleo la pili) Longhorn Publisher.(K) Ltd. Nairobi.

Mlacha, S. A. K (1999). *Kamusi ya Sheria* : *Kingereza –Kiswahili*. Tanzania: Dar-es Salaam.

--------------- (1986). "Uprooting the Traditional Culture." Africana Mar Bugensia 2/86, Frankfurt.

--------------- (1971*). A Structural Study of the Novel.* Educational Sermas Centre L.t.d. Dar-es-Salaam.

---------------- (1986*). "*The Imagery of Conflict in The Novels of Kezilahabi"Kiswahili54: DaresSalaam.

----------------- (1993). "Kiswahili Prose fiction and the Society" E.P.D Dar-es-Salaam.

----------------- (1984). Riwaya za Visiwani *(1970- 1980*) na Ujenzi Riwaya za wa Jamii Mpya."Wahariri: Mbogo, E. na Mdee, M. S. MULIKA16, TUKI.

------------------ ( 1985). “Wahusika katika riwaya za Kiswahili Tanzania.” ( 1970-1982). MULIKA 17, TUKI.

Mohamed, S. M. (1976). *Nyota ya Rehema.* Eastern Africa: Oxford University Press.

----------------------(1972). *Kiu*. Nairobi: East Africa Publishing House.

Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

------------ (1977). *Asali Chungu.* Shungwaya Publishers, Nairobi.

---------------- (1980). *Dunia Mti Mkavu.* Nairobi: Longman.

-----------------(1981) ``Kupatana na Riwaya zangu.” Mwamko 2. Jarida la Chama cha Kiswahili chuo kikuu cha Nairobi.

---------------- (1988). *Kiza katika Nuru*. Nairobi: Oxford University Press.

---------------- *(1988). Pungwa.* Nairobi:Oxford University Press.

---------------- (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longman.

--------------- (1990). *KivuliKinaishi*. Nairobi: OxfordUniversity Press.

--------------- (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Montgomery, L.M. (1985). *The Selected Journals of L.M. MontgomeryCanada*: OxfordUniversity Press.

Mpesha, N. (1996). *Children’s Literature in Tanzania*: A Literary Appreciation of its Growth and Development. PhD. Dissertation. Kenyatta University.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East Africa Education Publishers.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: ACTS.

Mukobwa, M. (1986). *Uhakiki wa Fasihi Unahusu Nini?*Katika *Mwamko*3, Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi, 44-63.

Murning, G.W. (2007). *Children of Resoluton.* England: Legend Press Indepent Book Publisher.

Musau, P. (1985). “Euphrase Kezilahabi : Mwandishi Aliyekata Tamaa”. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. [Haijachapishwa].

Mutua, J. M. (2013) “Uchanganuzi wa Fantasia Katika Hadithi za Watoto za Nyambura Mpesha” Tasnifu ya M. A.Chuo Kikuu cha Egerton. [Haijachapishwa].

Ndung’o C.M. (1998). *African Oral Literature: A case of Kikuyu and Kiswahili Proverbs.* PhD. Thesis of Kenyatta University.

Nganje, D. K. (1993). *Mwongozo wa Masaibu ya NduguJero.*Nairobi: Kenya Literature Bureau.
Ngugi, P. (2009a). *TheRole and Place of Children's Literature in Kiswahili in KenyanPrimary Schools*. Published Conference Paper.
Ngugi, P. (2009b). *Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya.*PhD. Dissertation. University of Venna.
Ngugi, T. (1981).*Writers in Politics*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Phoenix Publisher. Nairobi
Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Kisasa za Kiswahili*.Zanzibar: Nairobi University Press.
Njogu, K. na Chimerah, R. (1997). *Ufundishaji wa Fasihi*, *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JomoKenyatta Foundation.
Nodelman, P. (1990). *Words about Pictures:The Narrative Art of Children Picture Books*. Athens, Ga: U. Georgia press.
------------- (1992). *The Other Orientalism, Colonialism and the Children's Literature*. Children's literature Association Quaterly 17:29 35: GeorgiaPress.
-------------- and Reimer, M. (2003). *The Pleasures of Children's Literature. 3rd Edition*. Boston: Ally na Bacon.
Nodelman, P. (2005). *Bibliography of Children's Literature Critisism* : Georgia press.
Nozick, R. (1974). *Anarchy, State and Utopia*. Blackwell: OxfordUniversity.
Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL 61201.
Nyaigoti C. N. (1982). *Mke Mwenza*. Heinemann Educational Publishers, Nairobi.
Okin, S. M. (1989). *Justice, Gender and the Family*. New York: Basic Books.
Ongeti, K.I. (1984). *Visiki*. East African Educational Publishers Ltd., Nairobi.
Robert, S. (1991). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Mkuki na Nyota Publishers. Dar es Salaam.
Rose, J. (1992). *The Case of Peter Pan or the Impossibility of Children's Fiction*. Philladelphia: University of Pennsylvania Press.
Rose, L. (1991). *The Erosion of Childhood: Child Opression in Britain 1860-1918.* Canada: Routledge.
Rudman, M. (1995). Children's Literature: An issue approach. (3rd edition). White Plains, AY: Longman [ED 379 684].
Sen, A. (1992). *Inequality Reexamined* Cambridge, M. A: HavardUniversity Press.

----------(2009). *The Idea of Justice*. Cambridge: HavardUniversity Press.

Smart, S. M. And Smart, C. R. (1997). *Children Development and Relationship*:Fourth edition.

Somba, J. N. (1969). *Alipanda Upepo na Kuvuna Tufani*. Nairobi: Heinmann Education Books.

Soyinka, W. (1974). Masaibu ya Ndugu Jero (Mtafsiri A. S. Yahya) Nairobi: Oxford University Press.

Syambo, B. (1997). *Mwongozo wa Visiki*. Nairobi: Mc Millan Kenya Ltd.

Tasson, P., Beith, K., Eldridge, H., Gough, A. (2002). Diploma in Child Care and Education. USA: Heinman Education Publishers.

Taylor, C. (1996). Sources of the Self Making of the Modern Identity. Great Britain: Alhenaeum Press Ltd.

Taylor, R. (1981). Understanding the Elements of Literature. London: Macmillan.

Temple, C. (1993). "What if 'Beauty' had been ugly?''Reading Against theGrain of Gender Bias in Children's Books: Language Art.

TUKI. (2006). English- Swahili Dictionary(Toleo la tatu). Dar es Salaam: Oxford University Press.

Velten, C. (1907). Alfu- Lela Ulela, Walter Deeruyler ISSN 0014-6242

--------------(1907). Prosa and Poesie. Berlin: Selbstverlag.

Walibora, K. (2010) "Uhalisia na uhalisia Mazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum" SWAHILI FORUM 17 Mainz: Johannes Gutenberg University.

Wamitila, K. W. (2002). Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake. Nairobi: Phoenix Publishers.

----------------- (2003). Kamusiya Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publications Ltd.

----------------- (2004). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: English Press.

---------------- (2010) Kazi ya Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wandera, S.P. (1996). Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: (1800-1900). Uhalisi au Ugandamizaji. Tasnifu ya M.A.ChuoKikuu cha Egerton. [Haijachapishwa].

Warren, A. na Welleck, R. ( 1986). Theory of Literature and Literary Criticism. Midlesex; England: Penguin Books.